# KUCHAGUA MCHUMBA
## Njia Tukufu Yenye Kupendeza

**Kimekusanywa na:**
ABBAS NA SHAHEEN MERALI

**Kimetarjumiwa na:**
SALMAN SHOU

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 – 9987 – 17 – 098 – 2

**Kimekusanywa na:**
ABBAS NA SHAHEEN MERALI

**Kimetarjumiwa na:**
SALMAN SHOU

**Kimehaririwa na:**
Alhaj Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Machi, 2016
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

**KWA KUSHIRIKIANA NA:**

The World Federation of KSIMC,
Islamic Centre, Wood Lane, Stanmore,
Middlesex, HA7 4LQ, United Kingdom.
**Tel:** +44 (0) 20 8954 9881 | **Fax:** +44 (0) 20 8954 9034
**Barua Pepe:** secretariat@world-federation.org
Registered Charity in the UK No. 282303

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ........................................................................ 1

Utangulizi.......................................................................................... 4

**SURA YA 1: MUUJIZA WA NDOA ........................................... 9**

Uhusiano wa Kwanza wa Binadamu ............................................... 9

Uzuri wa Ndoa - Kwa nini nifunge Ndoa? ................................... 10

Vikwazo Kwenye Ndoa ................................................................. 16

**SURA YA 2: NITAJUAJE KAMA NIPO TAYARI ................ 22**

Kigezo .......................................................................................... 22

Ishara za Dhahiri ........................................................................... 22

**SURA YA 3: NIANGALIE NINI KWA MCHUMBA? .......... 31**

Umuhimu wa Kuchagua Mchumba .............................................. 31

Ni Nani Niwezaye Kumuoa? ......................................................... 32

Kigezo cha Kiislamu...................................................................... 32

**SURA YA 4: KANUNI MUHIMU ZA KI-FIQH: .................. 40**

Sehemu ya 1- Mlolongo wa Uchunguzi: ....................................... 40

Mchakato wa Uchunguzi Katika Uislamu ..................................... 40

Kanuni za Uchunguzi..................................................................... 40

Kanuni za Kuchanganyikana ......................................................... 42

Hitimisho........................................................................................ 43

**SURA YA 5: MBINU ZA KUCHAGUA MCHUMBA........... 45**

Mbinu za Kuchagua Mchumba katika Uislamu............................ 45

Nitampatataje Mtu Ambaye Nadhani Atanifaa? .............................. 46

Nitawajuaje Ili Niweze  Kufanya Uamuzi? .................................. 49

Kuupinga Mchakato...................................................................... 49

**SURA YA 6: HAJA YA KUJIANDAA...................................... 58**

Umuhimu wa Kujiandaa ................................................................ 58

Kijue Unachokitafuta ..................................................................... 58

Tambua Unachotaka Kuuliza......................................................... 58

Kuhakiki Maadili na Utu ............................................................... 58

Mambo ya Kuzingatia.................................................................... 58

**SURA YA 7: BAADA YA MAWASILIANO YA KWANZA... 81**

Nini Kinachotokea Baadaye?...........................................................

Shinikizo la Nje.............................................................................. 83

**SURA YA 8: NITAJUAJE? ...................................................... 85**

Hisia Kwambazo ‘Unajua  Ndani’ tu ............................................ 85

Ishara za Dhahiri .......................................................................... 85

Umuoe Rafiki, Sio Mpenzi ........................................................... 85

**SURA YA 9: ISTIKHARA...................................................... 100**

Istikhara ni Nini?.................................................................... 100

Matumizi ya Istikhara Katika Kuchagua Mchumba .................. 100

Matumizi Mabaya ya Istikhara .................................................. 101

Matumizi Sahihi ya Istikhara ..................................................... 101

Maoni ya Maulamaa Mashuhuri Juu ya
Matumizi ya Istikhara ................................................................ 105

**SURA YA 10: KUMTEGEMEA MWENYEZI MUNGU.... 108**

Kukabiliana na Matatizo Yenye Uwezekano .............................. 108

Taasisi ya Ndoa ......................................................................... 108

Umuhimu wa Swala ya Rakaa Mbili ......................................... 111

Umuhimu wa Tawassuli Kutoka Kwa Maasumin....................... 111

Du’a Zilizopendekezwa .............................................................. 115

**SURA YA 11: KITU GANI KIFUATACHO? ....................... 118**

Njia ya Kusonga Mbele .............................................................. 118

Posa ........................................................................................... 118

**SURA YA 12: KIPINDI CHA UCHUMBA........................... 120**

Baada ya Uamuzi ....................................................................... 120

Kwa Nini Uwe na Kipindi cha Uchumba? ................................ 121
Kipindi cha Uchumba Kiwe Kwa Muda Gani? .......................... 122
Ndani ya Kipindi cha Uchumba................................................ 122
Je! Nimefanya Uamuzi Sahihi? ................................................ 126
Itakuwaje kama Mambo Hayaendi Sawa?................................. 132

**SURA YA 13: KANUNI MUHIMU ZA KI-FIQH: .............. 134**

Sehemu ya 2 - Kipindi cha Uchumba ........................................ 134
Kanuni za Kipindi cha Uchumba.............................................. 134
Uchumba Uliovunjika.............................................................. 135

**SURA YA 14: VIPI IWAPO KAMA ..................................... 137**

Huwezi Kumpata Huyo Anayefaa?........................................... 137
Uwe na Imani........................................................................... 137

**SURA YA 15: KUCHAGUA MCHUMBA ............................ 139**

Baada ya Talaka ...................................................................... 139
Kusonga Mbele Baada ya Talaka............................................. 139
Lini Nianze Kukutana na Watu Tena?...................................... 140
Mchakato Ni Upi?.................................................................... 143
Yupi Unayepaswa Kumuoa?.................................................... 143
Vikwazo Vinavyowezekana Kuwapo........................................ 147



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 6 10/20/2015 4:31:54 PM

Mambo Yenye Msaada ........................................................ 148

Kukutana ........................................................................ 148

Kufanya Uamuzi ............................................................... 151

Uhusiano Huo Mpya ........................................................... 152

**SURA YA 16: MIKATABA ................................................ 154**

Mikataba Katika Uislamu ................................................... 154

Mut`a (Ndoa ya Muda) ......................................................... 154

Nikah (Ndoa ya Kudumu) ..................................................... 154

Mahari - Zawadi kwa Mke .................................................... 160

Mkataba wa Yaliyo Kabla ya Ndoa ......................................... 162

THE WORLD FEDERATION

OF KHOJA SHIA ITHNA-ASHERI MUSLIM COMMUNITIES

"Uchapishaji wa kitabu hiki umewezekana kupitia msaada mkubwa wa Jumuiya ya Kimataifa ya The World Federation of Khoja Shia Ithna Asheri Muslim Communities."

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni mkusanyiko wa mada mbalimbali zikiwemo kuchumbia, mikataba ya ndoa, talaka n.k. Kitabu hiki kimetarjumiwa kwa Kiswahili kutoka lugha ya Kiingereza.

Licha ya kuwepo hadithi na riwaya nyingi za Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na Ahlul Bait (a.s.) wake zenye kusisitiza umuhimu wa ndoa ambazo zinaweza kuwatia hamu vijana wajiharakishe katika kuoa, kwa bahati mbaya, vijana wengi ambao wamefikia umri wa kuoa huchelewa kuchukua hatua ya kuelekea kwenye ndoa, hatua ambayo ina uzito mkubwa sana hivyo kwamba inabeba nusu ya imani ya dini yake.

Kwa kufikiri kwa undani zaidi, ni dhahiri kwamba ucheleweshaji huu hausababishwi na hali ya utepetevu au kudharau thamani ya ndoa; kwa usahihi zaidi, inaonyesha yapo matatizo katika mbinu zinazotumika ambazo kwazo vijana hutafutia wachumba wanaofaa. Katika baadhi ya mifano, mbinu huonekana za bandia na zisizoathiriwa na hisia, kama vile kutoa maelezo binafsi kwa washenga wasiojulikana. Katika mifano mingine, huduma za ushenga za kimila hutumika lakini hii husababisha ukatishaji tamaa kupitia majaribio ya mara kwa mara yaliyoshindikana. Mwishowe, hali hii huwaelekeza vijana kukata tamaa juu ya mfumo huo. Kwa wengine, mchakato wote unaweza kuwa wa kutisha kiasi kwamba wanaamua kufanya usirisiri. Kwa bahati mbaya, katika kadhia nyinginezo, sababu zilizotajwa hapo juu huishia kuwafanya vijana waamue kutumia mbinu mbadala za kutafuta mchumba, ambazo si zote ni halali, au hata kuwa zenye mafanikio kwa kipindi kirefu.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 1 10/20/2015 4:31:54 PM

Mchakato wa kutafuta mchumba anayefaa kwa vyovyote vile sio uliyonyooka na rahisi. Hata hivyo, hii haina maana kwamba mchakato lazima uwe wa kutisha na kuchosha kama unavyokuwa nyakati zingine. Kitabu hiki kinalenga kumwandaa mtu kuwa katika njia ya kutafuta mchumba akiwa na taarifa zinazotakiwa na mwongozo katika kila hatua ya mchakato huo.

Kitabu kinaanza kwa kusisitiza uzuri wa ndoa, na kutambulisha sababu kwa nini mtu anahitaji kuanza safari hii ya kutafuta 'mwenza'. Vikwazo vinavyowezekana ambavyo watu wanasema kwamba ni vyenye vipingamizi vimeshughulikiwa na ufumbuzi unaowezekana pia umetajwa. Halafu hii inafuatiwa na njia za kutambua iwapo kama mtu yupo tayari kuchukua hatua hii ya kuoa au hapana, kwa kuangalia vigezo vya Kislamu na pia dalili za dhahiri.

Hii ni moja kati ya kazi kubwa zinazofanywa na Taasisi ya Al-Itrah katika kuwahudumia kielimu wasomaji wake wazungumzaji wa Kiswahili. Na kwa maana hiyohiyo, imeona ikichapishe kitabu hiki chenye hazina kubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo lake lilelile la kuwahudumia Waislamu, hususan wanaozungumza Kiswahili.

Hivyo, ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufaika vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwani tumekiona ni chenye manufaa sana hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Tunawashukuru waandishi wa kitabu hiki, Abbas na Shaheen Merali kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa ajili ya Umma huu wa Waislamu, Allah *'Azza wa Jallah* amlipe kila kheri na amuingize Peponi kwa salama na amani insha'Allah. Shukrani zetu za dhati ziwaendee ndugu zetu wa World Federation kwa mchango mkubwa uliowezesha kuchapisha kwa kitabu hiki. Allah awalipe kila la

kheri na awape tawfiki katika kazi hii ya tabligh. Halikadhalika tunamshukuru Ustadh Salman Shou kwa kukitarjumi kwa Kiswahili kitabu hiki, insha'Allah na yeye Allah Mwenye kujazi amlipe kila kheri hapa duniani na Akhera pia, bila kuwasahau na wale wote waliochangia kwa namna mmoja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera pia.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 3 10/20/2015 4:31:54 PM

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu,**
**Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.**

# UTANGULIZI

Zipo hadithi nyingi kupita kiasi ambazo zimeletwa kwetu na Ahlul Bayt (a.s.) juu ya uzuri na hekima ya ndoa, ikiwa ni pamoja na Aya kutoka kwenye Qur`ani Tukufu.

Hata hivyo, licha ya amri hii ya wazi kuhusu ndoa, vijana wengi ambao wamefika umri wa kuoa huchelewa kuchukua hatua ya kuelekea kwenye ndoa, hatua ambayo ina uzito mkubwa sana hivyo kwamba inabeba nusu ya imani ya dini yake.[1]

Kwa kufikiri kwa undani zaidi, ni dhahiri kwamba ucheleweshaji huu hausababishwi na hali ya utepetevu au kudharau thamani ya ndoa; kwa usahihi zaidi, inaonyesha yapo matatizo katika mbinu zinazotumika ambazo kwazo vijana hutafutia wachumba wanaofaa. Katika baadhi ya mifano, mbinu huonekana za bandia na zisizoathiriwa na hisia, kama vile kutoa maelezo binafsi kwa washenga wasiojulikana; katika mifano mingine, huduma za ushenga za kimila hutumika lakini hii husababisha ukatishaji tamaa kupitia majaribio ya mara kwa mara yaliyoshindikana. Mwishowe hali hii huwaelekeza vijana kukata tamaa juu ya mfumo huo. Kwa wengine mchakato wote unaweza kuwa wa kutisha kiasi kwamba wanaamua kufanya usirisiri. Kwa bahati mbaya, katika kadhia

[1] *Al-Kafi*, Jz. 5, uk. 328



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 4 10/20/2015 4:31:55 PM

nyinginezo, sababu zilizotajwa hapo juu huishia kuwafanya vijana waamue kutumia mbinu mbadala za kutafuta mchumba, ambazo si zote ni halali, au hata kuwa zenye mafanikio kwa kipindi kirefu.

Mchakato wa kutafuta mchumba anayefaa kwa vyovyote vile sio iliyonyooka na rahisi. Hata hivyo, hii haina maana kwamba mchakato lazima uwe wa kutisha na kuchosha kama unavyokuwa nyakati zingine. Kitabu hiki kinalenga kumwandaa mtu kuwa katika njia ya kutafuta mchumba akiwa na taarifa zinazotakiwa na mwongozo katika kila hatua ya mchakato huo.

Kitabu kinaanza kwa kusisitiza uzuri wa ndoa, na kutambulisha sababu kwa nini mtu anahitaji kuanza safari hii ya kutafuta ‘mwenza’. Vikwazo vinavyowezekana ambavyo watu wanasema kwamba ni vyenye vipingamizi vimeshughulikiwa na ufumbuzi unaowezekana pia umetajwa. Halafu hii inafuatiwa na njia za kutambua iwapo kama mtu yupo tayari kuchukua hatua hii ya kuoa au hapana, kwa kuangalia vigezo vya Kislamu na pia dalili za dhahiri.

Kitabu kinazungumzia mtu anaweza kuangalia nini mchumba mtarajiwa anaweza kuwa nacho kutoka kote, kwenye mtazamo wa kifiqhi na kutoka kwenye hadithi za Maasumin. Pia kitabu kina sehemu inayoelezea juu ya sheria muhimu za Kiislamu na hukmu ambazo zinaweka wazi taarifa muhimu kuhusu mchakato wa uchunguzi.

Halafu kitabu kinachimbua zaidi kwenye baadhi ya mapendekezo kwa ajili ya kutafuta mchumba mtarajiwa wakati mhusika akiambatana na Sheria za Kiislamu. Mazungumzo yanaelezea mbinu za kuweza kumjua mchumba mtarajiwa ili kuweza kuona kama zinakidhi vigezo vya kile kinachotafutwa. Vidokezo vya matayarisho kwa ajili ya awamu hii vimeelezewa kwa kina, zikiwa na maelezo kwa muhtasari ya maeneo na masuala ambayo yanapaswa

kujadiliwa na pande zote mbili; aina za maswali zimetolewa kwa lengo la kurahisisha zaidi mchakato huu, ambapo wakati huo huo ikihakikishwa kwamba masuala yote muhimu yanashughulikiwa.

Halafu hatua inayofuatia katika mchakato huu inaelezewa kwa muhtasari, na pia mtazamo wa kina umefanywa kuhusu jinsi mtu anavyoweza kuamua iwapo kama mtu huyu ndiye anayefaa au hapana. Suala lote hili muhimu limeshughulikiwa kwa kutazama kupitia mtazamo wa kisomi wa wajibu wa moyo na akili, na jambo linalosemwa kila mara kwamba ‘Nilijua tu kuwa alikuwa ndiye sawa yangu’ na ‘tulielewana hivi hivi tu’. Ishara za dhahiri ambazo zinaweza kusaidia kufanya uamuzi zimetajwa, ambazo zimeegemezwa kwenye maoni rejea ya hadithi fupi za kweli kutoka kwa watu kadhaa ambao tayari wamepitia humo, na wamekuja kuwa na ndoa zenye mafanikio.

Mada ya Istikhara na nafasi yake katika kuchagua mchumba, na hususani wakati huu wa kufanya uamuzi nayo imefikiriwa, ikifuatiwa na ukumbusho wa kila mara kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mambo kama haya, na pia utekelezaji wa vitendo fulani vilivyopendekezwa vya ibada na dua.

Endapo kwa jambo hili, mambo yanakwenda sawa, njia ya kuendelea mbele imetambulika. Maelezo ya kina kuhusu posa na uchumba yanatolewa, pamoja na kuangalia kwa karibu zaidi kipindi cha uchumba na dalili mbali mbali za dhahiri ambazo hutumika kama kiashirio kuwa mchumba mtarajiwa ndiye hasa aliye sahihi, au iwapo kama mambo hayo yanahitaji kutathiminiwa zaidi. Kanuni zingine mbali mbali za ki-Fiqh zinafuata, zikijumuisha kipindi hiki cha uchumba na pia nini kifanyike endapo uchumba utavunjika.

Endapo kama mtu atashindwa mara kwa mara kufanikiwa katika kumpata ‘mwenza anayefaa’, kuna maelekezo yametolewa kutoka



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 6 10/20/2015 4:31:55 PM

kwenye Qur`ani, ambayo baada yake suala la kurudia mchakato wote huu baada ya kutalikiana limezungumziwa. Mwisho, kitabu kinaishia na kutazama kwa undani zaidi mikataba mbali mbali ambayo inahusika katika kipindi hiki, yaani mkataba wa ndoa ya Mu`tah, mkataba wa ndoa ya kudumu (*Nikah*) na mkataba wa yale yaliyopo kabla ya ndoa. Dhana ya mahari imezungumziwa pia kwa undani wa kiasi fulani.

Katika kurejelea kanuni za fiqh ambazo zimeandikwa mwote kitabuni humu, inapaswa kuzingatiwa kwamba zote ni kwa mujibu wa Ayatullah al-Uzma Sayyid Ali al-Husaini as-Sistani. Wenye kuwafuata mujtahid wengine wanapaswa kurejelea kwenye Risalah ya mujtahid wao kuhusu sehemu hizi. Zaidi ya hayo, ambapo kitabu hiki kimeelezea kwa ufupi tu maelezo ya jumla yaliyorahisishwa ili kuweza kuongeza utambuzi na kutambua uwepo wa kanuni hizi, Risalah inatoa maelezo mengi zaidi juu ya maeneo binafsi yaliyoshughulikiwa na yanapaswa kupitiwa kwa rejea zaidi endapo itajitokeza haja.

Ni matumaini yetu na dua kwamba kitabu hiki kinakupatia taarifa na nguvu ya kuchukua hatua hii tukufu kuelekea kumpata mwenza, mtu ambaye Insha'Allah atakusaidia kuchukua hatua muhimu kuelekea kwenye lengo lako la mwisho, kuwa karibu zaidi na Allah, na ambaye ni kiburudisho chetu kama ilivyo tamkwa ndani ya Qur`ani:

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا
قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا

**"….. Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mwenyezi Mungu)" (Surat al-Furqan, 25:74)**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 7 10/20/2015 4:31:55 PM

Tungependa kuwashukuru wote wale waliotoa mchango wao kwenye kitabu hiki kwa njia moja au nyingine, na kuunga mkono mradi huu hadi mwisho. Mwenyezi Mungu awalipeni thawabu kwa kila jambo. Hususani, tungependa kushukuru vyanzo viwili ambavyo kutoka humo tulipata vitu vingi, kama ilivyoandikwa mwote kwenye kitabu hiki: *The Islamic Marriage Guidebook* kilichoandikwa na Islamic Humanitarian Service (www.al-haqq.com), na kingine *Solutions for Marriage* kilichoandikwa na Shabbir and Fatima Alibhai and co.

Mwisho, tunakuombeni msamaha kama yapo mapungufu au makosa yoyote ndani ya kitabu hiki; tafadhali tujulisheni na Inshallah, tutajaribu kurekebisha kwa ajili ya wasomaji wa siku za usoni. Pia tunakaribisha maoni au mapendekezo yoyote.

Utakapokuwa unakisoma kitabu hiki, tafadhali zikumbuke familia zetu katika dua, na pia Marehemu wote kwa kusoma Surat al-Fatihah.

Kwa unyenyekevu tunamwomba Mwenyezi Mungu aikubalie juhudi hii, na kama itakubaliwa, tunawakilisha juhudi hii kwa Imam wetu mtukufu wa zama zetu, Imam Mahdi (a.t.f.s.)

**“Sifa zote ni Stahiki Yake Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu.”**

**Abbas na Shaheen Merali**

# SURA YA 1

# MUUJIZA WA NDOA

### Uhusiano wa Kwanza wa Binadamu[2]

Tukizungumza kihistoria, uhusiano wa kwanza kabisa ulioanzishwa ni ule wa ndoa baina ya mwanamume - sio ule wa mama na binti yake, baba na mwanae mwanamume au uhusiano wowote ule. Ndani ya kitabu kiitwacho *Ettiquette of Marriage* (Adabu za Ndoa), pametajwa kile kisa kizuri sana cha Nabii Adam na ndoa yake, ambacho tunakisimulia hapa.

Baada ya kuumbwa kwa Adam alijihisi upweke na akalalamika kwa Muweza wa Yote kuhusu upweke wake. Mwenyezi Mungu akamlaza Adam katika usingizi halafu akamuumba Hawa akiwa mzuri mno.

Mwenyezi Mungu alimvika Hawa majoho ya Peponi na akamleta akiwa na mapambo mengine ya kujirembeshea. Katika wakati huu alimwagiza Hawa akae karibu na kichwa cha Nabii Adam. Adam alipoamka kutoka usingizini macho yake yakamuona Hawa, alivutiwa mno na uzuri wake hivyo kwamba alitaka asogee karibu naye ili amguse. Wakati huo huo, malaika walimzuia asifanye hivyo.

Adam akawauliza malaika hao: "Hivi Mwenyezi Mungu hakumuumba huyu kwa ajili yangu mimi?" Malaika wakajibu: "Ndiyo, lakini unatakiwa umwendee kwa namna inayofaa. Kwanza

[2] *The Islamic Marriage Guidebook, Islamic Humanitarian Service* (www.al-haqq.com)



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 9 10/20/2015 4:31:55 PM

lazima umpose (kwa kumuomba mlezi wake ruhusa ya kumuoa yeye), halafu unatakiwa umpe Mahari (zawadi), ikifuatiwa na kusomwa tamko la ndoa (mkataba wa ndoa)." Nabii Adam akauliza: "Nitamuomba nani ruhusa ya kumuoa Hawa?" Malaika wakajibu: "Lazima umuombe Allah" Halafu Adam akauliza: "Ee Allah! Mahari yake itakuwa nini?" Mwenyezi Mungu akajibu: "Mfundishe sheria za dini Yangu na umtakie rehema (kumsalia Mtume) Muhammad na Watu wa Nyumba yake."

## UZURI WA NDOA - KWA NINI NAPASWA KUOA?

Mwanadamu, kama ilivyo kwa kiumbe kingine chochote chenye mwili na roho, anayo mahitaji ya vitu kadhaa – ambayo kila moja ni umuhimu kwa ajili ya ulinzi wa uhai wake na ustawi. Kwa mfano, maumivu ya njaa na kuhitajia lishe humlazimisha mtu kula chakula ili awe na nguvu ya kuishi siku nyingine; hisia za kiu humfanya mtu anywe maji ambayo pia ni muhimu kwa uhai wa mtu. Vitu hivi na vingine vingi humwezesha mwanadamu kuishi maisha ya ustawi na afya njema.

Kwa kuwa mwanadamu amechaguliwa kama 'mbora zaidi katika viumbe', Mwenyezi Mungu ameweka msingi wa ndoa ili kuweza kuruhusu mahitaji haya ya maisha, ya kimwili na kiroho, yatimizwe kwa namna iliyo halali. Miongozo inaendana sana na akili - kwa kuwa sheria ni za ki-Mungu na masharti maalum yanaendana na roho zenye thamani za wanamume na wanawake. Mahitaji haya na kutimizwa kwao kupitia kwenye taasisi takatifu ya ndoa sasa yatazungumziwa kwa kina zaidi:

## 1. Ukaribu na Mwenyezi Mungu:

Ndoa huruhusu kutimia kwa mahitaji ya juu zaidi ya mwanadamu, la msingi zaidi likiwa ni haja ya kupata ukaribu zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kweli, sababu hii peke yake inajumuisha manufaa mengine yote ya ndoa yaliyoorodheshwa hapa chini na hili ndilo lengo hasa la juu kabisa, kwani lengo la jambo lolote katika kipindi cha tangu kuzaliwa hadi kifo ni kwamba humwezesha mtu kumtumikia Mola Wake na kupata ukaribu zaidi Kwake. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur`ani Tukufu:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

**"Na sikuumba majini na watu ila wapate kuniabudu." (51:56)**

Kwa hiyo, ndoa lazima itumikie kusudio hili la mwisho la utumwa kwa Mola na Muumba wa ulimwengu huu. Hapa chini tunaeleza jinsi ya kufanya hili.

## 2. Kukidhi Matamanio ya Kijinsia ya Asili

Tamaa na mahitaji ya kijinsia ni mahitaji ya msingi sana ya mwanadamu. Tamaa ijmai yenye nguvu iliyo ya asili ndani ya wanadamu inachukua nafasi kubwa katika kumlinda mwanadamu na kuendeleza kuwepo kwa jamii ya mwanadamu. Kwa hiyo, kwa kuwa ina nguvu sana na ya kimaumbile, si busara kutotii shauku hii au kujaribu kuizuia, wala haileti maana mtu kuiendekeza tamaa hii bila masharti na mipaka fulani; miishilizio yote hii iliyotajwa hapo juu imesababisha matatizo ya kijamii kama inavyoweza kuonekana kwenye mifano ya mapadri wenye mfadhaiko wa kutamani watoto wadogo na vurugu za kimaadili.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 11 10/20/2015 4:31:55 PM

Katika  Uislamu, ndoa inazingatia ukidhiaji wa haja za kijinsia katika njia iliyo halali na ya kisheria. Kwa kweli, utimizwaji wa haja hili ni wa muhimu sana kwa sababu ya matokeo yake mabaya yanayojitokeza kama haikushughulikiwa. Kwamba iwapo kama mtu anahofia kwamba kwa kutokuoa au kuolewa anaweza kuangukia kwenye dhambi, basi Uislamu unashurutisha kwamba mtu huyo anawajibika kuoa au kuolewa.

Mwanasaikolojia Abraham Maslow, katika maandishi yake juu ya mfumo wa mpangilio wa matabaka ya mahitaji ya mwanadamu anasema kwamba mahitaji ya kisaikolojia lazima yatimizwe kabla utambuzi wa nafsi haujajitokeza. Kwa maneno mengine, ili mwanadamu aweze kupata viwango vya juu zaidi vya kusudio, mahitaji yake muhimu yanayojumuisha chakula, ijmai na usingizi lazima yapatikane. Labda hii inaeleza umuhimu wa hekima iliyopo kwenye ndoa katika Uislamu na mhimizo uliowekwa juu ya ndoa za mapema. Katika Uislamu lengo la juu kabisa ambalo mwanadamu anatakiwa kulipata ni utiifu kwa Mwenyezi Mungu; hata hivyo, kama binadamu hakukamilika kimaumbile na kihisia, ataondolewa kwenye kupita katika njia ya ukaribu wa kiroho kuelekea kwa Mola Wake.

### 3. Faraja na ukamilifu

Mwanadamu hakuumbwa awe peke yake, sisi kwa kawaida hutamani sana kuwa pamoja na wenza, ukaribu na faraja. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur`ani Tukufu:

وَمِنْ ءَايَـٰتِهِۦٓ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَٰجًا لِّتَسْكُنُوٓا۟ إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُم
مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَـَٔايَـٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 12 10/20/2015 4:31:55 PM

**"Na katika ishara Zake ni kuwaumbia wake zenu kutokana nafsi zenu ili mpate utulivu kwao, na akajaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya kuna ishara kwa watu wanaofikiri." [Surat al-Rum, 30:21]**

Ndani ya aya hii tunaona kwamba Mwenyezi Mungu anachukulia uumbaji wa wanawake ni mojawapo ya ishara Zake. Mwenyezi Mungu sio amewaumba hawa watu wawili tu, lakini ili pawepo na amani na utulivu baina ya wawili hao, Yeye ameweka mapenzi na huruma baina yao ili waweze kuishi maisha ya utulivu.

Katika aya nyingine, Mwenyezi Mungu anamwelezea mwanamume na mwanamke kama vazi la kila mmojawao:

..... هُنَّ لِبَاسٌ لَّكُمْ وَأَنتُمْ لِبَاسٌ لَّهُنَّ .....

**"…Wao ni vazi lenu na nyinyi ni vazi lao…." [Surat al-Baqarah, 2:187]**

Mfanano huu unaturuhusu sisi kuelewa namna jinsi mwanamume na mwanamke wanavyoleta faraja hii, na kwa ufupi, kukamilishana wao kwa wao. Mavazi yetu na nguo zetu hutuongezea sisi uzuri. Hufunika kasoro zetu za kimaumbile na mambo fulani yasiyo ya kawaida. Kwa njia hii, mume na mke kila mmojawao anapaswa kuchukua wajibu ule ule hasa katika uhusiano kwa kila mmoja wao. Endapo mke ana kasoro za kiroho, kimaadili au kisaikolojia au anayo mapungufu fulani katika tabia yake, basi mume lazima asaidie katika kufunika mambo haya na sio kudhihirisha kasoro zake kwa wengine na kwa mke naye hivyo hivyo.

Mavazi hutukinga kutokana na makali ya mazingira. Nguo zinaweza kutupatia joto wakati mazingira yanapokuwa ya baridi, au kutoa ulinzi dhidi ya joto. Mavazi yanaweza kutulinda miili

yetu kutokana na ardhi ngumu. Kadhalika mwenza wetu anapaswa kufunika wasiwasi na huzuni zetu, na anapaswa kufanya matatizo ya siku hadi siku kuwa mepesi kuyahimili. Hatimaye, kama vile ambavyo mwanadamu hawezi kuishi kiheshima bila ya nguo, mwanadamu huyo huyo mpweke pia hawezi kuishi maisha ya heshima na yaliyokamilika.

Kwa kulizingatia akilini lile lengo la mwisho la kupata ukaribu kwa Mwenyezi Mungu, ni utangamano huu na utulivu, ulinzi na msaada ambao ndoa huvitengeneza katika nyoyo zetu ambavyo vinamuwezesha mja wa Mwenyezi Mungu kupata ukaribu na Yeye.

## 4. Mtandao wa Kijamii

Katika tamaduni nyingi, na hususani katika utamaduni wa jamii ya India na Pakstani, watu wawili wanapooana, familia mbili huoana. Mtandao huu mpana wa kijamii wa kusaidiana unaweza kufaa sana, hususani katika nyakati za uzazi, vifo, mabadiliko ya mtindo wa maisha, malezi ya watoto na mazingira mengine yenye changamoto ambamo maisha yanaweza kutupitisha humo. Upo pia uwezekano wa manufaa ya kifedha ndani ya mfumo huu wa mtandao wa kusaidiana kijamii, zaidi ya hayo ambayo mume na mke wenyewe wameleta ndani ya ndoa. Hivyo, ndoa huleta utimilifu wa haja nyingine: haja ya msaada na uimara, na matokeo yake ni kwamba mtu anaweza kulenga juu ya haja kubwa zaidi za nafsi.

## 5. Muundo wa Familia.

Ndoa pia hutimiza haja ya kimaumbile kwa ajili ya kupata watoto na familia. Katika aya hii ya Qur`ani, kwa mara nyingine tena tunakumbushwa kwamba ni Mwenyezi Mungu ndiye aliyemuumba mwan-

adamu na halafu akamtengeneza mwenza (mwanamke) na kupitia kwa hawa watu wawili dunia ikajaa watu.

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱتَّقُوا۟ رَبَّكُمُ ٱلَّذِى خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَٰحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَآءً .....

**"Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni kutokana na nafsi moja, na akaumba kutokana na (nafsi) hiyo wa pili wake, na akaeneza kwa wawili hao wanamume na wanawake wengi….." [4:1]**

Hata bila ya watoto hata hivyo, muungano wa mwanamume na mwanamke hutengeneza fungamano baina ya wawili hao, na huwazawadia wao sifa ya kutokuwa na ubinafsi. Uhamisho wa fikra kutoka 'mimi' na kwenda 'sisi' huchochea kukua kwa tabia kama vile kujituma, ukomavu, uwajibikaji na ndiyo haya ambayo huwakilisha dhana ya 'familia.'

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Hakuna taasisi ndani ya Uislamu ambayo inapendwa zaidi na thamani zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko ndoa."[3]

Kama familia inajengwa kwenye msingi wa aina hiyo yenye mapenzi, ukweli na uaminifu na imani ya kweli kwa Mwenyezi Mungu na yote yale ambayo ameyaamuru, basi hakuna kitu ambacho kinaweza kuharibu jengo madhubuti kama hilo, na ni jengo hili madhubuti ambamo mtu anaweza kupata ukaribu kwa Mwenyezi Mungu.

Kulea watoto ni kazi nzito, ambayo inahitaji juhudi na uvumilivu. Kuwa na msingi madhubuti kama ndoa huruhusu wazazi kuhamasishana wao kwa wao na kupata nguvu kutoka kwa kila mmoja katika kuwalea watoto kwa njia nzuri iwezekenayo, kama

[3] *Bihar al-Anwar*, uk. 222, Juz. 34

watu watulivu walioko kwenye njia iliyo sahihi. Ndoa nzuri pia huzuia matatizo ambayo yameenea katika jamii leo hii, ambayo mara nyingi husababishwa na kuvunjika kwa muundo wa familia wa kiasili.

### 6. Thawabu za Kiroho

Kwa zaidi ya hayo hapo juu, hadithi kutoka Ahlul Bayt ambazo zinaelezea kuongezeka kwa thawabu za kiroho za vitendo vya ibada vya mtu aliyeoa au aliyeolewa, zikilinganishwa na za mtu asiye na ndoa, ni nyingi sana. Baadhi yake zimenukuliwa hapa chini:

Imesimuliwa kutoka kwa Imam Sadiq (a.s.): "Rakaa mbili anazoswali mtu aliye kwenye ndoa ni bora zaidi kuliko rakaa sabini anazoswali mtu kapera – asiye na ndoa."[4] – Mtukufu Mtume alisema: "Usingizi wa mtu aliye na ndoa ni bora zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko anayefunga saumu ya kila siku na kukesha usiku kucha akiswali."[5]

# HITIMISHO

Mwendelezo wa tabia zilizotajwa hapo juu ni hatua muhimu ndani ya njia ya kiroho kuelekea kwa Mwenyezi Mungu. Hii pia inaweza kuwa ni sababu ya Imam Ali (a.s.) amesimulia: "Hapakuwepo na maswahaba wa Mtume ambao wangeoa, bali Mtume alikuwa akisema imani yao imekamilika."[6]

### Vikwazo Kwenye Ndoa:

Vipo viunzi na vikwazo vingi ambavyo watu hukutana navyo wakati

[4] *Wasa`il ash-Shia*, Juz. 14, uk. 6
[5] *Bihar al-Anwar*, Juz. 103, uk. 221
6 *Makarimul Akhlaq*, uk. 99



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 16 10/20/2015 4:31:56 PM

wa kuoana, hususani mtu anapotaka kuoa akingali na umri mdogo. Baadhi ya vikwazo hivyo vimeelezewa kwa muhtasari hapa chini pamoja na ufumbuzi wake.

**Kikwazo 1: Tatizo la kiuchumi**

Mojawapo ya vikwazo vikubwa vinavyotolewa ni suala la uchumi: hivi mtu ambaye bado anasoma, au ndiyo kwanza anaanza kazi mpya, anaweza kumudu kuoa? Wataweza kugharamia sherehe za harusi na baada ya hapo kutoa gharama za kukimu familia?

**Ufumbuzi wa 1: Ahadi ya Mwenyezi Mungu**

> "Nilikuwa nasikiliza kaswida (*nasheed*) ya Kislamu juu ya ndoa na maneno yake yalinishtua kwani aliielezea ndoa kama njia ya 'kukamilisha dini yako' na si 'kukamilisha ndoto zako' kama ilivyo kawaida! Kwa ufupi ndivyo ilivyo. Kwangu mimi, kiroho imefanya wajibu mkubwa sana….. upo muunganiko wa ajabu sana katika kuswali pamoja, katika kutokuruhusu kingine ISIPOKUWA Mwenyezi Mungu kuwa baina yenu wawili. Wanandoa wanaweza kuwa 'kiashirio' kuelekea kwenye mambo makubwa zaidi ya kiroho, yanayoleta aina fulani ya kujikagua na kujisahihisha baina ya wawili." **Mwanamke USA (Marekani)**

Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur`ani Tukufu:

وَأَنكِحُوا۟ ٱلْأَيَٰمَىٰ مِنكُمْ وَٱلصَّٰلِحِينَ مِنْ عِبَادِكُمْ وَإِمَآئِكُمْ ۚ إِن
يَكُونُوا۟ فُقَرَآءَ يُغْنِهِمُ ٱللَّهُ مِن فَضْلِهِۦ ۗ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٢﴾



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 17 10/20/2015 4:31:56 PM

**"Na waozeni wajane miongoni mwenu na wema katika watumwa wenu na wajakazi wenu, wakiwa mafukara Mwenyezi Mungu atawatosheleza katika fadhili zake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua." [24:32]**

Pia imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Wapeni wenza wale makapera wenu, kwa sababu Mwenyezi Mungu huboresha uadilifu wao na huongeza riziki yao na huwaongezea ukarimu wao (maadili ya binadamu).[7]

Na: Mtu anayetelekeza na kuacha kuoa kwa kuogopa umasikini na shida, kwa kweli huyo ana fikra hasi juu ya Mwenyezi Mungu…"[8]

Kwa kweli, hata Mtume alishauri ndoa kuwa kama jibu la tatizo la umasikini, na kusema: "Oeni kwani hilo huongeza riziki zenu".[9] Pia inasimuliwa kutoka kwa Imam Sadiq (a.s.) "Riziki ipo kwa wake zenu na familia."[10]

## Ufumbuzi wa 2: Familia na Jumuiya

Msaada kutoka kwenye familia katika kutatua tatizo hili ni wa muhimu sana; ima msaada huu unakuwa wa kuwasaidia wanandoa hadi hapo watakapopata fedha za kutosha na kujitosheleza wenyewe, au kama wanawapa wanandoa hela za posho, au hata mkopo.

Kama hali ilivyo ni kwamba familia haiwezi kusaidia kifedha au sababu zingine, ni muhimu kwa jumuiya kufanya hivyo, kupitia kuanzisha mifuko ya dhamana, mifuko ya utoaji mikopo ya fedha, kamati na miundo mingine ya kutoa msaada. Fedha zinaweza kulipwa katika muda fulani na ziwasaidie wanandoa wengine wenye matatizo kama hayo.

---

7 *Nawadir al-Rawandi*, uk. 36

8 *Wasa`il ash-shi`* Juz. 3, uk. 5

9 *Wasa`il ash-Shi`a*, Juz. 3, uk.7

10 *Nuur al-Thaqalayn*, Juz. 3, uk.599

**Ufumbuzi wa 3: Usiwaige Majirani (wenye uwezo)!**

Kwenye jamii ambamo umuhimu mkubwa sana umewekwa kwenye kuthamini pesa na alama za hadhi, inaweza kuwa vigumu kushikilia na kuzingatia mambo ya msingi tu katika maisha. Lakini inaweza kufanyika. Kuanza na sherehe ya harusi isiyo na gharama kubwa, kuishi na familia hadi hapo mnapoweza kujitosheleza wenyewe, kuweka samani za bei nafuu, kujizoeza kutosheka kutachukua muda katika kuwajenga wanandoa kifedha, bila kusema daraja watakalopata katika akhera.

**Kikwazo 2: Elimu**

Tamaa ya kutaka kuendelea na masomo ya juu zaidi ni kikwazo kingine ambacho huwazuia watu wengi kufunga ndoa.

**Ufumbuzi:**

Hata hivyo, ndani ya jamii ya leo, inakuwa inakubalika zaidi na zaidi, na hata kutakiwa hasa kwamba mmojawapo wa wanandoa au wote waendelee na masomo baada ya kuoana. Wakati mwingine huposana, wakaendelea na masomo yao hadi kumaliza na halafu wakaoana.

> “Dada yangu mdogo alipoposwa kabla yangu nilifurahi sana kuwa ningepata shemeji yangu mwingine tena na niliweza kushiriki kikamilifu kwenye sherehe yake. Ninaamini kwamba pale anapokuja mtu anayefaa, unapaswa kukubali bila kujali kama wewe ni mtoto mkubwa au mdogo.” **Mwanamke, Uingereza.**

Pamoja na mapenzi na msaada wa wazazi na pia kutosheka na kidogo kama ilivyoelezewa juu, hakuna sababu ya hili kuwa ni



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 19 10/20/2015 4:31:56 PM

kikwazo. Kwa kweli, katika mifano mingi, kusoma baada ya kuoa kumethibitika kuwa ni rahisi zaidi na kunakovumilika zaidi:

> “Mwanzoni nilikuwa na wasiwasi wa kuchukua hatua ya kuolewa wakati bado nasoma chuo kikuu, kwani nilikwisha sikia hadithi za kutisha kutoka kwa marafiki, kwa kiasi cha kutakiwa kuhakikisha kwamba chakula cha jioni kinapikwa na nyumba inasafishwa kabla ya kuanza kujisomea! Alhamdulillah, kusoma wakati nimeolewa halikuwa tatizo kubwa kwangu na nadhani mawasiliano yalikuwa ndiyo ufunguo muhimu kwa hili. Kabla sijakubali kuolewa, nilikuwa nimehakikisha kwamba kusoma kutaruhusiwa na kukubaliwa na familia yangu mpya. Lakini jambo ambalo lilisaidia zaidi ni kwamba mume wangu naye alikuwa anasoma pia, hivyo alikuwa anajua kabisa kuhusu kilichokuwa kinanitokea: tuliweza kwenda maktaba wote wawili na tulihamasishana kujisomea kwa ajili ya mitihani. Kuishi na wakwe zangu wanaoelewa na wenye msaada sana pia kumesaidia hili kwani ilimaanisha kwamba nisiwe na wasiwasi kuhusu kuandaa meza kwa ajili ya chakula cha jioni wakati wa shughuli zenye mkazo za mitihani!” - **Mwanamke, Uingereza**

### Kikwazo 3. Watoto wakubwa

Ni desturi kwenye tamaduni nyingi kwamba kama yupo kaka mkubwa au dada mkubwa ambaye hajaoa au kuolewa wazazi hawakubali mtoto wao mdogo aoe au aolewe, hata kama wanahisi kwamba wamempata mtu anayefaa.

**Uvumbuzi:** Imani kama hiyo haina msingi katika Uislamu. Ndani ya kitabu chake, “Vijana na Kuchagua Mchumba” (*Youth and Spouse*



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 20 10/20/2015 4:31:57 PM

*Selection*), Mazaheri amekwenda mbali zaidi na kuwahamasisha vijana kuvunja desturi hii ya makosa, kuliko kuteswa na matokeo hasi ya muda mfupi na muda mrefu kwa sababu ya hilo.

**Kikwazo cha 4. Mke mtarajiwa anao umri mkubwa zaidi /amesoma zaidi na/au ana kipato kikubwa zaidi ya mume mtarajiwa.**

**Ufumbuzi:** Pamoja na kwamba linaonekana ni jambo lililopitwa na wakati, kwa bahati mbaya fikra hii bado ipo. Tena, hii nayo haina msingi wowote katika Uislamu na fikra kama hii inapaswa kubadilishwa. Mtu anahitaji tu kutazama mfano wa Mtukufu Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w.); alimuoa Bibi Khadija (a.s.) alipokuwa ana umri wa miaka 25 na Khadija alikuwa na umri wa miaka 28 au 40 (kufuatana na hadithi kutofautiana). Pia Bibi Khadija alikuwa mmojawapo wa wanawake wakwasi sana ndani ya Makka katika haki yake, licha ya utamaduni uliotawaliwa na wanamume wakati huo; akiwa amerithi msafara wa biashara wa baba yake baada ya kifo cha baba yake, aliikuza biashara na kuwa mkusanyiko mkubwa sana wa msafara katika eneo hilo.[11] Kwa hiyo, tunaona kutoka kwenye maisha ya Mtume kwamba kama mke mtarajiwa ana umri mkubwa zaidi, amesoma zaidi au ana kipato kikubwa zaidi, basi hicho kisiwe kikwazo cha kumnyima fursa ya kuolewa.

[11] Mtume Muhammad (s) - *A Concise Biography*, Dr M H Datoo



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 21 10/20/2015 4:31:57 PM

# SURA YA 2

# NITAJUAJE KAMA NIPO TAYARI ?

## VIGEZO[12]

Tatizo la kawaida linalowakabili wote wanamume na wanawake ni jinsi ya kutambua kama wapo tayari kuchukua hatua hiyo kubwa ya kuoa au kuolewa au bado.

Kifuatacho hapa chini ni mukhtasari wa vigezo kwa ajili ya pale mtu anapopaswa kufunga ndoa, pia na viashiria halisia ambavyo unaweza kuvitumia katika kufanya uamuzi huu.

### 1. Upevu wa Kimwili

Katika ufafanuzi wa kisheria wa Kiislamu, balekhe hutambuliwa kwa mojawapo ya mambo yafuatayo:[13]

**Wasichana:** Wakati wa kutimiza umri wa miaka 9 ya mwandamo wa mwezi.

**Wavulana:** Ama baada ya kutimiza umri wa miaka 15 ya mwandamo wa mwezi, au yote haya yafuatayo:

a. Mabadiliko ya ndani kwa ndani: Kutoka kwa manii kwa mara ya kwanza usiku. Manii hujikusanya ndani ya korodani tangu mtu anapobalehe na kuendelea na manii mengi zaidi yanaweza

---

[12] Imechukuliwa kwa uzito zaidi kutoka "*Solutions for Marriage*", Sehemu 2 kati ya 4 Shabbir cha M H Alibhai & Fatima Y Alibhai &co., and "*The Islamic Marriage Guidebook*", Islamic Humanitarian Service (www, al-haqq.com)

[13] *Islamic Laws*, kwa mujibu wa Fatwa ya Ayatullah al-Uzma Sayyid Ali al-Husaini as-Sistani, The World Federation, London,1994, Kanuni ya 2260



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 22 10/20/2015 4:31:57 PM

kutengenezwa kuliko yale ambayo mfumo unaweza kuyanyonya; inapotokea hivyo, manii hutolewa wakati wa kulala usingizi. Hali hii huitwa kama kutokwa na manii usiku/ndoto ya kutokwa na manii, au '*ihtlam*' kwa Kiarabu.

b. Mabadiliko ya Kimwili: Kuota nywele kwenye sehemu za siri chini ya tumbo. Kwa kuwa hamu ya ngono huanza wakati wa balehe na kama Uislamu usemavyo kwamba hamu ya ngono inapaswa kutimizwa kupitia ndoa tu. Uislamu umeruhusu ndoa mara mvulana na msichana wanapofika umri wa balehe. Hata hivyo, huu ndio umri wa chini kabisa na vipengele vingine (vimeelezwa hapo chini kwa muhtasari) vinatakiwa vitiliwe maanani kabla ya kufanya uamuzi wa kuoa au kuolewa.

## 2. Ukomavu wa akili

Ukomavu wa akili (*Rushd*) una umuhimu sawa na upevu wa kimaumbile. Uislamu umefafanua umri wa upevu wa kimaumbile lakini haukufafanua umri wa ukomavu wa akili. Badala yake umewaachia wazazi, walezi na wahusika wenyewe wafanye uamuzi kwa busara zao.

Ayatullah Khomein amefafanua 'balekhe' hivi: "Balekhe inamaanisha kuwepo kwa uwezo mkubwa wa mawazo na akili katika shughuli zake mtu, uwezo wa mtu kulinda mali yake isitumike vibaya na busara ya mtu katika kutumia kisheria."

## 3. Utayari wa Kiakili

Ndoa ni wajibu wa muda mrefu wa maisha ya mtu na hili ni jambo muhimu kwako kulifikiria. Yapo mabadiliko muhimu ambayo wote, mwanamume na mwanamke lazima wawe tayari kufanya ili kuifanya ndoa iwe yenye kufanikiwa. Kuna kuwajibika kiwakati, kihisia kiuchumi, na kadhalika.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 23 10/20/2015 4:31:57 PM

Mara nyingi – hasa kwa upande wa mwanamume – ni rahisi kutulia kwenye taratibu za kila siku za maisha ya ndoa baada ya fungate, akifikiri kwamba uhusiano umeimarishwa na sasa unaweza kuwekwa kwenye aina ya 'udhibiti wa mizunguko' kwa vile mazingatio yamehamishiwa kwenye kazi inayofuatia. Kijana yeyote anayefikiria kuoa kwa dhati kabisa lazima awe tayari kujitoa muhanga kwa mambo mengi na masikilizano mengi ili kuweza kusaidia uhusiano; hususani wote wawili lazima wawe tayari kufanya mabadiliko wao wenyewe na kukubali kwamba mambo fulani hayawezekani na hayapaswi kubadilishwa kwa upande wa wenzi wao, hata kama inaweza kuwa ni jambo gumu kulikubali.

**4. Ukomavu wa Hisia**

Ili ndoa iweze kufuzu upo ushirikiano mkubwa na wa karibu sana wa hisia za moyoni unaojitokeza baina ya mume na mke. Kuna muundo wa fungamano maalum baina yao, hali hii hurejelewa kwenye baadhi ya duru za kisaikolojia kama 'kusonga' ambamo akili zao huanza kuungana na kuwa kama kitu kimoja. Hali hii inafanana na fikra ile inayopigwa chuku sana katika kuhadithia kuhusu mpenzi kama 'kipenzi cha roho' na ina ukweli fulani ndani yake. Mwanamume na mwanamke ambao wameoana kwa furaha hawapo tena kama 'mtu binafsi'; kwa kiwango kikubwa, wamekuwa mmoja kiakili, kimwili, na kiroho. Kwa dhahiri huu ni uhusiano changamano na wa pekee wa watu wazima ambao huchukua kiasi fulani cha ukomavu wa hisia na uwajibikaji kutoka kwa wahusika wote wawili. Kama ambavyo wanachuoni wetu kadhaa wamesema, hali hii huhitaji mkondo ulio wazi na wa kuaminika wa mawasiliano baina ya mume na mke.

Watu ambao kabla ya hapo walikuwa huru katika kufanya maamuzi kwao na walikuwa wanafurahia muda mrefu sana wa uhuru binafsi watahitaji kutambua kwamba ndoa inahitaji utoaji



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 24 10/20/2015 4:31:57 PM

maamuzi wa kushirikiana kuhusu mambo mengi zaidi na kujitolea muda wao huru kwani watauelekeza kwa mwenza wake, na familia. Pia wanamume na wanawake lazima watambue kwamba zipo tofauti zenye msingi wa kijinsia katika jinsi wanamume na wanawake wanavyofikiri, kutatua matatizo, na kujieleza wenyewe, ambazo zinahitaji kuangaliwa wakati wanandoa wanapowasiliana.

Uelewa mkubwa wa tofauti hizi unaweza kupatikana kwa kusoma juu ya somo hili (angalia Orodha ya Vitabu Vilivyopendekezwa Kuvisoma iliyoko mwishoni mwa kitabu hiki), na kozi nyingi za uhusiano wa wanandoa pia huzungumzia masomo haya, na hutoa mifano na mazoezi ya kivitendo juu ya jinsi ya kushughulikia tofauti hizi. Utambuzi huu unaweza kuwa na manufaa sana katika kuongoza majibizano yetu na kuboresha mawasiliano ya kawaida na kuelewana baina ya wanandoa.

## 5. Uimara wa Kiuchumi

Ingawaje uimara wa kiuchumi si sharti muhimu, mara nyingi una uzito wakati wa miaka michache ya mwanzo ya maisha ya ndoa kwa wote wawili mwanamume na mwanamke. Wanandoa ambao wanajitahidi sana katika kuyaweka mambo sawa watapata wasiwasi wa ziada zaidi ya ule wa kawaida ambao hupitiwa na wanandoa ambao wamo kwenye siku zao za mwanzo wa ndoa yao. Wanandoa wapya watakutana na uwezekano wa matumizi mapya ya kifedha, kama vile matumizi ya kipindi cha fungate, kununua fenicha mpya, nguo, na vitu vya nyumbani. Kwa uhakika kuna kiwango fulani cha ongezeko la manunuzi ya chakula, viburudisho, usafiri, na pia matumuzi ya hapa na pale. Matokeo yake ni kwamba kuwa na uimara wa kifedha husaidia sana.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 25 10/20/2015 4:31:57 PM

Hata hivyo, masuala ya kiuchumi hayapaswi kuwa jambo la kuhangaisha sana wakati wa kufikiria ndoa, na kuna mifano mingi sana ya wanandoa ambao wameweza kuendelea kusoma baada ya kuoana, au mmojawao akawa anasoma na mwingine akiwa nyumbani. Kuushinda uchumi kama kikwazo dhidi ya ndoa ni mada ambayo imeelezewa zaidi kwenye Sura ya Kwanza.

## 6. Ujana

Uislamu unasisitiza sana kwamba ndoa haipaswi kucheleweshwa. Mwandishi wa *Youth and Spouse Selection* - "Ujana na Kuchagua Mchumba" ameelezea muda wa ujana kuwa kama 'majira ya kuchipua' ya ndoa, kwa kuwa mwanamume anatawaliwa na nguvu na uhai, na hali hii husababisha ndoa kustawi. Kama kipindi hiki hakikutumiwa, basi umri wa 'majira ya kupukutika kwa majani' unakaribia, na hapo mwanadamu hataweza kufurahikia na kutumia vilivyo manufaa ya ndoa.

Imesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Hakuna hata kijana yoyote ambaye anaoa wakati wa ujana wake, isipokuwa Shetani wake hulia kwa sauti kubwa akisema: 'Ole wake, ole wake, amejilinda nami kwa theluthi mbili za imani yake;' kwa hiyo, mwanadamu lazima awe na takwa ili kulinda theluthi moja ya imani yake iliyobakia."[14]

Sababu moja iliyo wazi kuhusu msisitizo huu ni kwamba kuoa katika umri wa ujana hupunguza nafasi ya vitendo haramu vinavyofanywa kwa sababu ya kutotimizwa kwa tamaa za kijinsia. Hata hivyo, sababu nyingine muhimu sana ni kwamba jinsi umri wa mtu unavyozidi kwenda juu ndivyo tabia yake na mwenendo wake unavyojipanga zaidi na kutokubali kushindwa, ambapo ndoa nzuri inahitaji uwezo wa kurekebishika na kuwa na tabia

[14] *Muntakhab Mizan al-Hikmah*, Juz. 1, uk. 457



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 26 10/20/2015 4:31:57 PM

zinazofanana; hali hii husababisha ndoa kuwa na matunda mazuri na yenye mafanikio.

## Muhtasari

Ingawaje ndoa imeruhusiwa mwanzoni mwa balekhe, na watu wetu wengi watukufu kihistoria walioa wakiwa wangali vijana, leo hii na katika zama hizi inaelekea sio uhalisia kufikiria ndoa kabla ya umri wa miaka 18. Wakati kuna upekee wa mambo kwenye kanuni hii, mtu anatakiwa kukumbuka kwamba si tu kwamba wanamume na wanawake wanabalekhe katika nyakati tofauti, pia wanaelekea kuchelewa kubalekhe ikilinganishwa na watu walioishi karne nyingi zilizopita. Namna ya maisha yetu ya sasa imekuwa ya kutatiza sana hivyo kwamba upo mwanya mkubwa kiasi baina ya balekhe na ukomavu katika mambo ya kiuchumi na kijamii. Makala inayozungumzia juu ya vijana wa Marekani inasema, "Vijana wa kimarekani wanaoingia karne ya 21 hawajakomaa sawa na wahenga wao walivyokuwa wamekomaa wakati wanaingia karne ya 20. Tofauti inaonekana wazi kwenye maeneo yote ya maendeleo ya ujana: ngono, mapenzi, ndoa, elimu na kazi. Kimaumbile, vijana wa leo wanakomaa mapema zaidi kuliko vizazi vilivyopita, lakini kukomaa kihisia wanachukua muda mrefu zaidi hadi kukuza mahusiano ya kiutu uzima."[15] Matokeo yake ni kwamba, si rahisi kwa wavulana na wasichana wa enzi zetu kuoana mara tu wanapokomaa kimaumbile.

Pia umri wa miaka 18 ni kipindi muhimu cha mabadiliko katika maisha ya vijana wengi katika jamii ya nchi za Magharibi. Kwa kawaida huu ni wakati ambapo maamuzi makubwa kuhusu elimu ya kabla ya sekondari hufanywa na mipango ya kazi pia hufanyika. Katika wakati huu, vijana huwa wamehama kutoka kwenye fikra ya vijana walioko kwenye vyuo vya elimu ya juu na kuwa vijana

[15] *Newsweek*, Special Edition Spring 1990, pg. 55



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 27 10/20/2015 4:31:57 PM

wakubwa waliokomaa ambao wanaingia kwenye nguvukazi au kuelekea kutafuta elimu ya juu zaidi. Mabadiliko haya, yenyewe tu, yanahitaji kiwango fulani cha ukomavu ambacho kilikuwa hakihitajiki kabla ya zama hizi.

Ingawaje kukomaa kwa mawazo, akili na hisia ni sifa muhimu ambazo anapaswa kuwa nazo mtu anapotaka kuoa, lazima itambulike kwamba kitendo cha kufunga ndoa ndani mwake na kwenyewe kunabadilisha zaidi watu na huwasaidia kukomaa zaidi. Yaweza kuwa isiwezekane kudai ukomavu wa asilimia 100 kabla ya ndoa, lakini kwa hakika mtu lazima atakuwa amechukua hatua fulani kadhaa muhimu kwenye mwelekeo huu. Zaidi ya hayo, kuna tabia katika familia nyingi ya kuwaharakisha vijana kwenye ndoa wakati pengine hawajawa tayari au bado hawajavutiwa na hatua hiyo. Jambo hili linaweza kusababisha hasara zaidi kuliko uzuri, na hali ya kila mhusika inahitaji kufikiriwa kipekee. Kwa lugha iliyo rahisi, yeyote anayekaribia kufunga ndoa anahitaji kuridhishwa na uamuzi huu.

## DALILI ZA KAWAIDA

**Silika:**

Mtu anayefaa sana kuamua kwamba upo tayari kufunga ndoa ni wewe mwenyewe. Kama vile tujuavyo tu kupitia sheria maumbile kwamba tunahitaji kula na kunywa, hivyo hivyo, haja za kisilika ambazo Mwenyezi Mungu ameziweka ndani ya wanadamu kwa ajili ya mwenza huamsha na kutusukuma sisi kutafuta mchumba.

Hata hivyo, matatizo hujitokeza pale silika hii inapokandamizwa kwa sababu yoyote. Vipengele vya nje kama vile vilivyoorodheshwa chini vinaweza kuwa na uzito mkubwa sana juu ya silika hii na



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 28 10/20/2015 4:31:57 PM

kuzuia mtu asivitambue kwa usahihi, na kuchukua hatua kuhusu hali hii. Vipengele hivi vinaweza kuwa ni pamoja na:

> Nilitambua kwamba niko tayari kuanza kutafuta pale nilipoanza kuhisi dalili za upweke, kama niliyekuwa ninakosa kitu fulani hivi…au mtu fulani. Ingawa wakati nilipoangalia huku na kule nilijikuta bado nimezungukwa na idadi ya watu ambao nilikuwa nao wakati wote katika maisha yangu. Hapo ndipo liliponigonga. Watu waliokuwa wamenizunguka hawakubadilika, mazingira yangu yalikuwa hayajabadilika – Mimi nilikuwa nimebadilika. Bila shaka niliingia katika kuanza kutafuta vitu vya kunikamilisha, kuziba mapengo. Wakati hilo likikwama, kama lilivyo dhahiri kwamba litashindikana, nilianza kutambua kwamba sio "kitu" ambacho kitaziba pengo hili, bali ni "mtu." – **Mwanamke, Marekani**

"Sina fedha ya kutosha."

"Bado sijapata shahada yangu."

"Jamii haiafiki mtu kufunga ndoa akiwa mdogo hivi."

"Siwezi kumpata anayekidhi vigezo vyangu."

"Itakuwaje kama mtu ninayemtafuta hajaniposa au hakubaliani na posa yangu?"

Kwenye Sura ya Kwanza tumeelezea vikwazo hivi vichache, ambapo kushinda baadhi ya viunzi vingine kunahitaji mabadiliko katika kutuliza mawazo na kuwa imara katika kumtegemea Mwenyezi Mungu.

## Ishara Zingine Mbali mbali

Ishara zingine zinazoonyesha kwamba upo tayari kuoa au kuolewa ni pomoja na kuona baadhi ya alama au zote zilizotajwa hapo chini:

a. Tamaa ya kujamiiana.

b. Kutaka kuwa na mwenza.

c. Upweke, pamoja na kwamba unaweza kuwa watu wamekuzunguka. Upweke huu unaweza kuwa ni hisia mpya ambayo unakutana nayo, hata kama marafiki zako wa nje nao wanakuwepo pale pale.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 30 10/20/2015 4:31:57 PM

# SURA YA 3.

# NIANGALIE NINI KWA MCHUMBA?

## UMUHIMU WA KUCHAGUA MCHUMBA MTARAJIWA

Swali kubwa linalofuata ni kuhusu kitu gani mtu anapaswa kuangalia ili kuweza kumtambua mwenye uwezekano wa kuwa mchumba?

Hili ni suala lisilotakiwa kuchukuliwa kirahisi, kwani unajaribu kuchagua mtu ambaye utatumia naye muda wa maisha yako uliobakia. Mbali ya kuchagua imani na dini yako mwenyewe, hakuna uchaguzi na uamuzi mwingine katika maisha unaoweza kulingana na huu. Ndani ya makala iitwayo *"21 Suggestions for Success"* (Mapendekezo 21 kwa ajili ya Kufuzu) iliyoandikwa na H Jackson Brown Junior, mwandishi mzuri sana wa *New York Times*, pendekezo namba moja ni "Funga ndoa na mtu sahihi. Uamuzi huu mmoja utabainisha 90% ya furaha au mateso yako."

Zaidi ya hayo, mara nyingi imesisitizwa kwamba hatua ya kwanza ya kupata watoto wema na wacha Mungu ni kuchagua mchumba sahihi; watoto hawarithi sadifa za kimaumbile tu za wazazi wao, pia huathiriwa na tabia bainifu na welekeo wa wazazi wao. Katika kuthibitisha hili, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Oa ndani ya kabila zuri, kwani kwa hakika kile kinachozaliwa juu ya mfupa



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 31 10/20/2015 4:31:57 PM

kitatokeza kwenye nyama."[16] Wazazi ndio msingi wa uhai wa watoto wao na ni wao ndio watakaoonyesha mifano kupitia na maneno yao na matendo yao. Methali moja mashuhuri ya kisekula inathibitisha jambo hili: "Mkono unaotingisha susu ndio hutawala dunia."

Ingawaje Uislamu unapendekeza kutokuchelewesha ndoa, hii haimaanishi kwamba mtu afanye haraka na asiwe mzingativu. Kwa usahihi zaidi ni kwamba lazima uwe mwangalifu na msikivu, na ujaribu kutokuruhusu kushughulishwa na mambo ya juu juu. Hata hivyo, hii haimaanishi ukwamishwe na uwe mwenye kuwa na wasiwasi kuhusu mambo madogo. Ni muhimu uwe na wastani. Jaribu kadiri uwezavyo, hakikisha nia yako ni safi. Halafu umwachie Muweza wa Yote.

## Ni Nani Niwezaye Kumuoa?

Kwanza, ni muhimu kumtambua yule ambaye Uislamu umeturuhusu sisi kuoana naye na si vinginevyo. Kuna vikwazo fulani juu ya uchaguzi wa mchumba wako kutegemea na uhusiano wa damu na wa kidini.

Sheria hizi zimefanyiwa mukhtasari kama ifuatavyo:[17]

### 1. Makatazo kwa msingi wa uhusiano wa damu.

Yapo mahusiano fulani ya damu ambayo ni haramu kwako kuhusiana na ndoa (kama kanuni ya kawaida, yeyote yule ambaye ni Maharimu wako[18] huruhusiwi kuoana naye). Orodha ya ndugu kama hao imeandikwa ndani ya Qur`ani kama ifuatavyo[19]:

---

16 *Kanz al-Ummal*, hadithi namba, 4455

17 *Marriage and Morals in Islam* (Ndoa na Maadili ndani ya Uislamu), Sayyid Muhammad Rizvi

18 Mahrimu: Ni kundi la watu ambao hairuhusiwi kisheria kuoana nao, kwa sababu ya undugu wa damu au hali ya kindoa.

19 Suratul al-Nisa (23-24)

**Kwa Wanamume:**

Mama, binti yako, shangazi, mamamkubwa, mamamdogo, mpwa, mama wa kunyonya, dada wa kunyonya, mama mkwe, binti wa kufikia, mke wa mwanao, wanawake wote walioolewa, shemeji yako (haiwezekani kwa mwanamume kumuoa shemeji yake wa kike - kama mke wake bado yu hai).

**Kwa Wanawake:**

Baba, mwanao mwanamume, mjomba, ami, mpwa wa kiume, mume wa mama yako wa kukunyonyesha, kaka wa kunyonya, baba mkwe, mtoto wa kufikia wa mume wako, mkwe wako wa kiume.

**2. Makatazo kwa Msingi wa dini.**

Mwislamu mwanamume wa Madhehebu ya Shia Ithna-Asheri, anaweza kumuoa mwanamke ambaye ni Shia Ithna-Asheri na mwanamke Mwislamu ambaye sio Shia Ithna-Asheri. Hata hivyo, endapo kuna dalili za hatari ya kutolewa kwenye imani yake kama Shia Ithna-Asheri, basi ndoa hiyo inakatazwa. Pia anaweza kumuoa mwanamke wa Kiyahudi au Mkristo kwa ndoa ya Muta tu. Lakini hawezi kuoa mwanamke wa imani nyingine yoyote ama katika ndoa ya kudumu au ya Muta.

Mwanamke wa Madhehebu ya Shia Ithna-Asheri anaweza kuolewa na: Mwanamume wa Madhehebu ya Shia Ithna-Asheri au mwanamume ambaye ni Miislamu lakini si wa Madhehebu ya Shia Ithna-Asheri, ingawaje ni bora kutofanya hivyo; na endapo zipo dalili za uwezekano wa kupotoshwa na kutoka kwenye imani yake, basi ndoa hiyo inakatazwa. Lakini katika hali yoyote ile hawezi kuolewa na mwanamume ambaye si Mwislamu.

**3. Kufunga ndoa na binamu.**

Ingawa sheria ya Kislamu haikatazi ndoa baina ya mabinamu, kuna mambo yanayojaribu kulizuia jambo hili. Mambo haya hasa zaidi ni kwa sababu ya ongezeko la hatari ya mtoto yeyote wa ndoa hiyo kurithi dosari za kijenetiki na magonjwa kama thalathemia.

## VIGEZO VYA KISLAMU[20]

Pili, kama ilivyo kwa vipengele vyote vya maisha yetu, Uislamu umeweka muongozo juu ya sifa zipi njema ambazo tunapaswa tuzitafute kwa mchumba. Tukiwa nazo sifa hizi katika akili zetu, itakuwa rahisi kuendelea katika mwelekeo ulio sahihi, Inshallah.

Sifa Hizi zimeorodheshwa kwa mukhtasari kama ifuatavyo hapa chini:[21]

**1. Ucha Mungu**

Mwandishi wa kitabu kiitwacho “Kijana na Kuchagua Mchumba” (*Youth and Spouse Selection*) anasema, “Mtu asiyekuwa na dini, hana chochote.”[22]

Mtu mmoja alipokwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kutafuta muongozo kwa ajili ya kuchagua mchumba, yeye (s.a.w.w.) alisema: “Ni sharti juu yako wewe kuwa na mchumba mcha Mungu.”[23]

Akiwa anajua udhaifu wa binadamu kwenye urembo na ukwasi, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameonya: “Mwanamume anayemuoa

20 *Youth and Spouse Selection*, Kijana na Kuchagua Mchumba, Ali Akbar Mazaheri

21 Kwa mapitio ya upana zaidi juu ya vigezo hivi, tafadhali rejea kwenye kitabu *Youth and Spouse Selection* cha Ali Akbar Mazaheri

22 *Youth and Spouse Selection* cha Ali Akbar Mazaheri

23 *Wasa`il ash-Shia*, Juz. 14, uk. 30



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 34 10/20/2015 4:31:57 PM

mwanamke kwa sababu ya ukwasi wake, Mwenyezi Mungu humwacha mtu huyo kwenye hali yake hiyo, na mtu anayemuoa mwanamke kwa uzuri wa sura yake tu, atakuta ndani mwake (vitu) ambavyo havipendi (adabu mbaya) na Mwenyezi Mungu ataviweka vitu hivi vyote pamoja (uzuri wa sura na ukwasi) kwa mtu anayemuoa mwanamke huyo kwa ajili ya imani yake (ucha Mungu)."[24]

## 2. Tabia Njema

Kigezo muhimu kinachofuatia ni kuwa na tabia njema. Baadhi ya sifa bainifu ambazo zimejumuishwa kwenye tabia njema ni pamoja na kutumia lugha stahifu, kuwa mkweli, kuwaheshimu watu wengine, kuwa mnyenyekevu, mkarimu na mwenye subira.

Imam ar-Ridhaa (a.s.) alimwandikia majibu mtu ambaye alimuuliza kama ni busara kumuoza mwanawe wa kike kwa mtu ambaye anajulikana kwa tabia yake mbaya. Imam (a.s.) akajibu: "Kama tabia yake si njema (mwenye hasira) usimuoze binti yako kwake."[25]

Ni utaratibu huo huo utatumika kwa bibi harusi mtarajiwa kama hana tabia njema. Mwanamke wa aina hiyo, ingawaje anaweza kuwa na sura nzuri na tajiri, atayafanya maisha ya mume wake kuwa ya mateso. Atajitahidi kuwa mvumilivu katika matatizo yanayojitokeza kwenye maisha ya ndoa.

## 3. Familia ya Heshima

Katika Uislamu, umuhimu hautolewi kwenye umaarufu, utajiri, au hadhi ya familia; badala yake unatolewa kwenye staha na udini na ucha Mungu wao. Aina ya familia ambayo unataka kuoa au kuole-

[24] *Wasa`il ash-Shia*, Juz. 14, uk. 31
[25] *Al-Kafi*, Juz. 5 uk. 563



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 35 10/20/2015 4:31:57 PM

wa inapaswa kufikiriwa kwa sababu kuu mbili muhimu. Kwanza, sifa zao kwa hakika kwa karibu sana zitafanana na zile za mchumba wako, kwa sababu ya urithi wa kinasaba na mazingira na mafunzo aliyopata mchumba wako wakati anakua. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Oa kutoka kwenye paja lenye heshima, kwani manii na jeni huwa zina athari."[26]

Pili, ni jambo lisiloepukika kwamba wakati wote mchumba wako atakuwa sehemu yao, atakuwa pamoja nao kwa muda mwingi, na pia watachukua nafasi katika maisha ya watoto wenu.

## 4. Akili

Inapendekezwa kwamba uchague mchumba mwenye akili. Hii haimaanishi kwamba ni lazima mchumba mtarajiwa wa kiume au wa kike awe amesoma, au kama amesoma, lazima awe amepasi vizuri, bali inarejelea uimara wa akili. Akili imara inaweza kutofautisha baina ya haki na batili, kupanga na kusimamia maisha ya heshima, na kukuza familia nzuri.

Imam Ali (a.s.) alikataza kwa juhudi zote kuoa mtu mjinga na mwenda wazimu, akisema: "Epuka kuoa mwanamke mjinga, kwani kuwa naye ni masikitiko na watoto wake pia, wataharibika."[27]

Ujuzi na elimu, pia, ni mambo ambayo yamesisitizwa sana katika Uislamu, na yana athari kubwa kwenye maisha ya watu.

## 5. Mwonekano

Ingawaje udini na ucha Mungu ni muhimu sana, haimaanishi kwamba hatutilii maanani mwonekano wa kimaumbile na sura nzuri ya mchumba mtarajiwa. Kinyume chake, kufanya hivyo itakuwa ni ku-

[26] *Makarimul Akhlaq*
[27] *Wasa`il ash-Shia*, Juz. 14, uk. 56



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 36 10/20/2015 4:31:57 PM

fanya kosa baya sana, kwani mvuto hufanya sehemu madhubuti ya ndoa nzuri.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema: Mtu anapotaka kuoa mwanamke, anapaswa kuuliza kuhusu nywele zake, kama vile anavyouliza kuhusu uzuri wake wa sura (uso), kwani nywele ni mojawapo ya aina mbili za uzuri wa (wanawake).[28]

## 6. Mchukuano

Umuhimu wa mchukuano baina ya wanandoa hao hauwezi kusisitizwa vya kutosha, na kukosekana kwa hili mara nyingi huwa ndiyo sababu ya ndoa zenye matatizo. Hii ni kwa sababu ndoa ni muungano wa watu wawili na familia zao, na jinsi ulinganifu na usawa wa watu hawa wawili unavyokuwa imara, ndivyo uhusiano wao utakavyokuwa na nguvu zaidi.

Ni muhimu kufafanua nini maana ya mchukuano. Katika kuchagua mchumba, hakurejeshi kwenye tofauti ya matabaka au mambo mengine ya kimaada kama hayo, wala haimaanishi kutafuta mtu ambaye atafanana kwa usahihi kabisa kuhusu historia yake na utamaduni wake na ule wa kwako; bali kinachomaanishwa ni upatanifu wa yote, mambo ya kiroho na kimwili, pale ambapo tabia za wanandoa zinakuwa na uwiano na kukamilishana zenyewe kwa zenyewe.

Ni dhahiri, haiwezekani kumpata mtu mwenye hali ya kuchukuana na wewe kwa ukamilifu kabisa, na pia ipo mifano inayotuzunguka ya wawili walioonekana kuwa hawana mchukuano, lakini wameoana na kufaulu katika mahusiano yao; hata hivyo, kwa sehemu kubwa, inapendekezwa kuitafuta sifa hiyo.

Hapa chini yapo maeneo maalum ambamo hali ya mchukuano imependekezwa:

[28] *Bihar al-Anwar*, Juz. 103, uk. 237

**a. Uwana Dini**

Ni vema zaidi kwa yule mwanamke ambaye ameshikamana na sheria na kanuni kuolewa na mwanamume aliye kama yeye.

> Mimi na mume wangu tunatokana na halfia za tamaduni tofauti, na kutokana na fikra yangu, pamoja na kwamba changamoto zinakuwepo kuhusiana na tofauti hii, sidhani kama ni mbaya zaidi kuliko zile zinazowekwa na ndoa ya wenye tamaduni moja. Alhamdulillah, ninahisi kwamba ndoa yetu imefanikiwa na itaendelea kufanikiwa kwa sababu tunayo mawazo yanayofanana kuhusu jinsi ya kutekeleza dini na mambo ya kiroho ndani ya maisha yetu. Tangu mwanzoni, sote wawili tulikuwa na maono yanayofanana ya jinsi gani tulitaka watoto wetu walelewe, na familia yetu iendeshwe namna gani. Uelewa huu wa pamoja uliunda msingi wa mahusiano yetu. Kwa sababu tulikubaliana kwenye mambo muhimu zaidi katika maisha (yaani dini, falsafa ya maisha, kulea watoto, na kadhalika), tofauti ndogondogo zingeweza kumalizwa kupitia mazungumzo na masikilizano." - **Mwanamke, Marekani.**

Mtu mmoja alimuuliza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Ni kina nani ambao lazima tuwaoe?" Yeye akajibu: "Wale wanaofaa." "Ni kina nani hao wanaofaa?" Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Watu wa imani ni wenza sawa na watu wa imani."[29]

Imam Sadiq (a.s.) alisema yafuatayo kuhusu Bibi Fatima (a.s.) "Kama Mwenyezi Mungu asingemuumba Ali, hapangekuwepo na mwanamume mwenye hali ya kuchukuana na kuwa sawa naye Fatima hapa duniani toka enzi za Adam hadi mwisho wa dunia."[30]

---

[29] *Wasa`il ash-Shia*, Jz. 14, uk. 563

[30] *Bihar al-Anwar*, Jz. 43, uk. 92



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 38 10/20/2015 4:31:57 PM

**b. Akili**

Imam Sadiq (a.s.) amesema: "Mwanamke mwenye akili na hekima lazima asiolewe na yeyote isipokuwa mtu mwenye busara na hekima."[31]

Ishara za wazi juu ya jinsi ya kuhakiki kama mchumba mtarajiwa analingana na vigezo vilivyotajwa hapo juu zimezungumziwa kwenye Sura ya 6.

[31] *Al-Kafi*, Jz. 5, uk. 350



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 39 10/20/2015 4:31:57 PM

# SURA YA 4

# KANUNI MUHIMU ZA FIQHI:

## SEHEMU YA 1-
## MLOLONGO WA UCHUNGUZI

### Mchakato wa Uchunguzi Katika Uisalmu

Kama ilivyo kwa vipengele vyote vya maisha yetu, sura na muundo ambao mchakato wa kuchagua mchumba huchukua hutegemea juu ya Sheria ya Kiislamu. Kwa hiyo, ili kuweza kutafuta na kuelewa mbinu inayofaa ya kuchagua mchumba, ni muhimu kutambua kanuni za fiqhi za msingi.

Kwa ajili ya kusudio hili, kanuni muhimu za fiqhi zimesisitiziwa hapo chini zinazohusiana na uchaguzi wa mchumba na kipindi cha uchumba kwa mujibu wa Ayatullah al-Uzma Sayyid Ali al-Husaini as-Sistani.[32]

### Kanuni za Uchunguzi

Utafiti kuhusu mwenye uwezekano wa kuwa mchumba mtarajiwa hufanyika ama kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia ya mzunguko. Uchunguzi wa moja kwa moja ni pale wote mwanamume na mwanamke wanapoulizana kuhusu mambo wao kwa wao, ambapo uchunguzi wa mzunguko ni pale ambapo wanaulizia kuhusu mwenye uwezekano wa kuwa mchumba mtarajiwa kutoka kwa mtu mwingine (kama vile rafiki, ndugu wa mhusika, mtu aliyeko katika jumuiya hiyo, jirani na kadhalika).

[32] Mfumo wa maadili kwa Waislamu wanamume na wanawake.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 40 10/20/2015 4:31:57 PM

Kanuni za mbinu hizi zote za uchunguzi zimetolewa hapa chini:

**Kanuni za uchunguzi wa njia ya mzunguko:**

- Inaruhusiwa kufanya utafiti na uchunguzi kuhusu yeyote kati ya wachumba watarajiwa kutoka kwa mtu yeyote, hata kama italazimika kutafuta makosa yake au yale ya familia yake husika.[33]

    Hata hivyo, mtu anaruhusiwa kuchunguza dosari zile zinazohusiana na ndoa tu na kumjua mhusika wa upande mwingine (kuhusu maisha ya ndoa). Katika hali zingine zote, hairuhusiwi kutafiti katika maeneo mengine ya maisha ya mtu kwa kisingizio cha uongo juu ya ndoa.

**Kanuni za Uchunguzi wa Moja kwa Moja**

- Kila mmoja wa mchumba mtarajiwa anaruhusiwa kumuuliza mwenzake moja kwa moja kuhusu wao wenyewe, kwa sharti kwamba uchunguzi huu hauruhusu vitendo vyovyote vilivyoharamishwa.[34]

**ANGALIZO:** Inakatazwa kwa hao wawili kuzungumza wakati wakiwa na hisia za ashki yoyote ile, au kwa wao kuwa peke yao mahali kwenye faragha, au kugusana ama kwa ashki au la, na hivyo lazima wajiepushe na mambo haya.

- Kila mchumba mtarajiwa anaweza kuangalia picha ya mwingine (kwa lengo la kuona uzuri wake) kwa kusudio la ndoa, alimuradi masharti mengine yafuatayo yanatimizwa:

    a. Mwanamume anaweza kuangalia picha ya mwanamke ambaye si Maharimu kwake ambaye amevaa vazi la

---

[33] *Ibid,* Kanuni ya 229
[34] *Ibid,* Kanuni ya 231

hijabu kikamilifu, kwa sharti kwamba si kwa nia ya kupata starehe au furaha.[35]

b. Kama mwanamke ambaye si Maharimu ndiye yumo kwenye picha na hakuvaa vazi la hijabu kwa ukamilifu, halafu inatokea kwamba mwanamke kwa kawaida ni yule ambaye huvaa hijabu kamilifu na mwanamume anayeiangalia picha hiyo anamtambua, haruhusiwi kutazama picha hiyo.[36]

c. Kama mwanamke ambaye yumo kwenye picha si Maharimu na hajavaa vazi kamili la hijabu, lakini yeye ni miongoni mwa wale ambao hawavai vazi la hijabu kikamilifu au havai hijabu kabisa, na hata kama angeambiwa kuvaa lakini asingesikiliza, basi si tatizo kutazama picha yake.[37]

## Kanuni za Kuchanganyikana Kijamii

Alimuradi watu wawili hawajatamka aina yoyote ya mkataba wa ndoa, wao si Maharimu kwa kila mmojawao. Kwa hiyo, ni muhimu kutambua kanuni za kuchanganyikana kijamii ambazo hutawala mwenendo baina ya wale wasio Maharimu.

## Kwa Wanamume:

- Wanamume wanaruhusiwa kuwasemesha wanawake ambao si Maharimu kwao alimuradi masharti haya mawili yanazingatiwa:[38]

1. Si kwa nia ya ashki.

[35] *Ibid,* Kanuni ya 57
[36] *Ibid,* Kanuni ya 58
[37] *Ibid,* Kanuni ya 58
[38] *Ibid,* Kanuni ya 172



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 42 10/20/2015 4:31:57 PM

2. Mazungumzo hayo yasielekee kumfanya mmojawao afanye dhambi.

- Kama mwanamume anajua kwamba akizungumza na mwanamke ambaye si Maharimu kwake ataangukia kwenye dhambi, basi ni lazima asizungumze naye; ama iwe kwa sababu ya jinsi azungumzavyo mwanamke au mada ni ile ambayo itamfanya mwanamume afanye dhambi.[39]
- Hairuhusiwi kuzungumza na mtu kuhusu kitu chochote ambacho kinahusiana na masuala ya mapenzi au umwanandani (isipokuwa kwa mwenza wake).[40]

**Kwa Wanawake:**

- Wanawake huwa wanaruhusiwa kuzungumza na wanamume ambao si Maharimu wao endapo masharti yafuatayo yatazingatiwa:[41]

a. Mazungumzo hayo hayafanywi kwa nia ya ashki na kutaka kupata starehe ya ngono.

b. Mwanamke asiifanye sauti yake kuwa nyororo na ya kuvutia (hivyo kwamba mwanamume anaweza kuvutiwa kwake, hata kama anazungumza kuhusu mada ya kawaida).[42]

c. Pasiwepo na hofu ya kuangukia kwenye uovu.

**Hitimisho**

Katika kuhitimisha, wakati wa kipindi cha uchunguzi na katika nyakati zingine zote, endapo nia inageuka kuwa ya kiashki waka-

[39] *Ibid,* Kanuni ya 174
[40] *Ibid,* Kanuni ya 181
[41] *Ibid,* Kanuni ya 192
[42] *Ibid,* Kanuni ya 185

ti wa mazungumzo, mawasiliano haya ni kinyume cha sheria na hayaruhusiwi. Kwa hiyo matokeo ni kwamba mazungumzo na mawasiliano yanahitaji kuwekewa mipaka na yanaweza kuendelea tu kabla ya wakati ambapo hayajaonekana ya kukatazwa



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 44 10/20/2015 4:31:58 PM

# SURA YA 5

# MBINU ZA KUCHAGUA MCHUMBA

## MBINU ZA KUCHAGUA MCHUMBA KATIKA UISLAMU

Ambapo ndani ya jamii ya nchi za Magharibi kuchanganyikana kijamii baina ya wanamume na wanawake ni jambo la kawaida, hali hii imepingwa na kukatazwa katika Uislamu, kama ilivyosisitiziwa na Sheria ya Kislamu kama ilivyozungumziwa ndani ya Sura ya 4.

Zaidi ya hayo, kwa sababu uamuzi huu ni wa msingi sana katika kuamua maisha yako yote, ni muhimu kwamba unapata utambuzi kamili kwamba yule unayemchagua NDIYE huyo hasa. Huu ni umuhimu usioepukika kulingana na mwandishi wa "Kijana na Uchaguzi wa Mchumba" (Youth and Spouse Selection), na kwa hiyo ni uamuzi ambao hautakiwi kufanywa kwa wepesi. Njia hii hufanya kazi pande zote mbili, yaani mchumba lazima akubaliwe na wewe tu mara unapokuwa na uhakika kuwa huyo ndiye sahihi kwa ajili yako, na vivyo hivyo mwenza mtarajiwa anaweza kukataliwa na wewe tu mara unapokuwa na uhakika kwamba huyo si sahihi kwa ajili yako.

Tukiwa tunazingatia hayo hapo juu, na pia kutaka kufikia vigezo vya Kislamu ambavyo vimezungumziwa kwenye sura ya nyuma, yanatokeza maswali mawili muhimu pale ambapo ndoa inafikiriwa.

**1.** Nitampataje yule ambaye ninaweza kudhani anaweza kuwa mwenye kufaa?

**2.** Nitawezaje kuwajua ili niweze kufanya uamuzi? Maswali haya sasa yatajibiwa kwa kina.

### Nitampataje yule ambaye ninaweza kudhani anaweza kuwa mwenye kufaa?

Kimbilio la kwanza la kuendea ni wazazi, ambao wanatambua vizuri sana utu wako na aina ya haiba ambayo mwenza wako anatakiwa kuwa nayo ya kukufaa wewe. Pia wao wanakutakia kilicho bora kwa hiyo inahakikishwa kwamba wataendelea kujaribu!

Wapatanishaji, au 'Washenga' ni kituo kingine muhimu cha kuendea. Watu hawa sio kwamba wanasaidia tu kwa kupendekeza wachumba watarajiwa wenye uwezekano bali pia baadaye husaidia, katika mchakato wa kuwatambulisha hao wawili na kupanga mikutano, na kadhalika. Jumuiya zilizo nyingi zina kamati zenye 'washenga' kama hao. Hata hivyo, mara kwa mara unapaswa kujaribu kuhakikisha kwamba wapatanishaji ni watu wa kuaminika, wanao uzoefu wa michakato hiyo, na wanao ujuzi na utambuzi wa kutosha kuhusu matatizo ya uchaguzi wa mchumba mtarajiwa na ndoa.

Hivi karibuni kumekuwa na hatua chanya ya washenga ya kusaidia kuweza kuwajua vema zaidi watu ambao wanajaribu kuwakutanisha kupitia mikutano ya ana kwa ana ya wahusika na maelezo mengi ya kina, badala ya taarifa ya kawaida kama umri, urefu, na taaluma. Hili ni muhimu na linaweza na linapaswa kufanywa na pande husika zenyewe, kwani viwango vya juu vya mafanikio vimepatikana pale ambapo mshenga anazijua yeye binafsi pande zote mbili. Wazazi na washenga wanapaswa kuzingatia kwamba wakati wakiwa wanaweza kupendekeza mchumba mtarajiwa kwa ajili ya watoto wao, uamuzi wa mwisho



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 46 10/20/2015 4:31:58 PM

wa kuendelea uko mikononi mwa watoto wenyewe. Wakati mwingine, inawezekana ukawa umesikia, umeona, au kukutana na mtu, kwenye harusi, chuo kikuu, au mahali pengine popote, na unataka kuliendeleza jambo hilo. Endapo hali ikiwa hivyo, basi tena, unapaswa kuzungumza na wazazi au washenga wengine wanaofaa ambao wanaweza kufanya mawasiliano na upande mwingine na kuendeleza jambo hilo mbele.

“Nikiwa aina ya mtu huru, nilijikuta kwenye hali ya utata nilipoanza kuendeleza mambo na mtu ambaye alikuwa akilini mwangu. Kwa upande mmoja, sikuwa na furaha ya kweli kupitia kwa washenga wengi mno kwa ajili ya kufanya yale mawasiliano ya kwanza lakini wakati huo huo pia nilikubaliana na hali hiyo ili kudumisha heshima kwenye hali tete kama hii ingekuwa ni ujinga mkubwa kwangu mimi kujaribu na kufanya mpango wa mawasiliano mimi mwenyewe - hivi kweli nilikuwa ninamtaka huyu mchumba wangu mtarajiwa kuwa wa aina ambayo angeitikia utangulizi wa moja kwa moja kama huo kwa vyovyote vile? Nashukuru kutokana na jumuiya ambayo mimi nilikuwamo, niliweza kumtambua mtu fulani ambaye si tu alikuwa anamjua mtu huyo mhusika bali pia alikuwa ananijua mimi na nilihisi kujiamini kwamba atakuwa na tahadhari na pia kutoa utambulisho wangu kwa njia ambayo mimi ningefanya. Bila shaka ilikuwa pia muhimu kwamba mtu huyu ambaye alikuwa anachukua dhima kwa ajili yangu alikuwa yeye mwenyewe ni mtu wa muonekano wa heshima na kuaminika ili kuweza kupandikiza kujiamini kwa mchumba mtarajiwa.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 47 10/20/2015 4:31:58 PM

Mara alipofanya mawasiliano ya kwanza na baba yake, niliweza kukutana na mtu huyo kwenye mazingira mazuri ya "Nikiwa aina ya mtu huru, nilijikuta kwenye hali ya utata nilipoanza kuendeleza mambo na mtu ambaye alikuwa akilini mwangu. Kwa upande mmoja, sikuwa na furaha ya kweli kupitia kwa washenga wengi mno kwa ajili ya kufanya yale mawasiliano ya kwanza lakini wakati huo huo pia nilikubaliana na hali hiyo ili kudumisha heshima kwenye hali tete kama hii ingekuwa ni ujinga mkubwa kwangu mimi kujaribu na kufanya mpango wa mawasiliano mimi mwenyewe - hivi kweli nilikuwa ninamtaka huyu mchumba wangu mtarajiwa kuwa wa aina ambayo angeitikia utangulizi wa moja kwa moja kama huo kwa vyovyote vile? Nashukuru kutokana na jumuiya ambayo mimi nilikuwamo, niliweza kumtambua mtu fulani ambaye si tu alikuwa anamjua mtu huyo mhusika bali pia alikuwa ananijua mimi na nilihisi kujiamini kwamba atakuwa na tahadhari na pia kutoa utambulisho wangu kwa njia ambayo mimi ningefanya. Bila shaka ilikuwa pia muhimu kwamba mtu huyu ambaye alikuwa anachukua dhima kwa ajili yangu alikuwa yeye mwenyewe ni mtu wa muonekano wa heshima na kuaminika ili kuweza kupandikiza kujiamini kwa mchumba mtarajiwa.

Mara alipofanya mawasiliano ya kwanza na baba yake, niliweza kukutana na mtu huyo kwenye mazingira mazuri ya hadhara ya watu wengi nikiwa na utambuzi badala ya 'uingiliaji hai' au mahudhurio ya moja kwa moja ya familia zote mbili. Mchakato huu ulinifanyia kazi nzuri kwani hata hivyo ingawa familia yangu mara zote walikuwa wanapata taarifa, bado nilikuwa na hisia kwamba mchakato huo ulikuwa mikononi mwangu, hivyo ulipunguza shinikizo lisilokuwa la lazima ambalo lingeathiri uamuzi wangu." **Mwanamume – Uingereza.**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 48 10/20/2015 4:31:58 PM

## Nani Amuulize Nani?

Kwa kawaida, kila mara imekuwa ni kijana (mwanamume) na familia yake ndiyo wanaoanza mazungumzo katika posa yoyote. Hata hivyo, hili halina msingi wowote wa lazima katika Uislamu. Mfano uliowekwa na Bibi Khadija (a.s.) na Mtume Muhammad (s.a.w.w.) unasimama kama somo zuri kwetu kwamba zoezi hili haliihitaji kuwa desturi na zaidi ni kipingamizi cha kitamaduni kuliko kuwa cha kidini.

Bibi Khadija (a.s.), mmiliki wa msafara wa biashara mkubwa kabisa katika eneo hilo, alimwendea Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kupitia kwa mshenga. Katika msafara wake wa kwanza, ambao ulikuwa wa kwenda Syria, alimpatia faida kubwa sana kwenye biashara yake, na pia Khadija alipendezewa na taarifa zilizomfikia yeye, kumhusu Mtume kutoka kwa mhasibu wake, Maysara ambaye alifuatana na kundi hilo.

Ingawa Bibi Khadija (a.s.) alishapokea na kukataa posa nyingi kutoka kwa waposaji matajiri na wenye uwezo, kwa kweli yeye alichukua hatua ya kwanza na kupeleka posa ya ndoa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kupitia kwa mtumishi wake mwanamke, aliyeitwa Nafisa. Halafu Bibi Khadija (a.s.) alipeleka posa rasmi kupitia kwa Hadhrat Abu Talib (a.s.) ammi yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye ndiye akazungumza na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na jambo hilo likakamilishwa. Kwa hiyo, jambo la posa linaweza na linapaswa kuanzishwa na kuendelezwa na upande wowote unaovutiwa, iwe upande wa mwanamume au mwanamke.

## Nitawajuaje Ili Niweze Kufanya Uamuzi?

Baada ya yule mwenye uwezekano wa kuwa mchumba akishatambuliwa, mchakato wa kiuchunguzi ufuatao kwa kawaida unafanyika.

## 1. Upelelezi wa Njia ya Mzunguko

Pande zote mbili kila mmoja unaulizia kuhusu upande mwingine. Mchakato huu hufanyika kwa kuwauliza ndugu zao, marafiki zao, wafanyakazi wenzao, watu wa jumuiya, jamaa wanaofahamiana nao na kadhalika. Kwa dhahiri kiasi cha uchunguzi hutofautiana kutegemea na mhusika unamjua kiasi gani. Kuna mambo fulani ya mtu ambayo kwa kawaida huchunguzwa. Na hayo ni:

- Sifa za familia ya mhusika: Tabia zinazo mwelekeo wa kufuata mkondo ndani ya familia, kwa hiyo, kwa kufikiria hili unaweza kupata baadhi ya maoni kuhusu sifa na maadili ya mtu. Wakati fulani Mtume alisema: "Oeni miongoni mwa kundi fulani fulani kwani wao ni watu wa staha, hivyo wanawake wao pia wamekuwa na staha. Na msioe miongoni mwa kundi la watu fulani fulani, kwani wanamume zao walifanya vitendo vichafu, kwa hiyo wanawake zao pia wamekuwa wachafu."
- Sifa za mtu mwenye uwezekano wa kuwa mchumba: kwa ujumla watu wanayo maoni gani kuhusu wao, sifa zao kwa ujumla, wanajihusisha na aina gani ya mambo (kwa mfano madrassa, na kadhalika), kwa wakati huu wanafanya nini kama vile masomo na kazi, na kadhalika.

Kuna umuhimu mkubwa kwamba kanuni na masharti ya uchunguzi yaliyozungumziwa ndani ya Sura ya 4 yanafuatwa, kuhakikisha kwamba Sheria ya Kislamu inafuatwa, na kwamba hakuna uchunguzi mwingine usio wa lazima unafanywa kwa kusudio lingine lolote, wala taarifa inayopatikana isije ikatumika vibaya

> "Mimi mwenyewe nimepita kwenye mchakato mara nyingi zaidi kuliko ambavyo ningependa. Kila mara, kwa kawaida ilianza na barua pepe halafu ikaendelea hadi kwenye kukutana. Kutokana na uzoefu wangu nitakwambia hivi - kamwe hautajua kwa uhakika ila hapo utakapokutana naye, kwa hiyo hakikisha kwamba hilo linatokea mapema sana kwenye uhusiano wenu."
> **Mwanamke, Marekani, (USA)**

### 2. Picha

Hatua inayofuatia kwa kawaida huwa ni kubadilishana picha. Kwa mara nyingine tena kanuni na masharti ndani ya Sura ya 4 lazima yafuatwe. Picha inatakiwa kutumika kama muongozo tu katika kumtambua mtu na haipaswi kutumika kwa ajili ya kumkubali au kumkataa mtu kabisa.

Hata hivyo, hatua hii sasa inazidi kupungua katika matumizi na kujaribu kuzuiwa. Hii ni kwa sababu mara nyingi watu huangukia kwenye mazoea ya kuegemeza uamuzi wao juu ya ama kuendelea au la juu ya msingi wa picha. Hii ni kuliangalia jambo hili kirahisi mno na inazinyima pande zote mbili fursa ya kujuana kweli kweli kuhusu haiba ya kila mmoja wao na maadili yake. Inapaswa kufahamika kwamba picha haziwasilishi uhalisi inavyofaa hasa. Mara nyingi pia imegundulika kwamba jinsi unavyozidi kumjua mtu, ndivyo unavyozidi kumwelewa kwa tofauti zaidi.

### 3. Barua-Pepe

Baadhi ya watu hupendelea kuchagua kuwasiliana kupitia barua pepe, alimuradi wana baraka za wazazi wao. Barua-pepe hizi zinapaswa kutumika kwa ajili ya mambo yanayoendelea kama vile malengo,



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 51 10/20/2015 4:31:58 PM

matakwa na matumaini kwa ajili ya wachumba na mipango yao ya baadaye. Haya yamezungumziwa zaidi kwa kina katika Sura ya 6.

Barua pepe hazipaswi kuwa za hali ya kuzidi mambo mengi mno ya kibinafsi na burudani; si tu kwamba inawezekana kuwa haramu na yenye kukatazwa, lakini pia kwa sababu mambo kama hayo yanaweza kuufunika uwezo wako wa kufanya uamuzi unaofaa. Kuwa na mtu ambaye anajua mambo mengi ya maisha yako kwa kina pia inaweza kuwa si jambo linalofaa iwapo lengo la kuchumbiana halitafanikiwa, kwa wakati wote kuna uwezekano wa kufedheheka kwani hautakuwa na udhibiti wa taarifa zako za siri na jinsi zinavyotumiwa.

Kwa hiyo, mchakato wa barua pepe hautakiwi kuendelezwa kwa muda mrefu sana ili kwamba haya matatizo yenye uwezekano wa kutokeza yazuiwe, na pia kwa sababu kuna mambo mengi sana unayoweza kutokana na maandishi; mkutano wa ana kwa ana unaweza kukupatia picha iliyo kamili zaidi ya tabia ya mtu. Pia maneno yanaweza kufasiriwa vibaya kwa urahisi, hususani kama mpo katika kuanza kujuana tu na hisia zikawa zinahusika.

### 4. Mawasiliano ya simu

Masuala hayo hapo juu pia yanaweza kuzungumziwa kwenye simu kama pande zote mbili zitapendelea, ingawaje tena pia pawepo na baraka za wazazi. Inapaswa kuwekwa mipaka juu ya urefu wa muda wa mazungumzo na idadi ya marudio ya simu. Endapo patakuwepo na kupiga zaidi ya simu moja, inapendekezwa kuwe na mwanya wenye heshima na wa kufaa baina ya kupiga simu moja na nyingine kwa ajili ya kuruhusu kutafakari na kufikiria.

Sawa na zile nukta zilizotajwa hapo juu, upigaji simu hautoi picha kamili ya mtu, na hususani inaweza kufanya hali kuwa ngumu



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 52 10/20/2015 4:31:58 PM

na kufedhehesha ya kumuuliza maswali ya maisha binafsi mtu ambaye ni mgeni kwako.

**5. Mikutano**

Mfumo huu wa desturi ya 'kukutana' labda ni mojawapo ya mifumo inayofaa sana kwa nafasi ya kuwawezesha wenza watarajiwa kukutana. Ndiyo, mikutano si mara zote inakuwa ya kawaida wala mandhari inayofaa sana ambapo utakutana na mume au mke wako wa siku zijazo, lakini imejaribiwa na kupimwa na kuonekana kuwa ni mbinu inayofaa sana na iliyofuzu katika masuala ya ndoa.

Mara familia za pande zote mbili zikiwa zimekwisha wasiliana kuhusu suala hili (ama kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia ya mshenga), tarehe na muda wa mkutano wa kwanza inawezekana ikapangwa. Kwa kawaida hasa, lifuatalo huwa litatokea, ingawaje linaweza kutofautiana kutoka  hali moja na hali nyingine:

Mvulana na wazazi wake au baadhi ya watu wa familia yake watakwenda nyumbani kwa msichana (mchumba mtarajiwa) kupata chai au kula chakula. Mvulana atatambulishwa kwa watu wa upande wa msichana, na halafu msichana atatokeza na kutambulishwa kwa watu wa upande wa mvulana. Pande zote mbili zitakaa kwa muda kiasi, na baada ya hapo itapendekezwa kwamba mvulana na msichana waende kuzungumza kwa muda mfupi ndani ya chumba kingine; lazima izingatiwe hapa kwamba eneo hilo ni lazima lisiwe la faragha moja kwa moja au lililofungwa milango.

Msichana na mvulana sasa watakuwa na muda wa kuvunja ukimya na kuanza kuulizana maswali; zoezi hili linaweza kuchukua saa 1 au 2, au hata zaidi. Kwa wakati huu, watatakiwa kurudi na kuungana na familia zao, na upande wa mvulana wataondoka muda mfupi baada ya hapo. Hawa vijana wawili watahimizwa kukutana



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 53 10/20/2015 4:31:58 PM

tena, au kuwasiliana kupitia na njia zingine (barua pepe, simu – njia hizi sasa zitatumika kwa lengo la kupanua mikutano) kabla ya kufanyika uamuzi; mchakato wa kufanya uamuzi umezungumziwa kwenye kurasa za mbele ndani ya kitabu hiki.

Hivi karibuni, pamefanyika mabadiliko ndani ya desturi hii, ambapo wachumba sasa wanaonekana kuanza kuchagua kukutana wao kwa wao mbali na nyumbani; mathalani kwenye mgahawa au sehemu inayofanana na hiyo, ili kupunguza urasimu uliomo kwenye mfumo huu. Wakati wote mabadiliko haya yanapaswa kufanywa kwa ruhusa ya wazazi, na utambuzi wa Sheria ya Kislamu. Bila kujali mahali, mojawapo ya faida kubwa ya mkutano huu ni kwamba pande zote mbili zinaweza kugundua na kuelewa mengi kuhusu haiba ya ujumla ya upande mwingine. Imam Ali (a.s.) amesema: Chochote anachofikiria mtu kuhusu lolote hudhihirishwa na utelezaji wa ulimi na hisia za uso."

Zaidi ya hayo, huruhusu wachumba kuona muonekano na umbile la kimwili la kila mmoja; kwa wachumba kuishi pamoja kama mume na mke, ni muhimu kwamba pamoja na ulinganifu kwenye vipengele vingine, wanapaswa kumuona kila mmojawao anavutia na kupendeza. Kuhusiana na hili, tunazikuta hadithi nyingi. Bwana mmoja aitwaye Mughayra bin Shu`ba alimposa mwanamke, lakini alikuwa hajamuona sawasawa. Mtume akamwambia: "Kama ungekuwa umemuona, pangekuwepo na matumaini zaidi ya mkataba mrefu na wa kudumu na maelewano baina yenu wawili (katika maisha yenu)."[43]

Pia Mtume (s.a.w.w.) alimwambia mmoja wa masahaba wake ambaye alitaka kumposa mwanamke: "Mwangalie mwanamke uso wake na mikono yake."[44] Mtu mmoja alimuuliza Imam Sadiq (a.s.)

[43] *Wasa'il ash-Shi'ah*

[44] *Mustadrak al-Wasa'il*

"Je, mwanamume anayetaka kumuoa mwanamke anaweza kuona nywele zake na urembo wake?" Imam (a.s.) alijibu: "Hakuna tatizo kama hana nia ya kulifurahia hilo (yaani awe anafanya hivyo kwa kusudio la kuoa na si kuashki)."[45]

## Kuchagua Msiri

Jambo la lazima na muhimu katika safari hii ya kutafuta mwenza wa maisha ni kuweza kuwa na Imani na mtu wa kumwamini; ndoa ni moja ya maamuzi matatu ambayo utayafanya katika maisha yako - mengine mawili yakiwa ni imani unayochagua na kazi unayochagua.

Kwa hiyo, ni muhimu kabisa kwamba unampata mtu unayeweza kuzungumza naye katika mchakato wote, unayeweza kushirikiana naye hisia za kuvunja moyo na za furaha, mtu anayeweza kufasiri hisia zako na labda akusaidie kuona picha kubwa zaidi pale ambapo wewe huwezi, na ambaye unayeweza kutaka ushauri mzuri kutoka kwake.

Ni busara kwamba unampata mtu ambaye ame kuzidi umri, ambaye unamtegemea ambaye ameoa na kwa hiyo atakuwa amepita kwenye angalau sehemu ya mlolongo huo kama si wote. Si lazima iwe mtu mmoja tu. Inaweza kuwa watu wawili au watatu ambao wapo karibu na wewe na unaowaamini kwa ukamilifu. Itakuwa ni bora zaidi, mtu huyo awe yule ambaye unaweza kuomba ushauri kutoka kwake sasa, wakati wa harusi inayotarajiwa, na baadaye, yaani mtu unayemuona kuwa msindikizaji bwana harusi mzuri sana wa kweli.

Mwishoni, mara zote rudi kwa wazazi wako pia na kutaka ushauri kutoka kwao, kwani wao ni watu ambao si tu wameweka maslahi yako mazuri sana ndani ya nyoyo zao, lakini wakati wote

[45] *Wasa'il as-Shi'ah,* Juz. 14, uk. 60



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 55 10/20/2015 4:31:58 PM

watakutakia kila la kheri na kukupenda wewe bila masharti.

> "Kukutana na mtu ni mchakato wenye kuogofya sana. Haijalishi unakutana naye mara ngapi, 'uzoefu' wa kiwango gani unadhani unao kuhusu suala hilo, kila mtakapokutana hali iko tofauti, na kila mara unahisi kama vile ndiyo mnakutana kwa mara ya kwanza na kamwe hamjakutana bado. Neva zinasisimka, viganja vya mikono vinaanza kutoka jasho, na bado umezidiwa kabisa na hali ya 'Vipi kama hakuna jambo la kuzungumzia?!' Hofu. Kinachofanyika hapa ni kwamba jambo hilo si mchezo, bali ni jambo ambalo wengi wetu hufanya wakati wanatafuta 'yule makhsusi hasa'. Lakini unajua nini? Inshallah unapokutana na mtu ambaye ni sawa yako, hisia hizo hutoweka haraka. Na unajua nini tena? Mkutano umefanya kazi kwa ajili ya watoto wangu, mabinamu zangu, na pia kwa ajili yangu mwenyewe." -
> **Mwanamke, Marekani, (USA)**

**Kuupatia Mchakato Changamoto**

Ndani ya nchi za Magharibi, tunaishi kwenye jamii ambamo kuwekeana miadi na kukaa kinyumba kabla ya ndoa ni kawaida inayokubalika kwa watu wawili katika kutambuana. Vijana, wanaume na wanawake kwa mfululizo wanakutanishwa kwenye vyuo vikuu na sehemu za kazi. Hii inamaanisha kwamba ni jambo lisiloepukika kwamba mbinu za kimila kama zilivyozungumziwa ndani ya kitabu hiki zinapewa changamoto wakati wote.

Fikra inayopewa changamoto na vijana wa jumuiya zetu mara nyingi zaidi ni, "Inawezekanaje kujua kwamba umempata mtu aliye sawa yako, baada ya muda mfupi kama huo wa mawasiliano?" Swali



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 56 10/20/2015 4:31:58 PM

hili ni la msingi na litaelezewa kwenye sura zifuatazo kwa undani zaidi.

Hata hivyo, tukiliangalia jambo hili kwa ukaribu zaidi, tutaona kwamba suala halisi si mfumo wa mikutano tulionao sisi. Kwa usahihi zaidi ni utambulisho wa mwanzo hilo ndilo tatizo, yaani tunapaswa kwenda kukutana na nani, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na taarifa za kutosha na matayarisho juu ya jinsi ya kutumia fursa ya mkutano huo na kitu gani cha kutarajiwa kutokana na mkutano huo, hilo ndilo suala halisi linalosababisha matatizo.

Inshallah, taarifa iliomo ndani ya sura ifuatayo na zingine zifuatazo zitakusaidia kuyashinda matatizo kama hayo.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 57 10/20/2015 4:31:58 PM

# SURA YA 6

# HAJA YA MAANDALIZI

## UMUHIMU WA MAANDALIZI

Kama Benjamin Franklin alisema kwa uzuri sana, “Kwa kushindwa kujiandaa, basi unajiandaa kuanguka.”

Umuhimu wa kujitayarisha hauwezi kusisitiziwa vya kutosha. Endapo umejiandaa, hususani kabla ya mkutano, basi una muelekeo wa kuweza kutumia fursa hiyo kwa ukamilifu kabisa wa uwezekano wake na kufanya uamuzi mzuri.

### Tambua Unachokitafuta

Kabla hujaanza kutafuta nusu yako nyingine, ni muhimu kwamba unakuwa nayo aina fulani ya mawazo kuhusu ni sifa zipi unazozitafuta. Kama hujafikiria jambo hili na unajiingiza tu kwenye mkutano basi ipo hatari ya kwamba unaweza ukafanya uamuzi wa haraka haraka na usio wa busara (huenda ni kwa matokeo ya shinikizo la familia au mambo mengine) ambayo baadaye utakuja kuyajutia.

Mara unapokuwa umetambua sifa zile unazozitafuta kwenye hiyo nusu ya pili, utaona kwamba maswali unayotaka kuyauliza yatatiririka kama kawaida.

### Jitambue Wewe Mwenyewe

Kutambua ni nani unayemtafuta, hatua muhimu unayotakiwa kuchukua ni ‘kujichambua wewe mwenyewe,’ kwa sababu unahitaji kujitambua wewe ni nani ili uweze kujua ni mtu yupi unayemtafuta



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 58 10/20/2015 4:31:58 PM

ambaye ataendana na wewe. Chambua haiba yako, nguvu zako, mapungufu yako, malengo yako, vivutio vyako, kitu gani hukufurahisha, kipi hukuhuzunisha, unataka nini katika maisha na kadhalika, kwa sababu mara nyingi zaidi, utaona kwamba utaelekea kumpenda zaidi mtu ambaye ni imara katika mambo ambayo wewe una udhaifu, lakini wakati huo huo, anayo maono kama ya kwako, mapendeleo kama ya kwako, na malengo kama ya kwako.

**Wajue Wazazi Wako/Familia Yako**

Kipengele muhimu cha kuwa wewe ni nani kinathibitishwa na wale ambao wamekuwa na athari muhimu katika maisha yako, na matarajio yako katika maisha. Mara nyingi zaidi hao ni wazazi wako na kwa hiyo njia moja ya kujitambua wewe ni nani ni kuwafasiri wazazi wako, shakhsia zao, mapendeleo yao, jinsi wanavyojihusisha na dunia, wajibu wao kwa jumuiya, kazi wanazofanya, uhusiano wao na familia za karibu, jinsi wanavyopata burudani na jinsi wanavyoshughulikia hali mbali mbali katika maisha yao. Mara nyingi utaona kwamba jibu la swali 'wewe ni nani?' litakuwa la wazi zaidi kila utakavyozidi kufanya utafiti wa maisha yao.

**Chagua watu wa mfano wa kuigwa**

Kwa kawaida kile kinachosaidia kwenye hatua hii ni kuchagua 'wanandoa ambao ni mfano bora' ambao unaweza kuhusiana nao. Wanandoa ambao unawategemea katika namna vile wanavyoendesha maisha yao, maadili waliyonayo, jinsi wanavyo husiana wao kwa wao, na watoto wao na jamii kwa ujumla, mtindo wao wa maisha, mafanikio yao, wajibu wanaotekeleza kwenye jamii pana zaidi, na kadhalika.

Kuwatambua 'Wanandoa wa mfano bora' kwa kawaida ni kitendo cha kisilika ambacho wengi wetu hukifanya bila ya kukitambua.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 59 10/20/2015 4:31:58 PM

Inaweza kuwa ni wazazi wako, kaka yako, dada yako, binamu yako, rafiki yako, na kadhalika. Ni muhimu kwamba unakuwa karibu nao ili uweze kuepuka kuwakadiria katika kiwango cha juu juu tu. Ukishawatambua 'wanandoa wako wa mfano bora' lazima utenge muda fulani na uzipe muhimu zile nukta zinazowafanya wao kuwa mfano bora kwako. Ukiziandika sifa hizi itakusaidia sana katika kutayarisha muelekeo wa maisha yako ya baadaye na aina ya mtu unayemtafuta ambaye atalingana na muelekeo huo. Mathalani, inawezekana kwamba unawaangalia wanandoa hao ile jinsi wanavyoonekana kuhusiana wao kwa wao, na watoto wao, na jumuiya pana zaidi na kadhalika.

## Tambua Unachotaka Kuuliza
## Maadili na Shakhsia

Uelewa wetu juu ya viambato ambavyo huwaunganisha watu wawili pamoja ni iwapo wana maadili na malengo muhimu yanayofanana na mtazamo wa maisha unaofanana, sifa ambazo huwafanya watu wawili kuchukuana. Jambo la pili la kuleta mchukuano ni haiba shakhsia.

Endapo maadili msingi yanafanana, kuwa na haiba tofauti inawezekana isiwe tatizo. Wakati mwingine inaweza kuwa hata ndiyo sababu ya ulinganifu kwa kuwa mnaweza kukamilishana, mathalani:

- Mwenye kufikiri kwa moyo anaweza kumkamilisha mwenzake mweye kufikiri kwa kichwa.
- Mwenye hali ya maamuzi ya ghafla dhidi ya maamuzi ya uangalifu
- Mwenye hali ya utulivu dhidi ya hali ya taharuki
- Mwenye hali ya kulala dhidi ya hali ya utayari na mashughuli



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 60 10/20/2015 4:31:58 PM

- Mwenye sauti ya juu na kivutio cha nadhari dhidi ya sauti ya kimya nyuma ya mtu

Hata hivyo, haiba hizi huwa na mwelekeo wa kukamilishana zaidi pale ambapo kuna tofauti za wastani miongoni mwao na si tofauti kubwa mno.

"Nilivyoona uhusiano wa ammi na shangazi, nikajua kwamba hicho ndio nilichokitaka kwenye uhusiano wangu mwenyewe, na kwa hakika hiki kilikuwa ni jambo la kutia moyo katika kuchagua mke wangu. Walikuwa, na wapo 'pamoja' sana na wanaendana. Wanafanya kila kitu pamoja na kama hawapo pamoja unaweza kujua kwamba bora wangekuwa pamoja. Huwasiliana vizuri sana, kwa kauli na vinginevyo, na hiyo huja na wakati, kujua kinachomfanya mwenza wako kuwa safi, kwa hiyo, unajua pale watakapopokea kitu vizuri na pale ambapo hawatapokea vizuri. Hufanya maamuzi pamoja, huaminiana kwa dhahiri hupeana matumaini kila wakati (bila tofauti). Wao ni 'nguzo' ya wao kwa wao. Wote wawili wanatoka kwenye familia imara lakini wametoka kwenye njia yao kuikubali familia ya 'mwingine' kama familia yake. Familia yao wenyewe ni imara kwa sababu wanaheshimiana ndani ya familia, kiini chake kikiwa ni upendo, haki, na uimara. Nisingesema mke wangu na mimi tunakubaliana kama hivyo, lakini si lazima kwamba hili ni jambo baya; lakini vyovyote iwavyo bado tunafaana kikamilifu. Nilidhani tungeweza kufanya kazi pamoja vizuri na kukua pamoja. Hilo ni jambo jingine ambalo nimejifunza kutoka kwa wale wanandoa wangu wa mfano bora - wakati wote wanalifanyia kazi hilo. Kwa sababu ndoa ni maisha kujifunga kama hivyo, unahitaji kuendelea kujifunza na kujirekebisha." -**Mwanamume, Uingereza.**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 61 10/20/2015 4:31:58 PM

**Kuyaangalia kwa Karibu Zaidi Maadili:**[46]

Kwa kigezo cha maadili, kinachomaanishwa hapa ni kwamba ni umuhimu kiasi gani wa maeneo fulani katika maisha yenu ambayo ni kiini kwenu. Kimsingi, ni kwa kanuni zipi huwa mnaendesha maisha yenu, na ni mara nyingi huamuliwa na maadili na utamaduni ambao ulitawala malezi yenu, na pia, mazingira ambamo inawezekana mlitumia muda mrefu.

Pamoja na kwamba msingi wa ndoa ni maafikiano, mara nyingi kuna mambo ambayo 'hayazungumziki'. Maadili fulani yatakuwa karibu sana na moyo wako na utaishi nayo katika kiwango cha kuelewa na nafsi iliyofichika na haupo tayari kuzungumzia juu ya kipengele hicho, mathalani hijabu. Maadili mengine, ambapo yanaweza kuwa na umuhimu, unaweza kuyatathimini na kuamua kwamba labda ni jambo ambalo ungeweza kuafikiana juu yake, kama vile mahali mtakapoishi baada ya kuoana. Ni muhimu kwamba mnazungumzia mambo haya katika hatua hii.

Maadili yanaweza kugawanywa kwa mfano hasa katika maeneo muhimu yafuatayo:

1. Familia na Wazazi
2. Imani
3. Mtindo wa Maisha
4. Kazi na Malengo ya Kifedha
5. Majumuisho Yote.

Kwa hiyo:

46 Taarifa nyingi sana zimechukuliwa kutoka kitabu kiitwacho: *Solutions for Marriage*, Sehemu ya 3 kati ya 4 cha Shabbir na M. H. Alibhai, & Fatima Y. Alibhai & co.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 62 10/20/2015 4:31:58 PM

- Imani yako inatawala vipi maisha yako ya kila siku.
- Jumuiya yako mwenyewe ina umuhimu gani ( yaani sehemu mnapokusanyika kwa ajili ya ibada) na ile jamii pana zaidi katika maisha yako ya kila siku.
- Familia yako ya karibu ina umuhimu gani katika maisha yako ya kila siku? Huwa mnakutana mara nyingi kiasi gani? Ni upi utaratibu wenu wa msaada wa haraka? Mnachanganyikana kwa kiasi gani kwa msingi wa siku hadi siku? Ni maadili gani ya msingi yanayotawala mfumo wa familia? Yaani mngeweza kuishi kwenye familia pana kiukoo? Au hapana? Nani atakuwa na wajibu kwa wazazi wa bwana harusi na bibi harusi?
- Kazi yako ina umuhimu kiasi gani? Je inafikia kwenye lengo? Ni kitu ambacho una mapenzi nacho sana? Ni muda kiasi gani unaopenda kuutumia juu yake? Wewe umezoea maisha ya kiwango gani? Je ni maisha ambayo unatarajia kuendelea nayo baada ya kuoa?
- Kuhusu maadili ya mtindo wa maisha, familia inayo umuhimu gani katika kuupangilia muda? Mtaishi namna gani baada ya kuoana (mtaishi wote pamoja kwenye familia pana kiukoo au mtaishi peke yenu)? Mahitaji ya mlo yana umuhimu kiasi gani (yaani kama mtu fulani atakuwa amejilazimisha mwenyewe kula mboga mboga tu)?

Haya sasa yataangaliwa kwa undani zaidi. Inawezekana kwamba mwanzoni wanandoa watadhani wanakubaliana juu ya masuala haya, au kama zipo tofauti, kwamba tofauti hizi ni ndogo na si za muhimu, au kwamba wataweza kubadili upande mwingine juu ya maoni yao kuhusu masuala haya, lakini ambayo baadaye yanarudi

kuwasumbua. Endapo baadhi ya masuala ambayo yameelezewa kwa muhtasari yanaweza kuwa muhimu kwako na yameelezewa katika hatua za mwanzoni, itaepusha usumbufu mwingi sana moyoni.

**ANGALIZO:** Masuala yafuatayo chini yanaweza yasijumuishe masuala yote unayohitaji kuyafikiria unapochagua mchumba na inawezekana yawepo mengine ambayo ni muhimu kwako na hayakujumuishwa chini.

## 1. Familia na Wazazi

Ipo haja ya kujadili juu ya wajibu ambao wazazi na familia wanauchukua katika maisha yenu; watu wa familia ya mwenza wako ndio watakaokuwa sehemu kubwa ya maisha yenu, ambao mtakuwa mnawasiliana nao sana na kuchanganyika nao, au hapana? Ni watu ambao maingizo yao na msaada wao, na pia kuwa pamoja nao na upendo wao vinakubalika? Je, hii inaafikiana na maadili yako na malezi yako, au ungependa iwe namna gani mnamo siku za usoni?

Suala lingine lenye kuhusiana na mjadala ni namna gani familia inafanya kazi, na mwenendo wa familia ukoje, miongoni mwao wenyewe, na familia pana kiukoo, na marafiki. Baadhi ya watu wanaweza kuwa karibu sana na familia ya kiukoo, na kukutana mara kwa mara, kwa mfano, jambo ambalo litaweza kukufaa au laa.

## 2. Imani

### a) Uzingatiaji wa Sheria za Dini

Ipo haja ya nyinyi wawili kujadili ni kwa kiwango gani kila mmoja wenu anazingatia mafundisho ya Uislamu na/au angependa kuyazingatia mnamo siku za usoni, kwa mfano:

- Umuhimu unaotolewa wa kutekeleza mambo ya wajibu.

* Umuhimu unaotolewa wa kutekeleza vitendo vya sunna (yaani vitendo ambavyo vimependekezwa kutekelezwa, lakini si wajibu) na kutokutekeleza vilivyo makruhu (yaani vitendo ambavyo vimependekezwa kutotekelezwa, lakini havikuharamishwa kama ukitekeleza).

*Haja ya kuhudhuria msikitini na ni mara ngapi (yaani kila siku, kila wiki, kila mwezi)

* Wajibu ambao kila mmoja wenu angependa kuubeba hapo msikitini, madrasa na maeneo mengine ya kidini.

* Maoni ya kila mmoja wenu juu ya masuala kama vile kusikiliza muziki, kula chakula sehemu ambazo vilevi vinauzwa au wapishi si Waislamu, na kadhalika.

> "Nilipoposwa kwa mara ya kwanza, nilianza kutambua katika kipindi cha miezi mitatu ya kwanza kwamba mposaji na mimi tulikuwa hatuna lengo la kuelekea upande moja kidini. Namna ambayo niliweza kulitambua hili ni kupitia na mazungumzo yetu, tuliweka kadiri tofauti za umuhimu juu ya masuala mbali mbali ya kidini, mfano ukiwa, ni sehemu zilizo sahihi kwenda kula chakula na kwa nini. Vilevile, nilikuwa na maoni tofauti na yake, kuhusu jinsi gani nilitaka kufuatilia masomo yangu ya kidini, na ingawaje mwanzoni nilihisi mipango yake ilifanana na ya kwangu, baadaye niligundua kwamba ilikuwa tofauti kabisa. Kwa hiyo, tulikuwa ni watu wawili tofauti kabisa, waliokuwa wanaelekea pande mbili tofauti kabisa." **Mwanamke, Uingereza.**

Mchukuano na maafikiano huhakikishwa kwa urahisi zaidi endapo nyinyi wote wawili mna kiwango kinacholingana cha imani



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 65 10/20/2015 4:31:58 PM

na kaida za kidini. Hata hivyo, ni muhimu kwamba hamna matarajio ya kuzidi kiasi, kwa sababu kama mna kiwango kinacholingana cha imani na mapenzi ya kidini, lakini mna kiwango tofauti cha utekelezaji (mfano kama mmoja wenu tayari anatekeleza jambo ambalo mwingine hatajali kutekeleza au angependa kulitekeleza), basi kila mara upo uwezekano kwamba mtakua pamoja. Hakika hii ni mojawapo ya zawadi za ndoa - kusaidiana kila mmoja wenu katika kuelekea kwenye imani, malengo na matamanio yenu mema.

## b) Hijabu

Hijabu ni suala muhimu kwa wanandoa wengi (pamoja na ukweli kwamba hijabu ina vipengele vingi, kwa kusudio la sehemu hii, inazungumzia kufunika mwili na nywele tu, yaani hijabu ya mwili). Kama mchumba tayari inazingatia hijabu, unaweza tu ukataka kuthibitisha kwamba ataendelea kuvaa baada ya kuoana. Endapo kwa sasa havai hijabu, hali hii ina umuhimu gani kwa wenza na/ au wazazi wao kwamba kwa sasa havai hijabu? Mume kwa ghafla atataka mke avae hijabu mara tu baada ya kuoana, au kinyume chake, avue hijabu baada ya kuoana?

Kwa maoni ya mume, kuvaa ushanga pia ni jambo linalotakiwa kuzungumzwa. Kama kwa sasa mume anafuga ndevu, je ataendelea kufanya hivyo baada ya ndoa? Je, mke atataka mume afuge ndevu mara baada ya ndoa au anyoe? Je, kuna suala la kuwa na ndevu kidevu chote au nusu kidevu?

## c) Jumuiya

Huyu mwenza mtarajiwa wako ni mwanachama wa jumuiya? Je ana wajibu wa namna yoyote ndani ya jumuiya hiyo au ana tamaa ya kufanya hivyo? Je, matukio ya jumuiya ni muhimu kwa maisha yenu?

## 3. Mtindo wa Maisha

### a) Mahali pa Kuishi

Mara wanapooana kwa kawaida wanandoa wanazo chaguzi mbili tu. Ama wanaweza kuamua kuishi na wazazi wao au na familia yao (kwa kawaida ni mume ndiye anayeishi na wazazi wake, na mke anakuwa mgeni ndani ya kaya yake), au wanaweza kuamua kuishi tofauti wao peke yao. Chaguzi zote zina manufaa yake na hasara zake. Umuhimu wa kuzungumzia suala hili kwenye hatua za mwanzo hauwezi kusisitiziwa vya kutosha. Pande zote mbili zinatakiwa kuweka mambo yote wazi na wajaribu na kuonyesha hisia zao zijulikane na kila mmoja wao.

Endapo mtachagua kuishi pamoja, ni muhimu kwamba sifa zote za msingi za familia yaani maadili, kanuni na utamaduni zinaelezewa mchumba na kwamba mume anadhihirisha wazi matarajio yake kwa mwenza wake mtarajiwa (kwa mfano, maisha ya familia na wajibu ambao kila mmoja wenu atauchukua ndani ya familia hiyo). Endapo mtachagua kuishi peke yenu, bado ni muhimu kwa mume kuelezea utamaduni wa familia kwa upana na matarajio yake ya maisha wakiwa pamoja wenyewe, na familia ya kiukoo itafanya nini ndani ya maisha yenu (kama kuna chochote).

Endapo wenza wote wawili watakuwa hawaishi ndani ya mji moja, ni muhimu kuamua ni yupi miongoni mwenu ambaye atahama kumfuata mwenzake. Jambo hili ni muhimu zaidi endapo umbali halisi wa kuhama ni mkubwa. Ni desturi kwamba kwa kawaida ni mke ndiye anayehama kumfuata mume, lakini siku hizi, kwa watu wengi kufuatilia elimu ya juu zaidi na mikondo maalum ya kazi, si rahisi kutekeleza desturi hii kila mara. Mtu ambaye amesomea kazi fulani na kufika ngazi ya ubingwa inawezekana akatakiwa kupitia



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 67 10/20/2015 4:31:59 PM

mitihani ya kufuzu ya kuchukua muda mrefu ili aweze kupata sifa ya kufanya kazi kwenye nchi nyingine, wakati mwingine bila uhakika wa kupewa cheti kingine cha uthibitisho na kutafuta kazi kwenye nchi nyingine. Je, upo tayari na unakubali kutoa muhanga huu wa kisaikolojia na/au wa kiuchumi?

### b) Watoto

Mngependa kupata watoto? Endapo jibu ni ndiyo, wangapi? Ingawaje idadi ya watoto inayotakiwa kwa hakika inaweza kubadilika baada ya kuoana kwa sababu mbali mbali, inatakiwa pawepo na makubaliano ya pamoja kwamba nia ya kupata watoto kwa hakika ipo ama haipo. Kupanga muda wa kupata watoto pia ni kitu ambacho lazima mkizungumzie. Je mtataka kupata watoto mara tu baada ya kuoana au mtangoja kwa kipindi fulani? Mtapenda kuwaleaje watoto wenu?

### c) Afya na Lishe

Kwa baadhi ya wanandoa, kwao hili sio tatizo. Kwa wengine hili linaleta changamoto kubwa na linaweza hata kuvunja ndoa. Masuala kama ya mtu fulani kujilazimisha kula mboga mboga tu, na kadhalika, na mambo madogo ya afya kama historia ya kisukari katika familia au shinikizo la damu ni mara chache sana kuwa na umuhimu. Hata hivyo, historia binafsi ya magonjwa makubwa ya kimwili, ulemavu, au ugonjwa wa akili (yaani *schizophrenia* - kuchanganyikiwa, *depression* - msongo wa mawazo) yanaweza kuwa na athari kubwa kwenye ndoa. Endapo inakuwa vigumu kuzungumzia mada kama hiyo wewe binafsi, inaweza kuwa na manufaa kupata taarifa kutoka kwenye vyanzo vingine. Suala kubwa ambalo limesababisha kuvunjika kwa ndoa kadhaa linahusiana na mmojawapo wa wanandoa kutumia vilevi (pombe), pamoja na kudai kwamba yeye ni Mwislamu.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 68 10/20/2015 4:31:59 PM

Mfano mdogo sana, lakini ni muhimu kwa wengi, ni iwapo kama mtu huyo huvuta sigara. Kweye baadhi ya jumuiya, tishio jipya (ambalo ni la kweli) ni maambukizi ya virusi vya ukimwi. Ingawa mambo haya ni magumu kuyauliza, kwa hakika ni vema kujua kabla ya kuoana badala ya baada ya kuoana.

## 4. Malengo ya Kazi na Uchumi

Yupi kati yenu atatafuta kazi? Yupi kati yenu atakuwa mwangalizi wa nyumba? Je, wote wawili mtatafuta kazi? Kama jibu ni ndiyo, nani atawajibika kwa watoto na uendeshaji wa nyumba? Utafutaji wa kazi utaathiri vipi maisha ya familia? Zipo ndoa kadhaa ambazo hazikufanikiwa juu ya suala hili, kwa hiyo ni muhimu kwamba suala hili linazungumziwa katika hatua hii, kwa sababu walioolewa mara nyingi huweza kutarajiwa kuajiriwa kwa kazi za kudumu na pia kusimamia nyumba. Mzigo huu wa nyongeza wa ‘kazi ya siku mbili kwa moja’ kwa kawaida ndiyo kichocheo cha kutokeza kwa matatizo.

Je, ni mmojawenu au wote wawili mtakuwa huru kutafuta elimu baada ya kuoana? Je, familia ni yenye kusaidia, hususani katika suala la mke anayetaka kutafuta elimu ya juu? Kuna athari zozote za kiuchumi kwa kuwa na mmoja wenu tu kutafuta kipato, ambapo mwingine anasoma?

## 5. Kwa Ujumla

Ni yapi matarajio yenu kwa ujumla kutoka kwa kila mmoja wenu? Mnayo maoni ya namna moja kuhusu maisha ya ndoa na maisha kwa ujumla? Nini malengo yenu, matumaini yenu na vipaumbele vyenu katika maisha? Je, yanafanana na ni jambo ambalo wote wawili kwa pamoja mnaweza kuelekea kuyafanyia kazi?



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 69 10/20/2015 4:31:59 PM

## Kuhakiki Maadili na Haiba

Maadili na matakwa ya mwenza wako mtarajiwa ni mambo ambayo yanaweza kuchunguzwa wakati wa mikutano, kwenye barua-pepe, na simu, kupitia mazungumzo ya kawaida na maswali kama yalivyoorodheshwa hapo chini. Hata hivyo, haiba ni kitu kinachotambulika wakati wa kuchanganyikana na 'kuwa' pamoja na mtu huyo, kwa sababu ni kwa jinsi mtu anavyoishi na maadili yake, na jinsi yanavyoingiliana na dunia inayomzunguka na mazingira yake.

"Mimi kama mwanamke ilikuwa muhimu kutambua maoni ya mwenza wangu mtarajiwa juu ya uaminifu na vurugu za nyumbani. Haya ni masuala na mada zenye mguso ambazo mara nyingi tunahofia kuwa zinaweza kumtishia mtu mwingine. Pia haina maana na hovyo (na pia inawezekana kabisa kuwa ni ufidhuli) kumuuliza mtu ambaye bado kwa namna fulani ni mgeni kwako kama angempiga mkewe au kutokuwa mwaminifu kwa mkewe katika ndoa. Kwa hiyo ili kuweza kugundua alikuwa anafikiria nini kuhusu masuala hayo mawili, nilimuuliza maswali ya mtego kama 'ungefanya nini kama ungegundua kwamba rafiki yako mzuri sana sio mwaminifu kwa mkewe" na 'ungejisikiaje kama ungemuona mtu anamtukana mwenzake wa muhimu mbele yako?' Haya yalikuwa maswali magumu kuyajibu, hususani ikitiliwa maanani baadhi ya desturi za kijamii za faragha na uingiliaji, lakini lengo langu halikuwa kumsaili yeye na kujua tabia yake kwa msingi wa jibu sahihi au lisilo sahihi. Nilitaka kuelewa jinsi ambavyo angeyachukulia matukio haya na mlolongo wa fikira zake katika kujibu maswali haya." - **Mwanamke, Afrika**.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 70 10/20/2015 4:31:59 PM

## Kuwa na Mazungumzo, Si Usaili

Mnapokutana kwa mara ya kwanza, jambo la muhimu kukumbuka ni kuweka mambo katika hali ya kawaida kadiri iwezekanavyo na kujaribu tu kuwa na mazungumzo ya kawaida, kinyume na 'mazungumzo' mazito kwa kuingia moja kwa moja kwenye maswali yenye shutuma. Vunja kimya kwa mazungumzo madogo (kuhusu hali ya hewa, hali ya barabarani na nini ulifanya wakati wa mwisho wa wiki mara nyingi huwa ndio mazuri), na halafu uone mazungumzo yataelekea wapi kutokea hapo.

Mara nyingi, anapojitambua kuwa ni nani na akawa na aina fulani ya mwelekeo na lengo (yaani mtu anapojitambua mwenyewe), mazungumzo yatakuwa na uelekeo na kutiririka ilivyo kawaida kwenye maeneo ambayo ni muhimu kwao bila kuhisi kwamba ni 'usaili.'

## Muda wa Maswali

Pamoja na kupata taarifa kupitia mazungumzo yenu, unaweza pia kutumuia maswali fulani kama nyenzo ya kuchunguza zaidi maadili. Mara nyingi, kuzungumzia habari zako mwenyewe kwanza ni njia ya kawaida kuyaingiza haya, kwani mara nyingi zaidi, kitu unachokisema kinaweza kuvuma na kujirudia pamoja nayo na kuweka wazi baadhi ya mambo yanayofanana, na maswali yatatiririka yenyewe kwa wepesi zaidi. Kwa mfano, "Kwa kweli mimi hufurahia sana kusafiri, mwaka jana nilikwenda Mombasa na nilikuwa na muda mzuri sana wa kufurahia…" "Ninayo familia Mombasa, kitu gani kilikufurasha sana huko Mombasa? Wapi pengine umewahi kwenda wakati wa mapumziko?" na kadhalika….

Maswali yanaweza kuulizwa katika njia mbili. Unaweza kutaka kuuliza maswali ya moja kwa moja kama: Ulikuwa wapi wakati wa



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 71 10/20/2015 4:31:59 PM

mapumziko? Au unaweza kutaka kuyauliza kwa namna ya kutatiza na ya mzunguko zaidi, ambayo italazimisha upande mwingine kufikiri zaidi kabla ya kujibu. Baadhi ya mifano ya aina zote mbili za maswali imetolewa hapo chini:

**Mifano ya Maswali ya Moja Kwa Moja:**

**1.** Wewe unautumiaje muda wako wa jioni wa siku za wiki?

**2.** Unautumiaje wakati wako wa mwisho wa wiki?

**3.** Wewe huwa unafanyaje unapopumzika na kujiburudisha?

**4.** Kwa kawaida huwa unakwenda wapi wakati wa likizo?

**5.** Unatumiaje/ulitumiaje muda wako huko chuo kikuu?

**6.** Ungebadilisha nini endapo Mwenyezi Mungu angerudisha wakati nyuma hadi hapo ulipokuwa na umri wa miaka 18?

**7.** Kitu gani ulikiona ndio kigumu sana katika kukua?

**8.** Ni kazi gani umeiona ni ngumu sana kuitimiza hadi sasa?

**9.** Sehemu zipi ungependa kuzulu wakati wa likizo na kwa nini?

**10.** Michezo/shughuli gani unazofanya na kwa nini?

**11.** Unawajibikaje kwenye jumuiya yako?

**12.** Ni wajibu gani unajiona unautekeleza mnamo siku zijazo ndani ya jumuiya yako?

**13.** Unawajibikaje nyumbani kwako?

**14.** Wewe umawajibika vipi ndani ya jumuiya pana zaidi?

**15.** Kazi yako ina umuhimu gani kwako?

"Lengo langu la kumsaili mwanamume ambaye angekuwa mwenza wangu wa maisha, ilikuwa sio tu kujua alikuwa ni mtu wa namna gani, lakini pia jinsi alivyofikiri, alikuwa na mtazamo gani juu ya maisha na juu ya masuala mbali mbali yahusuyo maisha, na jinsi alivyofanya maamuzi. Kama nilikuwa nimwamini mtu huyu kwa sehemu kubwa ya busara na furaha ya maisha yangu yote, ilikuwa nijue kwamba alikuwa ni mtu ambaye ningeweza kumwamini, kumheshimu na kufurahi kuwa naye. Kama ilivyo kwa barua pepe yoyote ya kwanza isiyo na uangalifu, maswali yetu yalianza na mambo ya msingi – taarifa za mambo ya kimaisha. Hata hivyo, pole pole tulianza kuulizana maswali yaliyochimba ndani zaidi kwenye maadili, vipaumbele na malengo ya maisha - maswali kama "Wito au falsafa gani juu ya maisha ungependa kuishi nayo?" na "Nini lengo/malengo yako ya juu katika maisha?" Kila jibu lilikuwa ni dirisha kwenye dunia yake na fursa ya kuelewa vizuri zaidi vipaumbele vyake na maadili yake." **Mwanamke, Afrika**

**16.** Ungeorodhesha vipi kulingana na kuyapa kipaumbele haya yafuatayo:

- Michezo na Mazoezi
- Kazi
- Familia
- Marafiki
- Jumuiya
- Elimu



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 73 10/20/2015 4:31:59 PM

- Kuchukua nafasi ya kazi ndani ya jumuiya
- Jumuiya iliyo pana zaidi
- Kusoma kwa ziada nje ya masomo ya shule
- Kusafiri na kuthubutu kwenye sehemu usizozijua
- Dini

**Mifano ya maswali ya mzunguko:**

1. Kama ungepewa fursa ya kula chakula cha jioni na watu watatu mashuhuri ambao wametembea sana hapa duniani wangekuwa ni nani hao na kwa nini?
2. Endapo ningemuuliza rafiki yako mzuri sana kuelezea tabia yako, ni vitu gani vitano ambavyo angevisema?
3. Endapo ningemuuliza rafiki yako mzuri sana kuhusu nguvu zako tatu kuu za uimara wako, angetaja nguvu zipi?
4. Kama ningemuuliza rafiki yako mzuri juu ya mapungufu yako makuu matatu, angesema nini?
5. Nani mwenye kauli/uamuzi wa mwisho miongoni mwa marafiki zako?
6. Ni mambo yapi yanayowaunganisha katika urafiki wenu?
7. Ni athari gani marafiki zako wamesababisha katika mwenendo wako? Itikadi za Kislamu? Chaguo la kazi? Tabia? Na kadhalika?
8. Ni sifa zipi unazozipenda kuhusu marafiki zako?
9. Punde tu umeona kwamba vazi la hijabu limepigwa marufuku kazini kwako/chuo kikuu unaposoma/ungeipokeaje taarifa hiyo?



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 74 10/20/2015 4:31:59 PM

"Nilipokuwa ninamuuliza maswali mume wangu mtarajiwa, ambapo maswali mengine yalikuwa ya moja kwa moja na zaidi ya aina ya 'kutaka-kukujua', na mengine yalikuwa zaidi ya aina ya 'kutaka-kujua-unavyofikiri' ambayo yalikuwa ndiyo kianzilisho cha mazungumzo. Hapa ndipo nilipopata kumjua hasa-kupitia mazungumzo hayo na uchangiaji wa mawazo nyuma na mbele ambayo yalikua kutokana na maswali mepesi. Wote wawili tulitumia idadi kadhaa ya maswali mafupi na pia (yaani ungefanya nini kama…..au, kama unge….) ambayo yalituruhusu sisi kugundua zaidi kuhusu maadili ya kila mmoja wetu na vipaumbele bila kuuliza maswali ya moja kwa moja au kuchosha. Mojawapo ya maswali muhimu sana ambalo nilimuuliza ni (na niliuliza swali hili katika njia kadhaa!) ilikuwa ni kitu gani alichokuwa anakitafuta kwa mchumba na alikuwa na fikira gani kuhusu maisha ya ndoa (aina ya mambo aliyofikiria kuyafanya katika maisha yake ya kifamilia). Maswali yenye mwisho wa wazi kama haya yaliniwezesha kuelewa matumaini na matarajio yake katika mahusiano na pia maono yake kwa siku za usoni kupitia maneno yake mwenyewe.

Mazungumzo yetu wakati wote hayakuwa mazito sana hata hivyo! Tulikuwa na sehemu yetu ya maswali na mazungumzo ya kufurahisha pia, na tulifanya ni jambo la kawaida kuchanganya maswali mazito na yale ya kufurahisha ili kupunguza hali ya hofu na kuwa na burudani zaidi wakati wa kuyajibu. Nadhani ni muhimu zaidi kuwa na mazungumzo haya mepesi pia kwa sababu ni hapa ndipo ambapo utajua kama unafurahia au hapana kuwa pamoja na mtu huyu na unaweza kujiona wewe ukiishi naye katika mambo mazito na kawaida. Kwa kweli, lengo la yote haya lilikuwa ni kujua kama huyu ni yule mwanamume ambaye nilitaka kuchukua safari ya maisha pamoja naye, ambayo kimsingi ndio safari ya kujikurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu." - **Mwanamke, Afrika.**

**10.** Punde tu umepata taarifa kwamba ndevu na nywele zote za usoni zimepigwa marafuku kazini kwako, ungeipokeaje taarifa hiyo?



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 75 10/20/2015 4:31:59 PM

**11.** Ndio kwanza tu umemsikia mtu anakusengenya kwa jambo ambalo ni la kweli, ungelichukuliaje hilo? Kuwa ni jambo ambalo si la kweli?

**12.** Hivi karibuni tu umepata taarifa kwamba ninatakiwa kwenda nchi za nje kwa uhamisho wa kikazi wa miaka miwili, ungekuwa na maoni gani?

**13.** Umealikwa na mfanyakazi mwenzako kwenda kwenye hotel/ mgahawa/baa bora kabisa kwenda kusherehekea mafanikio ya timu, ungefanya nini?

**14.** Endapo miongoni mwa marafiki zako wa familia, unalo jambo la msingi na unajua bila shaka kwamba wewe upo sahihi, lakini hakuna mtu mwingine yeyote yuko tayari kukubali jambo hili, ungefanya nini?

Unaweza pia kupenda kuheshimu maoni yako kuhusu masuala mengine yanayofaa ambayo yanaweza kuwa ya muhimu kwako, kwa mfano kitu chochote ndani ya habari za dunia, au jambo ambalo linaendelea ndani ya jumuiya, na kadhalika.

## MAMBO YA KUZINGATIA

### Kuzungumza Kuhusu Yaliyopita

Katika kipindi cha mchakato huu ambapo wachumba wapo katika kujuana, suala moja ambalo hujitokeza ni yaliyopita. Yapo maswali mawili yanayohusiana hapa:

**1.** Ni mambo gani yanayotakiwa kudhihirishwa kuhusiana na yaliyopita?



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 76 10/20/2015 4:31:59 PM

Imekatazwa kwa wachumba watarajiwa kufichua dhambi za mmoja kwa mwingine. Imam Ridhaa (a.s.) amesema: Mtu anayefichua maovu yake hadharani Mwenyezi Mungu humtelekeza. "Na mtu anayeficha maovu yake (akiyaonea aibu) husamehewa na Mwenyezi Mungu."[47]

Watu wengi hufanya makosa, na wanapoangalia nyuma huwa wanahuzunika sana na humgeukia Mwenyezi Mungu na kuomba toba. Endapo mtu ana uhakika kwamba kwa makosa yoyote ambayo atakuwa ameyafanya, na ameomba toba kwa makosa hayo na anaona huzuni ya kweli kweli na hakuna tena athari za siku za usoni kuhusu kosa hili, basi haitafaa kudhihirisha taarifa hii kwa mtu mwingine.

**2.** Kiasi gani cha kuweza kukubaliwa kuhusu yaliyopita ya huyo mtu mwingine?

Endapo taarifa fulani kuhusu mambo yaliyopita ya mtu inajulikana na inalichanganya suala hilo, basi ni muhimu kukumbuka kwamba historia ni muhimu, lakini suala la muhimu zaidi ni hali ya sasa. Mathalani, kama mtu amepotoka katika siku zilizopita, lakini tangu siku nyingi ameacha baadhi ya vitu alivyokuwa anafanya lakini hajutii makosa haya au hajatubu, basi hali ya mustakabali wake haiwezi kuwa na matumaini sana. Zaidi ya hayo, watoto wa mtu kama huyo wanaweza kuathirika vibaya.

Hata hivyo, ikiwa kama ambavyo imetamkwa hapo juu, mtu ametubu kwa dhati, hivyo kwamba ameamua kamwe kutojiingiza tena kwenye shughuli hizo, na ameibuka na sifa bainifu nzuri za kiroho, basi itakuwa ni makosa kumwacha mtu kama huyo. Kwa kweli, Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur`ani kwamba 'Huihuisha ardhi baada ya kufa kwake,'[48] dokezo la mabadiliko ya moyo kutoka kwenye hali ya dhambi na kutotii kwenda kwenye

[47] *Thawab al-A`mal*, uk. 213, namba. 1

[48] Surat al-Baqaral, Aya 164 (2:164)



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 77 10/20/2015 4:31:59 PM

hali ya ibada na utiifu. Kama mtu 'amehuishwa' na sasa anaishi maisha mazuri na anajitahidi kuwa bora zaidi na kujiendeleza, basi mambo ya nyuma isiathiri mambo ya siku zijazo, hata kama yalihusisha uhusiano wa kinyume cha sheria, madawa ya kulevya, kunywa vilevi, na kadhalika. Kwa kweli, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Yule anayetubu dhambi zake ni sawa na yule ambaye hana dhambi."[49]

Wapo wengi wanao thubutu kuvuka mipaka ya Kislamu wakati wapo kwenye umri wa ujana na wanapokuwa kwenye umri wa mwanzo wa utu uzima, lakini kadiri wanavyozidi kukomaa wanakuja kutambua na kujaribu kubadilika, na hili halipaswi kupuuzwa. Kwa kweli, wanaweza kuwepo watu kama hao ambao baadaye huwa watu wazuri kiakili na kidini, kuliko wale ambao, pamoja na kwamba hawajafanya dhambi yoyote ya wazi, wamejaa uovu, kama vile ujinga, kusengenya, wivu, kujikweza, majivuno, uvivu na kadhalika. Watu wengi hawazichukulii tabia hizi hasi kwa uzito, lakini zinaweza kuharibu maisha ya mtu.

Unapozungumza na mtu mwingine, ufumbuzi ni kwamba mara zote angalia uwezekano wa hali yake wa siku za usoni na iwapo kama wewe, kama mwenza wako wa siku za usoni, unaweza kumsaidia kufanikisha matarajio yake au la. Hakuna mfano mzuri kwa hili kama mazungumzo baina ya Imam Husayn (a.s) na Hurr, ambapo Imam hakumhukumu Hurr kwa kutegemea historia yake, lakini badala yake aliiona hali yake ya kweli ilikuwa vipi na kwamba Hurr alikwishatubu kwa uaminifu hasa.

## Usitie Chumvi Kwenye Ukweli

Wachumba wanapokutana kwa mara ya kwanza, neva huchukua nafasi kubwa ambapo wakati mwingine zinaweza kusababisha wewe

[49] *Kanz al-Ummal*, Hadith na: 10174



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 78 10/20/2015 4:31:59 PM

kutia chumvi kwenye ukweli kwa lengo la kutaka kuonyesha taswira ya mwanzoni nzuri. Haiwezekani kutilia mkazo wa kutosha kwamba kutia chumvi kwenye ukweli au kupindisha ukweli mara kwa mara huwa hatua ya muda mfupi, na mwishoni utajikuta unajiumiza mwenyewe, hiyo nusu nyingine na wote wale wanaokuzunguka. Kwa hiyo ni muhimu kwamba kabla ya kujibu maswali yoyote, weka kituo kwa muda ili ufikiri, na halafu utoe majibu yanayoendana na kile kilichoko moyoni mwako. Inshallah mwombe Mwenyezi Mungu akuongoze kabla humjaanza mazungumzo: Omba msaada wa Mwenyezi Mungu dhidi ya Shetani na muanze kwa jina Lake.

## Taarifa ambazo lazima Zidhihirishwe

Endapo, baada ya kusoma tamko la ndoa, mume au mke anaona taarifa fulani kuhusu mke/mume wake anayo haki ya kubatilisha ndoa, ingawa inawezekana wasifanye hivyo. Kwa hiyo ni muhimu kudhihirisha taarifa hii katika hatua za mwanzo, ili kujikinga na matatizo yanayoweza kujitokeza baadaye.

## Kuhusu Mke [50]

Endapo mume atagundua lolote miongoni mwa mambo sita yafuatayo, anayo haki ya kubatilisha ndoa:

a. Wenda wazimu, hata kama ni wa vipindi

b. Ukoma

c. Hali ya kuwa na mabaka kwenye ngozi

d. Upofu wa macho

[50] Sheria za Kiislamu, Kufutana na Fatwa ya Ayatullah al-Uzma Sayyid Ali al-Husaini as-Sistani, World Federation, 1994, Kanuni ya 2389

e. Ulemavu, hata kama ukiwa sio kwa kiwango cha kushindwa kutembea

f. Kuwepo kwa nyama au mfupa kwenye njia ya uzazi ya mwanamke, ambao unaweza ua kutoweza kuzuia tendo la ndoa au mimba.

**Kuhusu Mume**

Endapo mke atagundua lolote miongoni mwa mambo yafuatayo, anayo haki ya kuvunja ndoa:

a. Kama mume anaugua ugonjwa unaomfanya yeye ashindwe kutekeleza tendo la ndoa, hata kama ugonjwa huo uliambukizwa baada ya ndoa, au kabla au baada ya tendo la ndoa.

Kwa taarifa ya kina zaidi, tafadhali rejelea kwenye rejea kama ilivyoandikwa kwenye tanbihi.

# SURA YA 7

## BAADA YA MKUTANO WA KWANZA

### KITU GANI KINACHOTOKEA BAADAYE

Mara nyingi watu huwa na kawaida ya kufanya uamuzi wa haraka baada ya mkutano wa kwanza wa iwapo kama wanataka kuendeleza mambo mbele zaidi au hapana. Mara nyingi hili hutokea kwa kuegemea muonekano wa taswira ya kwanza. Hata hivyo, muonekano wa kwanza si kila mara huwa muonekano sahihi kwa sababu ya mambo mengine ambayo huja kujitokeza katika siku hiyo halisi hasa, kama vile: wasiwasi, siku ambayo unajisikia vibaya, kukosa kujitayarisha vizuri, kuchelewa kuanza, na kadhalika.

Kwa bahati mbaya pia Hollywood na Bollywood huchukua nafasi kubwa katika kutengeneza picha bandia na matarajio yasiyo ya kweli ya jinsi uchumba wetu, ndoa zetu, na mapenzi yanavyopaswa kuwa; sana haina muelekeo wa kuleta mtikisiko wa roho na mapenzi kwa kuonana kwa mara ya kwanza. Unapaswa ujikumbushe mwenyewe kwamba haiwezekani kumpata mchumba atakayekidhi matarajio yako na vigezo vyako vyote, lakini Inshallah, Mwenyezi Mungu atakuongoza kwenye uwezekano wa karibu. Isipokuwa kama una uhakika na bila shaka kabisa kuhusu kutokuendelea mbele na mambo, mnapaswa mkutane angalau mara moja tena na halafu myachukue mambo kuanzia hapo, kwa sababu mkutano wa kwanza mara nyingi huwa ni kivunja ukimya na wakati wote mtu anahitaji muda wa kufikiri kuhusu nini kilichosemwa kwenye mkutano wa kwanza.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 81 10/20/2015 4:31:59 PM

Endapo nyote wawili bado mnavutiwa kuyapeleka mambo mbele, mnaweza kukutana mara chache tena na muwe mnawasiliana kupitia njia zingine kama vile simu au intaneti, ili kuwapeni wote wawili fursa ya kufahamiana zaidi kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho. Ni muhimu kukumbuka kwamba katika hatua hii kanuni za kuchanganyikana na mtu wa jinsia tofauti lazima zifuatwe kabisa kama ilivyotajwa ndani ya Sura ya 4.

> Nilipokutana na mume wangu kwa mara ya kwanza, ilichukua mikutano mitano kwa mimi kushawishika kwamba yeye alikuwa ndiye mtu sahihi kwa ajili yangu. Halafu baada ya kuamua kwamba tulitaka kuoana, nilikuwa na kazi ya kumweleza kwamba mimi nilikuwa na mabaka kwenye ngozi kama Risalah ilivyosema kwamba hii ilikuwa mojawapo ya hali ambayo ingeweza kutangua *Nikah*. Kwa hiyo nilimuita ili tuzungumze kwa mara nyingine zaidi na nilikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi ambavyo mambo yangeisha, lakini Alhamdulillah, mambo yalikuwa mazuri kwa sababu alisema kwamba baada ya mikutano yote ambayo tulikwishafanya, alikuwa ananioa mimi kama nilivyo mimi, si kwa sababu ya muonekano wangu tu. Bado nilimuomba aangalie (niliondoa krimu niliyokuwa ninaipaka ili kuyafunika) na hakuwa na matatizo nayo." - **Mwanamke, Uingereza**

Kipindi hiki cha kufahamiana kwa kawaida hudumu kwa wiki chache; hali hii hukupa muda kabla ya kuhisi unataka kufanya uamuzi. Hata hivyo, inawezekana yapo mengi tu ambayo mnaweza kuambizana kabla hamjaingia kwenye uwanja wa 'haramu' (tabia zinazokatazwa) kama ilivyo fafanuliwa na Sheria ya Kislamu. Pande zote mbili za wazazi pia zinaweza kuanza kukosa furaha kama kipindi hiki kitarefushwa kwa sababu hiyo.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 82 10/20/2015 4:31:59 PM

Ni baada ya kipindi hiki ndipo huelekea kwenye ‘wakati wa kukata shauri’, ambapo unatakiwa kufanya uamuzi juu ya ama unadhani mtu huyo ndiye aliye sawa kwa ajili yako au hapana.

**Shinikizo la Nje**

Kwa bahati mbaya, inaelekea kuwepo na shinikizo kubwa kutoka nje katika mchakato wa kuchagua mchumba, ingawa kutoka kwa watu wenye nia njema na waaminifu, ama ni wazazi, washenga, au hata upande mwingine. Shinikizo hili linaweza kuanza kutoka baada ya mkutano hata mmoja tu, na linaweza kuja kwa namna ya maoni yafuatayo:

“Kwa nini mnachukua muda mrefu sana kufanya uamuzi?”

“Kwa nini unataka kumuona tena? Tayari mmekwishakutana kwa muda mrefu sana!”

“Utanivunja moyo wangu kama ukisema hapana…”

“Utabaki bila mke/mume daima milele…”

“Wewe sema tu ndiyo, matokeo yatafuata…”

“Ana matatizo gani mpaka unasema hapana?”

“Baada ya kupokea posa ya mume wangu mtarajiwa na tukafanya mkutano wetu wa kwanza nilichanganyikiwa kabisa…ilikuwa ni ‘ndiyo’ lakini nyuma ya ubongo wangu nilikuwa na ‘hapana’ ya wasiwasi pia na hiyo haikusaidia sana katika hali hiyo. Hata hivyo, sikutaka kukata tamaa na kuipa jaribio jingine hadi nilipofika kwenye jibu halisi. Kwa kweli, ilikuwa ni ile mikutano michache mingine zaidi tuliyofanya ndiyo iliyonifanya mimi niamue kwa uhakika na Alhamdulillah, sasa hivi ni wanandoa wenye furaha.” **- Mwanamke, Irani**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 83 10/20/2015 4:31:59 PM

Hususani kufuatana na kauli hii ya mwisho, ni muhimu kuzingatia kwamba si lazima kwamba mtu anahitaji kuwa na dosari ndipo akataliwe. Inawezekana tabia yake haiendani tu na tabia yako.

Kwa vyovyote vile, usimruhusu mtu yeyote kukushinikiza katika kutoa uamuzi kabla hujawa tayari. Uamuzi ni jambo ambalo unapaswa kulifikia mwenyewe kupitia mchakato wa kiuchunguzi, na ni haki yako ya kisheria Kiislamu kukubali au kukataa posa. Kufanya uamuzi ni jambo ambalo limeelezewa kwa kina katika Sura ya 8.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 84 10/20/2015 4:31:59 PM

# SURA YA 8

## NITAJUAJE?

### HISIA YA KWAMBA "UNAJUA YA NDANI TU."

Kwa hiyo mwishowe unajuaje kwamba huyu ndiye anayefaa?

Wakati wawili wanapochumbiana au kuoana na wakaulizwa swali kuhusu mke/mume wake: "Ulijuaje?" mara nyingi hujibu: "Mimi nilijua ndani tu." Watu wanapopita kwenye mchakato wa kuchagua mwenza (mke/mume) mara nyingi huhoji fikira hii, kwa kuuliza, "Inawezekanaje kwamba unaweza kumpata mwenza wako wa maisha baada ya mikutano michache?" na "Unajuaje kwa ndani kwamba huyu ndiye atakayekufaa?"

**Moyo**

Hapa ndipo Mwenyezi Mungu anakuja kuingilia kati, kwani Yeye ni Mdhibiti nyoyo na ni Yeye ndiye anayetia matumaini moyoni mwako kama umempata mtu sawa yako au hapana (kupitia na sauti ya nafsi yako, kwa mfano). Anatuambia ndani ya Qur`ani:

وَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ ۚ لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِي ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا مَّآ أَلَّفْتَ بَيْنَ
قُلُوبِهِمْ وَلَٰكِنَّ ٱللَّهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ ۚ إِنَّهُۥ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٣﴾

**"Na akiziunga nyoyo zao, lau ungelitoa yote yaliyomo ardhini usingeliweza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu amewaunganisha, hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima." (al-Anfal; 8:63)**

Ayah ii inarejelea kwenye vita virefu baina ya makabila ya Aus na Khazaraj ambavyo vilitokea mjini Madinah, ambapo pande zote mbili zilikuwa zinachukiana sana kupita kiasi, hivyo kwamba pale Mtume Muhammad (s.a.w.w.), kupitia msaada wa Mwenyezi Mungu, aliweza kusimamia amani baina yao, wao walistaajabu.

Pale ambapo mwanadamu anapotafakari juu ya uhai wake wa ndani na maisha ya dunia ya nje inayomzunguka, atatambua jinsi kwa upande mwingine mwanadamu ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu mwenye uwezo mkubwa sana na kwamba dunia yote imewekwa chini ya mwanadamu:

۞ وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِيٓ ءَادَمَ وَحَمَلْنَٰهُمْ فِي ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ وَرَزَقْنَٰهُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَفَضَّلْنَٰهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾

**"Na hakika tumewatukuza wanadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba." (17:70)**

Lakini bado yu dhaifu, na Mwenyezi Mungu analijua hili kuhusu mwanadamu:

يُرِيدُ ٱللَّهُ أَن يُخَفِّفَ عَنكُمْ ۚ وَخُلِقَ ٱلْإِنسَٰنُ ضَعِيفًا ﴿٢٨﴾

**"Mwenyezi Mungu anataka kuwahafifishia, na mtu ameumbwa hali ya kuwa ni dhaifu." (4:28)**

Tupo chini ya huruma ya nguvu ya kimungu hivyo kwamba ingawa tunazo nguvu za akili za kuitumia mvua ambayo hunyesha kutoka juu mawinguni, bado sisi hatuna udhibiti juu ya uumbaji wa mvua halisi; tunazo nguvu za kiakili za kutumia nishati ya jua, mafuta kutoka ardhini, upepo unaovuma na kadhalika, lakini hatuna kabisa udhibiti juu ya kuwepo kwa vitu hivi, hivyo kwamba tunalazimika kungojea hadi elementi hizi zinaletwa kwenye uwepo ndipo tuwe na uwezo wa kuzitumia.

Kimsingi, kwa kutafakuri, mwanadamu hutambua kwa dhahiri kwamba kwa hakika kwamba ipo nguvu ya kimungu, na kwamba tupo chini ya huruma Yake. Mathalani, huwa tunafanya nini tunapofikiri? Huwa tunatumia nini wakati tunafikiri? Kwanza kabisa hiyo fikra ilikujaje na kuwepo ndani ya ubongo? Kwa nini hukuizuia fikra hiyo isije kuwepo kwenye akili yako? Mhemuko ni nini? Mhemuko wa hasira ulikujaje kuwepo? Mhemuko wa mvuto ulikujaje kuwepo? Kwa nini ulivutiwa kwa urahisi tu na mtu fulani alipoingia chumbani? Na kadhalika. Inakuwa dhahiri na wazi kwamba ndiyo, tunazo nguvu na uwezo wa kushughulikia fikra hizi na mihemuko hii, lakini kweli sisi tunao udhibiti na nguvu juu ya asili na kuwepo kwa fikra na mihemuko ya kwanza?

**Mapambano ya Ndani zaidi:**

Wakati kwa wakati yanakuwepo ndani mwetu mapambano makubwa ya ndani kwa ndani, baina ya nafsi yenye kujilaumu (*nafs lawwaama*) na nafsi yenye kuamrisha maovu (*nafs ammara*), ambapo nafsi ya ammara wakati wote hujaribu kutuvuta na kutuondosha kutoka kwenye wema kwa kutumia minong`ono ya Kishetani:

وَإِمَّا يَنزَغَنَّكَ مِنَ ٱلشَّيْطَٰنِ نَزْغٌ

**"Na kama uchochezi wa shetani ukikusumbua,….." (7:200)**

"Baada ya mkutano wangu wa kwanza, upande wa pili walikuwa na hamu ya kutaka kujua uamuzi wangu bila kuchelewa sana, labda ni kwa sababu ya ukweli kwamba wazazi wa kijana walikuwa wanaishi nje ya nchi na kwa hiyo walitaka kukamilisha mambo haraka iwezekanavyo kabla mama yake hajaondoka. Mvulana huyo alikwishafanya uamuzi kwamba alitaka kuendelea na posa hii. Mimi kwa upande mwingine, nilihisi kwamba nilikuwa ninashinikizwa na familia ya mposaji kufanya uamuzi haraka. Sidhani kama nilipewa muda wa kutosha kuchunguza matakwa yake kwani mkutano wetu wa kwanza ulikuwa kwa muda wa saa moja tu, na mkutano wa pili, uliofanyika wiki iliyofuata ulidumu kwa muda wa nusu saa tu ambapo baada ya hapo alikuwa asafiri. Kwa hiyo, sidhani kama nilipata fursa ya kumjua vizuri kama ambavyo ningeweza, wakati huo. Pia ninadhani kwamba tamaduni na mila zetu zinaturudisha nyuma wakati mwingine. Mathalani, palikuwepo na mawazo ya kudumu kuhusu muda wa sisi kuweza kuzungumza, kutokana na sababu kwamba 'kimila' ilikuwa ni makosa kuzungumza kwa zaidi ya saa moja, kufuatana na upande wa mposaji."- **Mwanamke, Uingereza.**

Wakati huo huo, nafsi lawama kwa mfululizo huwa inajaribu kutuvuta sisi na kutuelekeza kwenye wema kwa kutumia akili na mzinduko wa kimbinguni:

..... وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّ ٱللَّهَ يَحُولُ بَيۡنَ ٱلۡمَرۡءِ وَقَلۡبِهِۦ ......

**"…Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake……" (8:24)**

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِن تَتَّقُوا۟ ٱللَّهَ يَجْعَل لَّكُمْ فُرْقَانًا .....

**"Enyi mlioamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atawajaalia upambanuzi…[51]" (8:29)**

Ili kuweza kuelezea vita hii ya ndani kwa ndani kwa uwazi zaidi, hebu tuangalie mfano ufuatao:

Fikiria asubuhi ya baridi ya majira ya kipupwe. Kengele ya kamsa kwa ajili ya sala ya Alfajiri ndiyo imeanza kulia; muda wa Sala umewadia na Shetani pia amewadia! Kutokea upande mmoja, *nafs ammara* haraka sana inaanza kazi yake: "Oh, kuna baridi, kaa kitandani kwa dakika zingine kumi zaidi, itegeshe hiyo kamsa katika hali ya kusinzia, Mwenyezi Mungu ataelewa kwamba hukulala vizuri usiku, Mwenyezi Mungu ataelewa kwamba una mitihani leo, na kadhalika." Kutokea upande mwingine inakuja minong`ono ya kimungu kutoka kwenye *nafs lawwaama*: "Amka na uende kukutana na Mola Wako, nenda ukamwombe Mola Wako na uombe msaada na muongozo Wake katika kila kitu unachonuia kufanya leo, mara utakaponyanyuka utajisikia vizuri!" Halafu akili inakuwa hiari ya kuamua isikilize mnong`ono wa ndani gani kati ya hiyo.

Kanuni hiyo hapo juu pia inaweza kutumika pale ambapo wachumba wapo kwenye mlolongo wa uchunguzi, ambapo baada ya kipindi cha mikutano, wachumba hao vijana huwa 'wanajua tu' kwamba wao wanachukuana au hapana, kupitia muongozo wa Mwenyezi Mungu (kama ilivyotajwa hapo juu). Wakati tu wachumba hao wanapokuwa na uhakika wa kile ambacho kila mmoja wao anachokitaka hapo minong`ono ya Shetani huanza: "Kwa nini unamkubali? Unastahili mtu mwingine bora zaidi ya huyu, huyu ni mshika dini sana hakufai."

[51] Hiyo ni elimu ambayo itawawezesha nyinyi kupambanua baina ya haki na batili.

Kwa upande mwingine, nyote wawili mnapokuwa na uhakika kwamba hamuwezi kuwa wachumba, minong`ono inakuwepo hapo: “Ni vema umwambie ndiyo, kamwe hutampata mtu mwingine aliye sawa yako, mwambie ndiyo, halafu unaweza kumbadilisha baada ya kuoana, mwitikie ndiyo, kwa vyovyote vile mwishoni mambo yatatengamaa, kubali kila kitu kwa sasa halafu baadaye tutayafanyia kazi,” na kadhalika.

**Ulinzi dhidi ya shetani:**

Sasa swali linajitokeza: “Nitajikingaje dhidi ya minong`ono ya uovu wa Shetani wakati wa kipindi cha mchakato wa uchunguzi wa kuchagua mchumba, na kutegemea hisia za ndani ya nafsi?”

**1.** Tafuta kinga kwa uaminifu kabisa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hivyo kwamba akulinde wewe dhidi ya minong`ono yake ya hila:

إِنَّ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوْا۟ إِذَا مَسَّهُمْ طَٰٓئِفٌ مِّنَ ٱلشَّيْطَٰنِ تَذَكَّرُوا۟ فَإِذَا هُم مُّبْصِرُونَ ﴿٢٠١﴾

**“Hakika wale wenye takua zinapowagusa pepesi za Shetani huzinduka.” (7:201)**

Kusoma Surat al-Nas ni mojawapo ya maombi ya moja kwa moja kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuomba kinga dhidi ya Shetani:



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 90 10/20/2015 4:32:01 PM

قُلۡ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ﴿١﴾

**"Najikinga kwa Mola wa watu,**

مَلِكِ ٱلنَّاسِ ﴿٢﴾

**"Mfalme wa watu,"**

إِلَٰهِ ٱلنَّاسِ ﴿٣﴾

**"Mwenyezi Mungu wa watu,"**

مِن شَرِّ ٱلۡوَسۡوَاسِ ٱلۡخَنَّاسِ ﴿٤﴾

**"Na shari ya mwenye kutia wasiwasi mwenye kurejea nyuma,"**

ٱلَّذِى يُوَسۡوِسُ فِى صُدُورِ ٱلنَّاسِ

**"Ambaye hutia wasiwasi katika nyoyo za watu,"**

مِنَ ٱلۡجِنَّةِ وَٱلنَّاسِ ﴿٦﴾

**"Miongoni mwa Majini na watu."**

**2.** Umwamini Mwenyezi Mungu, kwani Shetani hawezi kuwaathiri wale wanaomwamini na kumtegemea Mwenyezi Mungu:

إِنَّهُۥ لَيْسَ لَهُۥ سُلْطَٰنٌ عَلَى ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٩٩﴾

إِنَّمَا سُلْطَٰنُهُۥ عَلَى ٱلَّذِينَ يَتَوَلَّوْنَهُۥ وَٱلَّذِينَ هُم بِهِۦ مُشْرِكُونَ

**"Hakika yeye hana madaraka juu ya walioamini na wakamtegemea Mola wao. Hakika madaraka yake yako juu ya wale tu wanaomtawalisha na wale ambao kwaye wanaoshirikisha." (16:99-100)**

**3.** Wala hawezi kuwaathiri wale wenye takwa:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِن تَتَّقُوا۟ ٱللَّهَ يَجْعَل لَّكُمْ فُرْقَانًا .....

**"Enyi mlioamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atawajaalia upambanuzi ….." (8:29)**

Inshallah, kama kwa uhakika ni kweli unatafuta ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi kuwa na imani kwamba atakusaidia, na uwe na takwa, halafu hautakuwa mmojawapo wa wale wanaoikubali minong`ono ya Shetani. Qur`ani inatuambia sisi kuhusu mazungumzo baina ya Shetani na watu wa jahannam ambapo Shetani atasema:

وَمَا كَانَ لِىَ عَلَيْكُم مِّن سُلْطَٰنٍ إِلَّآ أَن دَعَوْتُكُمْ فَٱسْتَجَبْتُمْ لِى

**"….Na sikuwa na mamlaka juu yenu isipokuwa niliwaita mkaniitikia……" (14:22)**

## Akili

Hadi hapo tutakapofika kwenye kiwango cha imani ambapo tunaweza kuamini kwa ukweli kabisa ile miito yetu ya ndani na tunaweza 'kutambua' na kuchagua kwa usahihi baina ya ukweli na uongo, au baina ya shetani na mwema mtukufu, na kufanya maamuzi ambayo yameegemezwa juu ya sauti ya ndani peke yake ni hatari na ni lazima kuende sambamba na akili.

Jukumu kubwa la akili wakati wa kipindi cha mchakato wa kuchagua mchumba linahusisha kutathmini kwa uangalifu kila jibu la maswali yanayoulizwa kwenye mkutano. Akili lazima ihakikishe kwa busara kabisa iwapo kama majibu yanaridhisha na kuendana na matarajio au hapana, na iwapo 'kwenye maandishi' angalau, wachumba hao wana mlingano au hapana. Jukumu la akili kimsingi ni kuchukua hatua kurudi nyuma na kuchambua mazungumzo mstari kwa mstari, bila kutetereshwa na hisia binafsi. Matokeo ya mchakato huu ni kwamba itaonyesha kwa wazi maeneo ya ulinganifu na yasiyo ya ulinganifu baina ya wawili hao, ambayo yatatakiwa yajadiliwe zaidi.

## Kufanya Uamuzi

Wakati akili na nafsi (sauti ya ndani) zikiwa zinaendana na hakuna migongano baina ya uamuzi ambao akili imeufanya (kutegemea uchambuzi wa kimantiki), na vile nafsi inavyohisi, halafu hili sasa linawaongoza wale ambao wameposana au kuoana katika siku za karibuni kusema "Nilijua tu kwamba huyu ndiye alikuwa kwa ajili yangu" au "Ni vigumu kueleza hisia hizo, lakini nilikuwa ninajua tu."

Kwa maneno mengine, jinsi unavyopita kwenye hatua za uchunguzi, na kuwa na mazoea zaidi na mtu huyo, tabia zake, na



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 93 10/20/2015 4:32:04 PM

familia yake, kwa kawaida utavutiwa naye, au kutovutiwa naye. Hadi hapo muda utakapofika ambapo utajihisi umeridhika na kufurahi kuhusu uamuzi wako, ama ni wa kukubali au kukataa posa, usifayike uamuzi wa mwisho; badala yake mchakato wa uchunguzi na kufahamiana zaidi unapaswa uendelee, mpaka pawe hapana utata katika akili na moyo wako.

Ni huu muelekeano wa pamoja na mvuto uliopo ndani ya hao watu wawili ndiyo unaotengeneza mizizi ya mapenzi ya kudumu ambayo Mwenyezi Mungu huyaweka ndani ya mwanamume na mwanamke, na ambayo hudumu muda mrefu baada ya mapenzi ya ashiki yanayopita haraka. Na ni mapenzi haya, ambayo ingawa yanahitaji kufanyiwa kazi wakati wote wa maisha ya ndoa, ambayo yataruhusu wanandoa kukabiliana na mema na mabaya ya maisha, kwa vile wakati huo pana mapenzi ya wawili, mapungufu na kuteleza husamehewa na kusahauliwa kwa urahisi, na wakati mgumu huweza kuvumilika.

Kwa mara nyingine tena inafaa kukukumbusha wewe usijiamilishe kwenye shinikizo la nje unapofanya uamuzi, ulioelezwa kabla kwenye sura ya 7. Hivi ndivyo ilivyo hususani kama unadhani mtu huyo si sawa yako na huhisi mvuto wowote au muelekeo wowote kwake; usisikilize ahadi za watu kwamba mapenzi yatakuja yenyewe baada ya kuoana. Kama mizizi haipo, si tu kwamba mapenzi hayatajitokeza, lakini badala yake huzuni na chuki hutokeza, pamoja na machungu kwa ajili ya uamuzi mbaya ambao umefanywa.

"Wakati inapowadia ile siku ya kufanya uamuzi, hapo ndipo kwa ukweli na uhakika utakapojua – ambapo utakuwa uketi pale na kutoa uamuzi wa ndiyo au hapana. Ninajua kwamba kwa posa zilizopita, ningelikokoteza. Ningezungumza na marafiki/familia nyingi kuhusu jambo hilo-labda nilikuwa ninamtafuta mtu atakayetoa yale maelezo



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 94 10/20/2015 4:32:04 PM

ambayo mimi mwenyewe nilikuwa sijiamini kuyasema, ‘Hapana sio huyu.’ Hapa ndipo unapojua kwamba si sahihi anapokuwa wakati wote unapima mabaya na mazuri, wakati mambo madogo yanakusumbua sana unayafuta kwenye uwiano, wakati unapohisi kwamba kufanya uamuzi huu ni jambo kubwa sana duniani pale ambapo badala ya kuhisi msisimko kuhusu jambo hili unahisi kuzidiwa hofu kubwa na wasiwasi.

Pale anapokuja mtu sahihi – mambo hubadilika. Anaweza asilingane na vigezo vya mtu timilifu katika fikira zako, (na wote tunajua tunaye mmoja), kwa kweli wale waposaji wengine inawezekana walifuzu katika mambo mengi yaliyo kwenye orodha yako, lakini badala ya kuogopa kukutana au kuzungumza naye, unakuwa na shauku ya kukutana naye. Badala ya kupima mazuri na mabaya yake, unaacha kutilia maanani orodha chafu ya mapungufu (ingawa inaweza kuwepo-ambayo ni ndefu na chafu zaidi kuliko zingine.) yote haya kwa sababu unazo ‘hisia nzuri’ zilizoandikwa kwenye orodha yako ya mazuri.

“Sasa ninajua kwamba baadhi yenu lazima mnagumia kwa kutazama tu neno ‘hisia’, mimi nilikuwa mmoja wenu vilevile. Lakini kwa kuwa mkweli, hivyo ndivyo hasa ilivyo. Panapokuwa na nguvu isiyokanushika ambayo haikuruhusu kusema ‘hapana’, ambayo inakufanya utambue kusema ‘ndiyo’ unahisi kuwa ni sawa tu. Pale uamuzi ulio mkubwa kama wa kusema ndiyo kwa ajili ya ndoa, unaonekana kama ni kitu kidogo tu, na bado unasisimua, uamuzi ambao hivyo ndivyo unavyojua. Kamwe hapatakuwa na jibu zuri hili. Kamwe hapatakuwa na taa ya neno (yenye ishara ya umeme) iliyoandikwa jina lake, neno la kutoka kwa Mwenyezi Mungu likisema ‘ndiyo’, fidla (gitaa dogo lenye sura ya upinde) na maua nyuma yake (sisi wote hatupendi hivyo!) lakini Mwenyezi Mungu atakupa starehe (*sukuun*) hii, hisia hii ya amani – na hili ndilo unalolishikilia. Bado utakuwa na wasiwasi, bado utakuwa huna uhakika, lakini pamoja na yote hayo bado utataka kulifuata. Hivyo ndivyo nilivyojua.” **Mwanamke, Marekani.**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 95 10/20/2015 4:32:04 PM

## Dalili za Kawaida

Lengo la sehemu hii ni kusisitizia ishara halisi ambazo zinaonyesha iwapo kama akili na nafsi vinakubaliana kwa pamoja, au hapana.

**ANGALIZO**: Ni muhimu sana kuzingatia kwamba mambo yafuatayo si lazima yawe ya kushurutisha; yenyewe ni ya muongozo tu uliyoegemezwa kwenye uzoefu wa utabiri na hivyo yanaweza kuwa na uhusiano mdogo na wewe au hapana kabisa na yasitumike yenyewe tu kwa ajili ya kufanya uamuzi tu.

## Kuwaza

Kuwaza na uzingatiaji wa baadhi ya masuala fulani labda ni mojawapo ya nyenzo muhimu na yenye nguvu sana ambazo lazima uzitumie wakati wa hatua zote za uchunguzi na baada ya hapo wakati wa kipindi cha uchumba, kuweza kutambua kama umempata mtu aliye sawa yako au hapana.

Kuwaza kunatokana na uwezo wa kufikiri wa kila binadamu, na humruhusu mtu kuzingatia kweli kweli sura na uhalisia wa uamuzi unaowezekana. Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Unapokusudia kufanya jambo, fikiria matokeo yake kwanza. Endapo yatakuwa mazuri, basi endelea nalo, na kama yatakuwa mabaya, basi liache."[52]

Baadhi ya mambo ambayo unatakiwa kujaribu na kuzingatia:

### 1. Kuwa pamoja kama wenza

Mara nyingi hili ni mojawapo ya mambo magumu sana kuyafikiria, kwani mara nyingi sana mnakuwa mnajuana kidogo sana kuhusu maisha na mtindo wa maisha mwingine hususani kama familia zenu zikiwa zina taarifa ndogo juu ya historia ya pamoja. Hata hivyo, kwa taarifa ambayo mmekusanya wakati wa mchakato wa uchunguzi,

[52] *Al-Faqih*, Juz. 4, uk. 294, hadithi ya. 890



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 96 10/20/2015 4:32:04 PM

jaribuni kujiona kama wenza mlioko kwenye shughuli za maisha za kila siku, na kadhalika.

**2. Kuwa wenza miongoni mwa wengine**

Je, mnaweza kujifikiria kama wanandoa, mkiwa miongoni mwa kaka zenu, dada zenu, familia zenu, marafiki zenu, na kadhalika. Utajivuna kuwa naye mbele ya kila mtu, na kutokuwa na kuhofia wakati wote kuhusu nini watu wengine watasema nini kuhusu yeye au kwamba anaweza kukuaibisha?

**3. Kuwa marafiki wazuri sana**

Je! mnaweza kujiona kuwa marafiki wazuri sana, mnazungumza pamoja, mnafanya mazungumzo marefu pamoja, mnacheka pamoja, kukubaliana baada ya mabishano yoyote, bila ya kuwa kila mara mnaambiana mambo na kufurahia kimya pamoja.

**4. Kuwa sehemu ya familia ya kila mmoja wenu**

Je, mnaweza kujifikiria kuwa sehemu ya familia ya kila mmoja wenu, kuwatendea wazazi wenu wa pande zote na watoto wao kwa heshima na upendo, na kadhalika. Je, mnaweza kujihisi kila mmoja wenu akishiriki kwenye shughuli za kifamilia, na kufurahi na kujifunza kutoka kwenye familia. Hili ni muhimu sana kwa sababu kila mara watu wawili wanapoungana pamoja kwenye ndoa, pia familia mbili huungana pamoja. Kwa hiyo hakuna nafasi ya dharau au kutokuridhiana kuhusu jinsi familia nyingine inavyoishi au inavyoingiliana na watu wengine.

**5. Wazazi kwa Watoto Wenu**

Unaweza kumuwaza yeye kuwa baba wa watoto wako au mke huyo kuwa mama wa watoto wako. Kipengele hiki ni muhimu sana kwa



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 97 10/20/2015 4:32:04 PM

sababu kama unaweza kuvuta taswira ya yeye kuwa mzazi wa mtoto wako, mara nyingi utaweza kumuona yeye kuwa mwenza wako, kwa sababu sifa zile ambazo ungependa awe nazo kama mzazi kwa kawaida huwa ni sifa zile zile ambazo ungependa awe nazo kama mwenza.

### 6. Malengo

Malengo ni mambo ambayo kila mara ulikuwa ukifikiria ungeyafanya na mwenza wako. Wakati wowote mtu anapofikiria kuhusu ndoa, mara nyingi sana wanakuwa na shauku ya yale ambayo wangetaka kuyafanikisha wakiwa pamoja, kama vile kusafiri, kujifunza lugha, kufundisha kwenye madrasa, kujiunga na taasisi maalumu, kujifunza stadi mpya, kuhudhuria kozi/chuo kikuu, na kadhalika. Unaweza kutaamali mnafanya mambo hayo pamoja?

### 7. Kwa ajili ya wanawake tu:

Unapoona kwamba mambo yanakwenda vizuri, unaweza kuvuta taswira ukiwa unamkumbatia au kumshika mkono wake. Ni dhahiri kwamba huu ni mtihani mgumu kwa wanawake, kwa sababu wao kimsingi hawasukumwi na ashiki. Kama huipendi fikira hii basi kwa kawaida ni ishara nzuri ya jinsi nafsi yako inavyohisi hasa.

## FUNGA NDOA NA RAFIKI, SIO MPENZI

## MAPENZI DHIDI YA ASHIKI

Fungamano la kimwili na mvuto bila shaka ni jambo la muhimu sana unapochagua nusu yako ya pili (mchumba); hata hivyo, ni muhimu sana kuelewa kwamba kama fungamano la kimwili (linalosukumwa na ashiki) ndio jambo linalotawala na fungamano la kihisia (linaosu-

kumwa na urafiki na mapenzi) ni jambo linalofuata, au halipo kabisa, basi kila mara hili litakuwa vigumu kushughulikia. Dkt. Dorothy Tennov, mtafiti na mwanasaikolojia, aligundua kwamba "muda wa wastani wa msisitizo wa mahaba yasiyotulizika ni miaka miwili…. Hatimaye, hata hivyo, wote tunashuka kutoka mawinguni na kukanyaga ardhi tena. Macho yetu yanafunguka, na tunaona madutu ya mtu mwingine."[53]

Ndoa ambayo imeegemezwa kwenye fungamano la kihisia huelekea kuwa na kina zaidi na ukamilishaji na pia inaweza kuvumilia nyakati ngumu sana kuliko ndoa ambayo kimsingi imeegemezwa juu ya fungamano la kimwili, kwa sababu fungamano la kimwili kwa kawaida hupungua kufuatana na muda, ambapo fungamano la kihisia ni kinyume chake na huimarika kufuatana na muda, na hufanya hata lile fungamano la kimwili kuwa imara zaidi.

Baadhi ya ishara za halisia zilizoandikwa hapo juu zinaweza kukusaidia wewe kutambua kama fungamano hilo limesukumwa na mapenzi au ashiki.

[53] Gary Chapman, *The Five Love Languages*, Northfield Publishing, Chicago, 1995, uk. 30



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 99 10/20/2015 4:32:04 PM

# SURA 9

# ISTIKHARA

## ISTIKHARA NI NINI?

Istikhara ni utaratibu wa Kislamu ambao hutumiwa kufanyia uamuzi katika mambo muhimu ya maisha. Hili linapaswa kutumika pale tu ambapo uamuzi hauwezi kufanywa kupitia njia ya kutafakari, kutafuta ushauri na njia zingine za kawaida za kufanya maamuzi. Maana halisi ya Istikhara ni 'kutafuta uzuri' na kumwomba Mwenyezi Mungu kusaidia katika kufanya uamuzi huo. Utaratibu wa kawaida wa Istikhara hujumuisha swala, au kwa kutumia Qur`ani au Tasbiih; lakini kama tutakavyojadili, Istikhara inapaswa kuwa hatua ya mwisho katika kufanya uamuzi, na baada tu ya kutumia njia zingine zote na kushindwa kufikia uamuzi.

"Wakati mtu mmoja aliponiambia kwa mara ya kwanza kuhusu suala hili, nilifikiri, 'heeh?!' Lakini nilipoendelea kufikiri zaidi kuhusu swala hili, nilitambua kwamba kwa kweli ilikuwa ni sahihi kabisa. Kwa posa zilizopita ambazo sikuzifuatilia kwa sababu zingine, fikira ya mguso kimwili iliniondoa kwa nguvu kabisa." - **Mwanamke, Uingereza.**

**Matumizi ya Istikhara Katika Kuchagua Mchumba:**

Falsafa isiyo sahihi ambayo watu wengi wameambatana nayo ni Istikhara, au kutafuta kilicho kizuri zaidi kutoka kwa Mwenyezi Mun-



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 100 10/20/2015 4:32:04 PM

gu, kabla ya kufunga ndoa. Katika sura hii, tutazungumzia pande zote mbili yaani matumizi sahihi ya istikhara na yasiyo sahihi kwa kina zaidi.

## Matumizi ya Istikhara Yasiyo Sahihi

Wakati mwingine, hata pale ambapo mvulana na msichana hawajapata fursa ya kukutana wao kwa wao na kuzungumza na kuona kama wanaendana wao kwa wao, wazazi watakimbilia kwenda kwa mwanazuoni mkazi kufanya Istikhara. Kama jibu likija 'zuri', basi hata kama mvulana au msichana ni mtu muovu mkubwa sana au mwenye tabia mbaya, wazazi watamkaribisha kwenye familia kwa mikono miwili mikunjufu. Kinyume chake vilevile imeonekana kwamba kama mvulana au msichana ni mtu muadilifu, mwema, na muumini mcha-Mungu, lakini Istikhara ikitoa jibu 'baya' basi anakataliwa moja kwa moja bila ya fursa ya kuendelea mbele.

Nyakati nyingine, watu mara nyingi hupita kwenye kazi ngumu zote na michakato ya kutathmini iwapo kama wamepata mtu aliye sahihi, na halafu kwa bahati mbaya, bila kujali wachumba watarajiwa hao wanavyohisi, familia hutumia Istikhara ya Qur`ani kwa lengo la kufanya uamuzi wao wa mwisho na wa fungamano.

Kwa hiyo, lengo la sehemu hii ni kujaribu kupata uelewa bora zaidi wa mchakato huo wa Istikhara, kuondosha uelewa mbaya uliopo sasa kuhusu wajibu wa Istikhara, na kuelezea hatua ambazo mtu lazima azichukue kabla ya kutumia Qur`ani kama njia ya kufanyia Istikhara.

## Matumizi Sahihi ya Istikhara:

Istikhara ni utaratibu ambao umefundishwa na kuthibitishwa na Mtume wetu (s.a.w.w.) na Ahlul Bayt (a.s.); hata hivyo, yapo

masharti ya mwanzo mengi na hatua ambazo lazima zifuatwe kabla hatujakimbilia kwenye Qur`ani au Tasbih kwa ajili ya Istikhara.

Kuhusiana na ndoa, na pia kuzungumza na mvulana au msichana na kupata kujua mawazo yao, maoni na imani zao, hatua za Istikhara zinajumuisha:

**1. Istikhara kwa kuomba Dua:**

Hili linahusisha kumsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu, ikiunganishwa na staha na unyenyekevu katika kuelekea Kwake, pamoja na mtu kuomba mahitaji na matakwa yake kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Pia mtu anapaswa kuwa na dhana nzuri juu ya Mwenyezi Mungu na kujua kwamba Yeye hupendelea na kukubali lile ambalo ni zuri kwa waja Wake. Jambo la muhimu zaidi ni kwamba mtu awe na utulivu wa akili na moyo safi wakati anatekeleza kitendo chochote.

Kwenye kitabu chake Muhammad Baqir Haidari, kiitwacho; *'Istikhara'*[54] anasema kwamba: "Istikhara kwa kusoma dua kwa wakati wowote inachukua umuhimu wa kwanza na ndani ya hadithi imeelezwa kwamba inapaswa kusomwa kabla ya kufanya kitendo chochote."

Dua nyingi (kama vile dua ya 33 katika *as-Sahifah al-Kamilah as-Sajjadiyah*, ijulikanayo kama dua ya kuomba kilicho bora zaidi) inapaswa kusomwa, na huyo mtu lazima amwombe Mwenyezi Mungu kwa uaminifu kabisa kuiongoza nafsi yake kwenye kitu kile ambacho kwa kweli ndio bora zaidi.

**2. Istikhara ya kutafuta ushauri kutoka kwa wengine:**

Mtu anapotaka kujua ni nini hasa ambacho ndio kizuri zaidi kwa ajili yake, huomba ushauri kutoka kwa waumini ambao wana uwezo

[54] Kimetafsiriwa na Saleem Bhimji.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 102 10/20/2015 4:32:04 PM

wa kutoa ushauri huu. Kabla mtu hajaendelea na njia hii ya kutafuta ushauri, anapaswa kusoma dua na amwombe Mwenyezi Mungu amuongoze kupata kile kilicho bora zaidi na halafu aendelee kuwaomba wengine ushauri, ili kwamba dua hizi ziweze kumpa matokeo mazuri zaidi. Ni kupitia dua na fadhila mahsusi za Mwenyezi Mungu ambazo kwazo ushauri unatolewa na watu wengine na kwamba Yeye humuongoza mtu kwenye kile ambacho ni bora zaidi kwa ajili yake.

Kuwauliza marafiki na watu wa familia kuhusu mvulana au msichana pia inapendekezwa. Ingawa katika Uislamu, imeharamishwa kusengenya au kuzungumza mabaya kuhusu wengine, hata hivyo, Ulamaa wamesema kwamba haya ni mojawapo ya mazingira ambamo sheria imetoa mwanya, kwa ajili ya uboreshaji wa muundo wa familia.

**3. Istikhara kwa kuomba dua kwa mara ya pili:**

Endapo hata baada ya kuomba dua, kuomba kile kilicho bora zaidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kwa kutumia akili zake, na pia fikira, utafiti na kuomba ushauri kutoka kwa wengine, mtu anakuwa bado hajaweza kufikia hitimisho na bado anakuwa na shaka na kutokuwa na uhakika ndani ya moyo wake, basi jambo zuri zaidi la kufanya ni kurudi kwa Mwenyezi Mungu kwa mara nyingine – Mrekebishaji halisi wa moyo – na amwombe Yeye kukinahi kwa moyo, msaada, na kuondosha tashwishi zote na uchanganyikiwaji.

Kama kweli mtu bado anayo shaka baada ya kupitia hatua zote hizi, hapo na ni hapo tu ndipo mtu anaweza kukimbilia Istikhara 'ya kawaida' ambayo tuna mazoea nayo.

**4. Istikhara ya kutumia Qur`ani:**

Endapo baada ya mtu kusoma dua kwa ajili ya kuomba apate kile kilicho bora zaidi na baada ya kufikiri na kuwaomba ushauri wen-



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 103 10/20/2015 4:32:04 PM

gine, bado hajapata amani na utulivu wa akili, ni hapo tu ambapo anapaswa kurejea kwenye Qur`ani ili kuondosha shaka zote na kutafuta jawabu. Istikhara hii kwa kawaida hufanywa na mwanazuoni (A'alim).

Kama Istikhara ikiashiria 'wema,' basi mtu anapaswa kufanya jambo lake na ajihisi amani; na kama matokeo yanakuwa 'mabaya', basi mtu anapaswa kuweka imani na mategemeo juu ya Mwenyezi Mungu na asiendelee na mipango yake.

Mbinu ya kubainisha kama matokeo ni 'mazuri' au 'mabaya' kutoka kwenye Qur`ani ni kwamba baada ya taratibu na masharti yote ya kufanya Istikhara kwa kutumia Qur`ani yametimizwa, endapo hiyo aya inayokuja ni ile ambayo inaamuru kwenye jambo zuri, wasifu wa Waumini, thawabu za wale watakaoishi Peponi, au bishara njema za Peponi – basi Istikhara hiyo itaashiria 'uzuri' na mtu anapaswa kuendelea na jambo alilonuia kulifanya akiwa na amani ndani ya moyo wake.

Hata hivyo, kama aya inayotokeza ni ile inayotaja ghadhabu au adhabu ya Mwenyezi Mungu, kukataza maovu, kueleza sifa za wasioamini na wanafiki, maelezo au ufafanuzi wa adhabu ya jahannam – basi mtu anapaswa kuomba hifadhi kwa Mwenyezi Mungu na asitekeleze hilo alilolikusudia. Endapo aya inayotokeza imo katikati ya aina mbili zilizotangulia kutajwa, basi Istikhara itambuliwe kama isiyopendelea upande wowote.

### 5. Istikhara ya kutumia Tasbihi:

Kufanya Istikhara hii, tasbihi inapaswa kushikiliwa mkononi na kumsalia Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na kizazi chake mara tatu pamoja na du'a zingine fupi. Halafu, unapaswa kushika sehemu fulani kwenye tasbihi hiyo halafu unahesabu mbili mbili. Endapo



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 104 10/20/2015 4:32:04 PM

mwishoni unabaki punje moja tu, basi unapaswa kutekeleza lile jambo lako; na kama punje mbili zinabakia, basi usiendelee na mpango wako.

Kwa maelezo zaidi juu ya jinsi ya kufanya Istikhara, pamoja na muda mzuri sana wa kuzifanya, na kadhalika, tafadhali rejea kwenye kitabu kiitwacho "*Istikhara*" cha Muhammad Baqir Haideri. Pia kinapatikana kwenye mtandao kwa anuani ifuatayo ***http://www.al-Islam.org/Istikharaa/.***

Kwa hiyo, katika kuhitimisha tumeona kwamba fikira ya kutumia Istikhara ya Qur`ani na Tasbihi kama kimbilio la kwanza, ambalo limeenea sana miongoni mwa jamii ya Waislamu, inapaswa kujaribu kuzuiliwa na kusimamishwa kabisa, kwani inaonekana kutokuwa na msingi wowote wa kweli hasa katika Uislamu kama kimbilio la kwanza katika kufanya maamuzi.

## MAONI YA WANACHUONI MASHUHURI (ULAMAA)

## JUU YA MATUMIZI YA ISTIKHARA.

**Imam Khomeini (r.a.)**[55]

Wakati akizungumzia matumizi yasiyofaa ya Istikhara, Imam Khomein alielezea mfano ufuatao:

"…Tukio ambalo alikuwepo msichana aliyempenda mvulana na katika hali zote, walikuwa wanaendana, lakini baada ya kuzungumza wao kwa wao, Istikhara ilifanywa na matokeo yake yakawa 'mabaya' na mazungumzo yakaishia hapo.

[55] Muhammad Baqir Haideri, *Istikhaara*, uk. 72



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 105 10/20/2015 4:32:04 PM

"Ni wazi kwamba majibu kwao hawa na maelfu ya watu kama hawa kuhusu Istikhara (na matumizi yake yanayofaa) ni kwamba kwenye mifano kama hii, ni mtu yule tu asiye na akili, ambaye hajali na ambaye hana uelewa sahihi wa Istikhara atafanya Istikhara kwenye mazingira haya."

**Allama Sayyid Muhammad Husayn Tabatabai (r.a.)**[56]

"Istikhara ni njia ambayo mtu anakombolewa kutoka kwenye tashwishi na kutokuwa na uhakika. Hata hivyo, kuhusu athari ambazo zitajitokeza baadaye kwa ama kufanya au kutokufanya jambo hilo, hayatakuwa ni wajibu wa Istikhara, na Istikhara haina uhusiano na hili.

"Mustakabali wa mtu anayefanya Istikhara – ima utakuwa mzuri au mbaya – ni sawa tu na yule mtu ambaye hakufanya Istikhara na akaendelea na maisha yake akitumia akili yake mwenyewe na kuomba ushauri kutoka kwa wengine. Kwa ufupi, Istikhara si lolote zaidi ya kitendo kinacholeta 'kuridhika kwa moyo,' 'huondoa shaka na kutokuwa na uhakika' na kama nyenzo ya 'matumaini, ustawi na furaha.'

"Kutoka kwenye riwaya za kuaminika zilizosimuliwa kutoka kwenye vitabu vya Shia na Ahl al-Sunnah, imetajwa kwamba Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alikuwa na desturi ya kuomba kilicho bora zaidi na aliendelea na maisha yake na alikuwa na kawaida ya kuwatia moyo wale waliokuwa karibu naye kufanya hivyo. Aliwakanya watu kuipuuza Istikhara….

"…Kwa hiyo, lipo tatizo katika kufanya Istikhara kwa njia ya Qur`ani au vitu vingine, kwani kama Istikhara inatoa jibu la kupendeza, basi mhusika atafanya jambo lake huku moyo wake

[56] Muhammad Baqir Haideri, *Istikhaara*, uk. 74-75



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 106 10/20/2015 4:32:04 PM

ukiwa umeridhika na nafsi yake kuwa safi; na kama jibu likiwa baya basi mtu amtegemee Mwenyezi Mungu na anapaswa kuendelea na shughuli zake zingine (na asifanye lile jambo ambalo alijaribu kulitafutia jibu kutoka kwenye Istikhara).

> "Baada ya vipingamizi vingi sana katika mchakato wa kutafuta mchumba, hatimaye nilikutana na mtu fulani ambaye nilihisi alikuwa na maadili kama ya kwangu na alionekana kuwa wa sawa katika viwango vingi, kuanzia kwenye msimamo wake juu ya dini hadi vile nilivyostarehe sana kwa ukaribu miongoni mwa familia yake. Tulipata kufahamiana kwa miezi michache na palikuwepo na shauku ya wazi katika kuyaendeleza mambo mbele kutoka kwenye familia zote na muhimu zaidi, yeye na mimi. Hata hivyo, kabla ya kufika kwenye kufanya uamuzi, upande wake (mwanamke) uliamua kwamba inapasa kufanya Istikhara- 'katika kujikinaisha tu.' Pamoja na ukweli kwamba, ilikuwa wazi kwa wote sisi wawili kwamba tulikuwa tunataka jibu zuri, bado waliendelea na mpango huo. Matokeo ni kwamba jibu lilikuwa 'baya' na baadaye athari za kihisia zilikuwa nzito sana hususani mama zetu!
>
> Niliomba kupata ushauri kutoka kwenye ofisi ya Ayatullah Sistani kama palikuwepo na uwezekano wa kupata ufumbuzi. Jibu lilikuwa zuri -tungeweza kuendelea na mpango wetu kinyume na matokeo ya Istikhara kufuatana na mazingira yetu hayo alimuradi tutoe sadaka, lakini jibu lilichelewa mno hivyo kwamba uhusiano wetu ulikwisha vunjika. Na nilianza upya." - **Mwanaume, Uingereza**

# SURA YA 10

# KUMTEGEMEA MWENYEZI MUNGU

## KUKABILIANA NA MATATIZO YENYE UWEZEKANO

Ni muhimu kuzingatia kwamba mara unapokuwa umedhamiria ya kwamba unataka kuchumbia au kufunga ndoa na upo tayari kuanza kutafuta, mwanzoni mambo yanaweza yasiende kwa haraka na urahisi. Yapo matatizo kadhaa ambayo unaweza kukabiliana nayo, kama vile:

- Hujui ni nani wa kwenda kukutana naye
- Huwezi kumpata mtu anayefaa na hujui kama utampata kamwe mtu aliye sahihi.
- Ulidhani umempata mtu aliye sahihi hasa lakini alikataa
- Ndio kwanza umepita kwenye uchumba uliovunjika
- Na mazingira mengine mengi kama hayo….

Katika hali zote hizi, lazima usikate tamaa au kuvunjika moyo; kumbuka, Mwenyezi Mungu yupo, na kwa uhakika atakufungulia milango.

### Taasisi ya Ndoa

Qur`ani na hadithi, vyote vimesisitiza kwamba ndoa ni taasisi ambayo inapendwa sana na Mwenyezi Mungu, Mtukufu Mtume



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 108 10/20/2015 4:32:04 PM

(s.a.w.w.), na Ahlul Bayt (a.s.). Kwa hiyo, kama mtu anataka kufuata Sunnah ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa ukweli kabisa na akafunga ndoa, inaonekana haielekei kwamba Mwenyezi Mungu, anapoendewa kwa moyo safi, hatafungua milango kwa mtu kama huyo. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Hakuna taasisi katika Uislamu inayopendwa zaidi na yenye thamani kwa Mwenyezi Mungu kuliko ndoa."[57]

Endapo dhana ya ndoa inapendekezwa mno mbele ya Mwenyezi Mungu, na mtu akataka kuingia kwenye sunnah hii iliyokokotezwa, inawezekanaje iwe kwamba Mwenyezi Mungu hatamnyooshea mkono mja wake huyo? Hususani pale ambapo amesema ndani ya Qur`ani Tukufu:

وَٱللَّهُ جَعَلَ لَكُم مِّنۡ أَنفُسِكُمۡ أَزۡوَٰجٗا وَجَعَلَ لَكُم مِّنۡ أَزۡوَٰجِكُم بَنِينَ
وَحَفَدَةٗ وَرَزَقَكُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِۚ أَفَبِٱلۡبَٰطِلِ يُؤۡمِنُونَ وَبِنِعۡمَتِ ٱللَّهِ هُمۡ
يَكۡفُرُونَ ٧٢

**"Na Mwenyezi Mungu amewafanyia wake kutoka na ninyi wenyewe, na amewafanyia kutoka kwa wake zenu wana na wajukuu, na akawaruzuku vitu vizuri. Basi je, wanaamini upotofu na wanazikufuru neema za Mwenyezi Mungu?" (16:72).**

Kwa hiyo ombeni Kwake na muelekeze du'a zenu Kwake Yeye tu kwa moyo safi! Nyoosheni mikono yenu kuelekea Kwake, ombeni kutoka Kwake tu! Mlilieni Yeye tu! Kwani Yeye Mwenyewe anatuambia kwamba:

57 *Bihar al-Anwar*, uk. 222, Na. 34

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِى عَنِّى فَإِنِّى قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ
فَلْيَسْتَجِيبُوا۟ لِى وَلْيُؤْمِنُوا۟ بِى لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

**"Na waja wangu watakapokuuliza habari yangu, Mimi niko karibu. Naitikia maombi ya muombaji anaponiomba. Basi na waniitikie Mimi na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka."(2:186)**

Mwenyezi Mungu hututahini kwa njia nyingi, lakini si zaidi ya zile tunazoweza kuvumilia. Anatuambia:

وَلَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا

**"Na hatuikalifishi nafsi ila kwa uwezo wake,….." (23:62)**

Wakati mwingine, kuna masuala ambamo takriban unakuwa na uhakika kwamba umempata mtu aliye sawasawa kwako, halafu unapeleka posa na unaona imekataliwa, kumbuka kwamba Mwenyezi Mungu anasema:

"..... وَعَسَىٰٓ أَن تَكْرَهُوا۟ شَيْـًٔا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰٓ أَن تُحِبُّوا۟ شَيْـًٔا
وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

**"…..Na huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu, na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua, na nyinyi hamjui." (2:216)**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 110 10/20/2015 4:32:06 PM

## Umuhimu wa Kuswali Swala ya Rakaa Mbili

Swala ya rakaa mbili inaweza kuswaliwa wakati wowote, ikikuletea wewe amani ya moyo na akili bila kikwazo, ambayo huja kwa kumuomba Mwenyezi Mungu, na Yeye tu, kwa ajili ya mahitaji na matamanio yako. Hasa, inapendekezwa kwamba swala ya rakaa mbili iswaliwe kabla na baada ya kukutana, na kwamba unaomba msaada wa Mwenyezi Mungu wakati wa mchakato wote.

## Umuhimu wa Kuomba *Tawassul* (Uombezi) kutoka kwa Maasumina:

Uombezi, au kutafuta njia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Maasumina, ni mbinu nyingine ambayo unaweza kuomba msaada na muongozo wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur`ani Tukufu:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱبۡتَغُوٓاْ إِلَيۡهِ ٱلۡوَسِيلَةَ وَجَٰهِدُواْ فِي
سَبِيلِهِۦ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ ٣٥

**"Enyi mlioamini mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikia. Mfanye juhudi katika njia Yake ili mpate kufaulu." (5:35)**

Yafuatayo ni maelezo ya jinsi kutafuta Uombezi kulivyomsaidia mtu fulani katika haja yake ya kutaka kuoa: Muujiza katika ardhi ya Mashhad: Jinsi Imam alivyomsaidia mwenye kuzuru kumpata mwenza wake wa maisha.[58]

Tukio la kimujiza lifuatalo limesimuliwa kwa Thiqat-ul-Islam Haj Sheikh `Ali Akbar Moravvej kutoka kwa Sheikh Muhammad

---

58 Mirza Mohammad Ali Khorasani, *Mashhad - The Land of Miracles*



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 111 10/20/2015 4:32:06 PM

ambaye alikuwa mtunza viatu hapo kwenye Kuba. Alikuwa amesikia kutoka kwa marehemu Mirza `Ali Naqi Qazwinii, ambaye alisema:

"Ilikuwa ni wakati wa *Nawruuz* (sikukuu ya mwaka mpya wa ki-Irani) na nilikuwa nimetoka kuelekea kwenye Kuba takatifu ili kwamba niweze kuwepo pale wakati mwaka mpya wa (Ki-Irani) utakapoanza. Kama ilivyo kawaida, ndani na nje ya Kuba hiyo takatifu kulijaa umati wa wafanya ziara, ambao walikusudia kutumia muda wa Mwaka Mpya wakiwa na mpendwa Imam wao, kama mimi mwenyewe nilivyokuwa.

Hata hivyo, niliweza kujipatia sehemu karibu na Kuba hiyo takatifu lakini kwa matatizo sana, na karibu yangu alikuwepo kijana ambaye alinishauri, "Muombe kwa kumsihi Imam na kwa lolote unalotaka. Uwe na uhakika kwamba atajibu wito wako na kutimiza mahitaji yako!" Niliposikia maoni ya huyu mfanya ziara kijana nilifikiria kwamba lazima atakuwa ama ananifanyia mzaha au amepata wazimu kidogo! Kana kwamba alikuwa ameisoma akili yangu, akasema: "Kamwe usifikirie kwamba mimi sina imani kwa Imam wangu au kwamba siko makini ninapokwambia kwamba atakutekelezea matakwa yako! Nimeona jinsi anavyofanya miujiza. Sasa nisikilize na acha wengine wajue jinsi alivyo na huruma." Bwana huyo akaendelea: "Kwanza, niruhusu nijitambulishe, mimi ninaitwa Nasrullah, kutoka Kashmir. Huko nyumbani baba yangu alikuwa na kawaida ya kunifanyia mambo yasiyofaa. Kwa hiyo, niliamua kuondoka Kashmir na kuelekea hapa Mashhad kutekeleza ziara na kuzuru Kuba takatifu iliyobarikiwa ya Imam mashuhuri, na wakati huo huo nimuombe amshauri mzee wangu arekebishe tabia yake! Kwa hiyo, nilianza safari yangu kuelekea Mashhad kwa miguu.

"Niliwasili kwenye mji mtakatifu salama baada ya siku kadhaa na nilikuwa mgeni wakati huo na nilikuwa sina mtu wa kumtembelea,



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 112 10/20/2015 4:32:06 PM

mara moja nilikwenda kuzuru ile sehemu takatifu (Kuba). Niliingia ndani nikasoma Ziyarat. Nilipokuwa karibu na kaburi iliyo tukufu, kwa bahati nilimtupia jicho msichana ambaye alikuwa pale na mama yake kwa ajili ya Ziyarat. Nilimpenda kwa kumuona kwa ile mara ya kwanza. Halafu nilikwenda kwenye kaburi, nikalishika na kumsihi Imam, 'Nimemuona msichana kwenye kaburi lako tukufu na ningependa kumuoa, kwa hiyo, tafadhali nikubalie matakwa yangu na uifanye ndoto yangu iwe ya kweli!' Halafu niliendelea kulia na kumsihi Imam mtukufu kwa unyenyekevu ili anikubalie maombi yangu, nikiwa nimesahau kabisa sababu iliyonifanya nije kwake. Nilichoka lakini bado niliendelea kushikilia kaburi huku nikirudia rudia ombi langu kwa Imam mtukufu! Halafu, nikaona taa za ndani na nje ya eneo hilo tukufu zote zimewashwa na nikatambua kwamba huo ulikuwa wakati wa swala za jioni. Nikaswali swala zangu na kwa mara nyingine tena nikaenda kwenye lile kaburi, nikalishika na kuanza kumsihi Imam mtukufu tena.

"Nilikuwa ninasema: 'Ee Bwana! Sitakuacha wewe hadi utakapokuwa umetimiza haja yangu!' Halafu ghafla nikasikia sauti inasema *'Ayyuhal Mu`minun! Fi-Amanillah* (Enyi wafanya ziara mlioamini! Mwenyezi Mungu awe nanyi katika kuondoka kwenu)' Niliondoka na kuelekea kwenye mlango wa kutokea kwa haraka kwani nilifikiria walinzi wa Haram hiyo walikuwa wanafunga sehemu hiyo takatifu kwa lengo maalum! Nilipofika kwenye meza ya mtunza viatu ili nichukue viatu vyangu, nilimuona mtu mmoja ameegemea kwenye mlango. Nilipomkaribia akasema, 'Wewe ndiye Nasrullah Kashmiri?' Nikiwa na mshangao mkubwa nikasema, 'Ndiyo wewe ni nani?' Akasema: 'Hebu nifuate, umeitwa huku!'

"Nikaanza kumfuata, na mwanzoni nilikuwa ninafikiria kwamba kwa kuwa niliondoka nyumbani bila kupata ruhusa ya baba yangu au hata kuwataarifu watu wa familia yangu, inawezekana baba



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 113 10/20/2015 4:32:06 PM

yangu amemwambia mmojawapo wa marafiki zake wa Mashhad watafute niko wapi na mtu huyu anaweza kuwa rafiki yake baba yangu na ananichukua kunipeleka kwake, ili niadhibiwe! Mtu huyu alinipeleka kwenye nyumba moja kubwa na aliniongoza kwa mtu aliyekuwa ananingojea mimi kwenye chumba kizuri. Aliponiona mimi akauliza, 'Wewe ni Nasrullah Kashmiri?' 'Ndiyo,' nikajibu, 'lakini wewe ni nani na unanijuaje mimi?'

"Mtu huyo akasema, 'Naam, baada ya muda mfupi utajua yote kuhusu mimi!' Halafu akamgeukia mmoja wa watumishi wake na akasema, 'Nenda kwa shemeji yangu na umwambie kwamba ningependa kumuona haraka iwezekanavyo.' Mtumishi aliondoka na baada ya muda mfupi alirudi akiwa amefuatana na huyo shemeji mtu. Walisalimiana na halafu huyo bwana akamwambia shemeji yake, 'Naam, ukweli ni kwamba mimi nimekuita hapa ili nikuambie jambo muhimu sana! Mchana huu baada ya chakula, dada yangu na binti yangu walikwenda kuzuru kaburi takatifu la Imam Ridha (a.s) ambapo wakati huo mimi nilikwenda chumbani kwangu kwa ajili ya usingizi mfupi wa mchana. Niliota ndoto ambayo ndani yake nilisikia mtu anagonga mlango. Nilipouliza alikuwa ni nani, mtu akasema, 'Imam Ridha angependa kukuona.'

Nikiwa nimefurahi kupita kiasi, niliamka kwa haraka, nikavaa nguo na kuelekea kwenye kaburi. Nilipolifikia tao la dhahabu *'Ivan-e Tala'*, nilimuona Imam Ridha akiwa ameketi kwenye busati hapo, lakini hapana mtu mwingine aliyeweza kumtambua yeye isipokuwa mimi tu. Aliponiona alisimama na akanikaribisha niketi. Na halafu akasema: "Huyu ni Mirza Nasrullah. Amemuona binti yako na amenisihi mimi nifanye mpango wa wao kuoana! Mimi nina uhakika watakuwa wenye kuchukuana vizuri kabisa! Sasa je, utamtoa binti yako ili aolewe na mtu huyu?' Yote haya yalitokea wakati nikiwa kwenye usingizi mfupi wa mchana (*kailula*), na niliyatambua wakati nilipoamka.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 114 10/20/2015 4:32:06 PM

Halafu mara moja nikamtuma mtumishi wangu kumtafuta Mirza Nasrullah, nikimpa maelekezo sahihi ya sura yake, ambayo niliiona kwenye ndoto yangu. Nilimwambia mfanyakazi wangu. 'Kamlete hapa!' Na sasa kama unavyomuona Mirza Nasrullah yupo hapa! Ndiyo sababu nimekuita wewe hapa kwani ningependa kupata ushauri wako juu ya jambo hili!'"

"Shemeji yake akasema, 'Pale ambapo Imam wetu mtukufu anapoamuru jambo lolote mimi ni nani kuwa na lolote la kuongeza? Ni wajibu wetu wa lazima kukubali maagizo yake na mimi nina uhakika (binti yako) atamfurahia sana huyo mtu ambaye amethibitishwa na Imam!' Niliposikia maoni ya bwana huyo na uthibitisho wa shemeji yake, niliangua kilio kwa furaha, kwani niliona jinsi haja yangu ilivyotimizwa kwa ukamilifu na uzuri kabisa na Imam mtukufu, mwenye moyo wa huruma.

"Baadaye matayarisho muhimu kwa ajili ya sherehe za harusi yalifanywa na bwana huyo muungwana. Waliwaalika watu wa familia yangu ambao kwa hali hiyo walishangazwa sana walipoona kwamba kijana wao alikuwa amechagua mwenza wa maisha kutoka kwenye familia maarufu. Nilifunga ndoa na mwanamke ambaye posa yake niliiomba kupitia kwa Imam mtukufu (a.s.) na tulikukuwa miongoni mwa wanandoa waliobarikiwa sana hapa duniani.

"Ndiyo maana, nilikushauri uombe kitu chochote kwa Imam Ridha na haja yako kwa hakika itakubaliwa."

## DUA ZILIZOPENDEKEZWA[59]

**1.** Imesimuliwa ndani ya hadithi kutoka kwa Imam Sadiq (a.s.) kwamba wakati wowote mtu anapokuwa na dhamira ya kupo-

[59] Wakati ambapo zipo dua nyingi sana kwenye mtandao na vitabu, tumeweza kudhihirisha moja tu (kama ilivyotajwa) kwenye vitabu vya hadithi



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 115 10/20/2015 4:32:06 PM

sa, anapaswa kuswali swala ya rakaa mbili, amhimidi Mwenyezi Mungu halafu asome dua ifuatayo:

اللهمّ إني أُريد أن أتزوج ، اللهمّ فاقدر لي من النساء أعفهنَّ فرجا ، وأحفظهنَّ لي في نفسها وفي مالي، وأوسعهنَّ رزقا ، وأعظمهنَّ بركة ، وأقدر لي منها ولدا طيبا تجعله خلفا صالحا في حياتي وبعد موتي

"Ewe Mwenyezi Mungu, ninatamani kufunga ndoa, kwa hiyo niwezeshe kumpata mwanamke miongoni mwa wale wenye kuhifadhi zaidi tupu zao, na mwenye kuilinda nafsi yake zaidi kwa ajili yangu, mwenye riziki pana zaidi kwa ajili yangu, na mwenye baraka zaidi kwa ajili yangu na mali yangu. Na niwezeshe kupata kiumbe mwema katika maisha yangu kutoka kwake (mwanamke huyo), utakayemfanya mtoto mwema kwa ajili yangu katika maisha yangu na baada ya kifo changu."[60]

**ANGALIZO:** Pamoja na kwamba maneno ya dua yanalengwa kusomwa na wanamume, wanawake pia wanaweza kusoma dua hii, baada ya kubadili maneno kwa namna inayostahili."[61]

**2.** Dua nyingine yoyote kwa ajili ya kutimiziwa haja pia inaweza kusomwa, kama vile swala ya rakaa mbili inayofuatiwa na kuekezea maombi yako. Ni muhimu kukumbuka kwamba kusoma dua zenyewe sio lengo pekee, bali ni njia ya kufikia lengo

[60] *Haliyatul Muttaqiin*, Jz. 4, sehemu ya 3, uk. 108

[61] Imethibitishwa na mwanazuoni Qum.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 116 10/20/2015 4:32:06 PM

kuu zaidi, nalo ni kujua na kujikurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu na kutambua kwamba sisi tunamtegemea Yeye kwa ukamilifu.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 117 10/20/2015 4:32:06 PM

# SURA YA 11

# KITU GANI KIFUATACHO?

## KUENDELEA MBELE

Endapo upande mmoja au pande zote mbili zinahisi kwamba mambo hayaendi sawasawa, na mchukuano hauonekani kufaa, basi kwa kawaida wazazi au mshenga watawajulisha watu wa muhimu na wa lazima.

Kama pande zote mbili zinaridhika kwamba mlingano wa wachumba watarajiwa unafaa, basi posa rasmi inapelekwa.

## POSA

**Nani Anayetoa Posa?**

Kwa kawaida katika tamaduni nyingi, ni mwanamume ndiye anayemposa mwanamke, ama afanye hivyo yeye mwenyewe moja kwa moja, au kwa njia ya kupitia kwenye familia au kwa mshenga.

Hata hivyo, hili halina msingi wa lazima katika Uislamu. Kama ambavyo imeelezewa kwenye sura zilizotangulia, ilikuwa ni Bibi Khadija (a.s.) ndiye aliyepeleka posa rasmi kupitia kwa Hazrat Abu Talib (a.s.), ambaye baada ya hapo alizungumza na Mtume (s.a.w.w.) na kwa njia hii jambo hili lilikamilishwa.

Kwa hiyo, posa inaweza na inapaswa kuanzishwa na upande wowote wenye kupenda kufanya hivyo, mwanamume au mwanamke.

**Unaweza Kumposa Nani?**[62]

Mbali na wanawake waliotajwa kwenye sura ya 3 ambao mtu anakatazwa kuwaoa, mwanamume anaweza kumposa mwanamke yeyote ambaye ni kapera (hana mume). Hata hivyo, posa haifai kwa mwanamke ambaye yupo kwenye muda wake wa eda kwa talaka ambayo inaweza kubatilishwa (talaka iliyoanzishwa na mume). Imekatazwa, ni haramu kumposa moja kwa moja au kwa mzunguko kabla ya kuisha kwa muda wake wa eda. Wanandoa ambao wametalikiana katika kadhia kama hii, wanaweza kuamua kubatilisha talaka yao wakati wa kipindi cha eda.

**ANGALIZO:** Mtalakiwa ambaye hajakamilisha uhusiano wa kindoa na mumewe hawi na muda wowote wa kungojea na anaweza kuolewa mara tu baada ya kutalikiwa kwake.[63]

Kwa taarifa za kina zaidi juu ya nyakati za kungojea (Eda) baada ya talaka, tafadhali rejea kwa Mujtahid wako.

[62] http/www.jaffari.org/resources/al-furqan/Al-furqan%201-8%2025%20May06%20 PROPOOSAL%20AND%20ENGAGEMENT.ptf

[63] *Islamic Laws* (Sheria za Kislamu) Kwa mujibu wa Fatwa ya Ayatullah al-Uzma Sayyid Ali al-Husaini as-Sistani, World Federation, London, 1994, Kanuni ya 2520



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 119 10/20/2015 4:32:06 PM

# SURA YA 12

# KIPINDI CHA UCHUMBA

## BAADA YA UAMUZI KUFANYWA

"Kwa sababu ya mazingira fulani, mchumba wangu na familia yake hawakuweza kututembelea kuja kufanya sherehe ya kurasmisha uchumba "kimila." Miezi kadhaa baada ya tangazo, mchumba wangu alikuwa arejee kwenda chuoni - alikuwa na saa 6 za mpito kwenye jiji nililokuwa ninaishi. Nilikutana naye uwanja wa ndege na tuliweza kuwa pamoja kwa muda fulani; hapo ndipo aliponipa pete yangu ya uchumba. Sio ile sherehe ya kufunga uchumba ya "kimila" kama ilivyo kawaida, lakini kwangu mimi ilikuwa sawa kabisa!" - **Mwanamke, Marekani (USA)**

Mara uamuzi ukishafanywa wa kuendelea mbele kwa mchukuano huo, kwa kawaida kufunga uchumba kutatokea. Hiki ni kipindi cha baada ya posa kukubaliwa, lakini kabla ya sherehe halisi za harusi.

Ni muhimu kutahadhari kwamba uchumba (bila ya mkataba uliotajwa hapo chini) hautambuliwi katika Sheria ya Kiislamu. Ni makubaliano ya kuoana, lakini sio makubaliano yenye kifungo na yanaweza kuvunjwa kwa sababu au bila sababu.

Mkataba wa ndoa ya muda (Mut`a), au wakati mwingine hata mkataba wa ndoa ya kudumu (Nikah), kwa kawaida hutamkwa



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 120 10/20/2015 4:32:06 PM

wakati wa kipindi cha uchumba. Hii huwapa wahusika fursa ya kuweza kujuana vizuri zaidi, bila ya kuvuka mipaka na kuingia ndani ya vitendo vilivyokatazwa. Ni baada tu ya Ndoa ya muda (Mut`a) au Ndoa ya daima kusomwa ndipo wachumba wanaweza kuzungumza kwa uhuru, wanaweza kukaa mahali pa peke yao, kushikana mikono, kugusana, kukumbatiana, kubusiana, na kadhalika. Mikataba hii itaelezewa kwa kina zaidi baadaye katika Sura ya 16.

Mara nyingi, sherehe ya kurasmisha uchumba huwa zinafanyika. Hii si desturi ya Kislamu, lakini alimuradi sheria za Kislamu zinafuatwa, hakuna tatizo. Hata hivyo, jaribu kufanya sherehe hiyo isivuke mipaka, na uhifadhi nderemo za furaha kwa ajili ya harusi! Zaidi ya hayo, sherehe ndogo nyepesi na kipindi kifupi cha uchumba vitarahisisha mambo endapo moja au pande zote mbili zinabadili nia na kuvunja uchumba. Kwa kweli, Mtume (s.a.w.w.) amekwenda mbali zaidi na kusema: "Tangazeni ndoa, lakini ficheni uchumba."[64]

## Kwa Nini Pawepo na Kipindi Cha Uchumba?

Kwa kutegemea uzoefu na uchunguzi wa mambo, tunapendekeza kwamba pawepo na muda kati ya kukubaliwa kwa posa na sherehe za harusi kwa sababu zifuatazo:

**1.** Sababu muhimu sana ni kumruhusu mvulana na msichana kujuana na kuwekana wao wenyewe katika hali ya usawa na kuzoeana, na kuimarisha fungamano lililojengwa wakati wa mchakato wa uchaguzi. Kipindi hiki pia huruhusu kuzatiti na kuimarisha mapenzi baina ya wawili hao.

**2.** Kipindi hiki huruhusu pande zote mbili kujitayarisha, kwa sherehe ya harusi na kwa ajili ya ndoa ya muda mrefu. Mata-

[64] *Kanz al-Ummal*, hadithi ya. 445362



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 121 10/20/2015 4:32:06 PM

yarisho haya ni ya kiakili, kimwili, kiroho na kiuchumi na ni sehemu muhimu ya matayarisho kwa ajili ya ndoa yenye mafanikio.

**3.** Pia ni kipindi kinachoruhusu wazazi na familia za wachumba kufahamiana na kuzoeana na kujitayarisha kwa ajili ya kipindi cha mpito cha watoto wao kuifanya safari hii ya kuelekea kwenye ndoa na kujitegemea.

**4.** Wakati mwingine vipindi vya uchumba ni vya kumruhusu mmojawapo au wachumba wote kumaliza masomo yao au majukumu mengineyo kabla ya ndoa.

### Kipindi cha Uchumba Kidumu kwa Muda Gani?

Pamoja na kwamba hakuna muda maalum ambao umewekwa kwa ajili ya uchumba, tunapendekeza kwamba muda unaofaa ni miezi sita hadi tisa. Huu muda hasa wa kipindi cha kawaida miongoni mwa uchumba unaofanyika leo hii.

### Katika Kipindi cha Uchumba

Mara nyingi hufanywa utani kuhusu kwamba kipindi cha uchumba ndio sehemu nzuri sana ya maisha ya ndoa! Pamoja na kwamba usemi huo si lazima uwe wa kweli, kwa kweli hicho ni kipindi kitamu sana kwani hapo ndipo wewe na mchumba wako mnapoanza kujuana kikweli hasa na kutayarisha mazingira ya maisha ya ndoa.

Yapo mambo fulani ambayo unaweza kufanya kuimarisha mchakato huu na kukusaidia humo njiani, pamoja na kwamba inapaswa kusisitizwa kwamba mnatakiwa kuwa na wastani na msije mkakuza mambo kwa lengo la kuinua kiwango cha matumaini kuwa juu sana. Pia inahimizwa kwamba mazoezi haya yanapaswa kuendelezwa baada kuoana. Nayo ni:



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 122 10/20/2015 4:32:06 PM

1. Kuthamini na kuheshimu maoni na hisia za kila mmoja wenu
2. Badilishaneni zawadi
3. Andikianeni barua za mapenzi (hata kama mnaishi katika jiji moja!)
4. Tembeleaneni, zungumzeni kwenye simu na barua pepe
5. Tokeni mkatembee pamoja (kwa ruhusa ya wazazi)
6. Mshiriki kwenye shughuli za kidini pamoja
7. Mjielimishe juu ya ndoa na masuala yahusuyo wazazi, kwa kushiriki pamoja kwenye semina za uchumba/ndoa, au kusoma vitabu juu ya mahusiano.[65]

**Urafiki wa Ndani**

Kama ambavyo imetamkwa hapo juu, kama mikataba (ya Mut`a au Nikah) imekwishasomwa, basi wao ni halali kwa kila mmoja wao, na urafiki wa ndani sana ni jambo la muhimu katika kujenga mafungamano yenu wakati wa kipindi hiki.

Neno la ushauri kwa wanamume wakati wa kipindi hiki ni kuwa wapole na si kuwa wenye mabavu sana katika mambo, kwani kwa kawaida huchukua muda mrefu zaidi kwa wanawake kuwa watulivu kimaumbile kwa wachumba zao.

Neno la ushauri kwa wanawake wakati wa kipindi hiki ni kuwa wazi, na sio kujidai kuwa na heshima sana. Mawasiliano ya wazi baina ya wachumba ni muhimu wakati wa kipindi hiki, kwani ndio yenye uwezo wa kuamua kila mazingira ipasavyo. Pia wachumba bado wanapaswa kuzingatia staha, heshima na maarifa ya kawaida hususani kwenye sehemu za hadhara ambapo mtu anaweza kujisahau.

[65] Orodha ya vitabu vinavyopendekezwa ipo kwenye faharisi.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 123 10/20/2015 4:32:06 PM

Kama angalizo la mwisho, furahia muda huu na kipindi hiki maalum, lakini acheni vipengele vilivyohifadhiwa hadi siku ya harusi. Ni muhimu sana kwamba unaheshimu uaminifu walioweka wazazi wako juu yako, na uzingatie masharti yoyote yale ambayo wanaweza kuwa wameyaweka, vilevile na shuruti ambazo unaweza kuwa umeziweka juu ya Mut`a, kwani masharti haya hayawezi kuvunjwa; haya yako pale kukulindeni nyinyi kama wachumba. Endapo mipaka kuhusu uhusiano wa kimaumbile inakiukwa, inaweza pia kuwa ni jambo la kufadhaisha na kusumbua sana endapo uchumba utavunjika.

**Mawasiliano:**

Wakati mwingine, katika kipindi cha uchumba, wachumba huwa wana hamu kubwa ya kuvutiana wao kwa wao au wanakuwa na wasi wasi wanaweza wakafanya jambo kwa makosa wakidhani wako kwenye 'tabia njema.' Ingawaje hili ni kawaida kwa kiwango fulani, kama ikizidi sana kiasi kwamba unajaribu kuficha athari hasi zote au mihemko hata kwa mambo madogo, basi hii inaweza kwenda kinyume cha matarajio na kulipuka mahali fulani mbele zaidi kwenye uelekeo.

Ufumbuzi katika kuzuia hili, na pia kuanza kushughulika katika uhusiano bora zaidi kiasi cha uwezekano baina yenu, ni kujenga mbinu nzuri zaidi za mawasiliano baina yenu. Hii inajumuisha kuwa wawazi katika kuzungumza kuhusu mambo ambayo yanaweza yakajitokeza ambayo huna raha nayo, ambapo unajaribu kubakia mwenye busara na mtulivu. Iweke akili yako wazi na jaribu kuwa muelewa juu ya nini kinachoweza kuwa kinamfika mwenzako, na usiwe mtu wa kujitetea pale masuala yanapoibuliwa. Wanamume na wanawake wana mitindo inayotofautiana ya mawasiliano na uchumba ndiyo mwanzo tu wa kugundua hili.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 124 10/20/2015 4:32:06 PM

“Wakati wa uchumba wetu, mume wangu na mimi tulikuwa na mijadala kadhaa juu ya jinsi tutakavyoshughulikia hali ambazo zingeweza kutokeza wakati wa ndoa yetu. Niliona mazungumzo haya ya mapema yalikuwa na manufaa sana kwani yalituruhusu sisi kutarajia hali kabla ya kuwa katikati ya hali hizo (wakati hisia zikiwa juu na kuathirika kukalazimisha maamuzi.) na kukubaliana juu ya taratibu za wazi na za pamoja zinazokubalika za kukabiliana na changamoto ambazo zingejitokeza. Kwa kuwa haiwezekani kuishi kwenye mazingira ya familia yoyote iliyopanuka bila ya kukabiliwa na migongano au kutofautiana kwa namna moja au nyingine, mojawapo ya mijadala kama huo tuliyofanya ni juu ya utaratibu gani ungekuwa bora kutumia kama mmoja wetu angejikuta kwenye mgongano na wazazi au watu wa familia ya mwenzake.

Baadaye katika ndoa yangu hali kama hiyo ilipojitokeza, niliona kwamba kama wanandoa hatukushtukizwa - lakini badala yake tuliweza kuangalia nyuma kwenye mazungumzo yetu wakati wa uchumba na kujaribu kutekeleza zile taratibu bora zinazofaa tulizokwisha kuzungumzia, badala ya kujibu moja kwa moja kwa kutegemea hisia za hamasa, mahitaji, na uathirikaji unaoweza kuwepo. Pia sisi wawili tulizungumza kuhusu hali ya mazingira mengine ambayo yangejitokeza ndani ya ndoa yetu - kama vile yeye mume wangu kusafiri kibiashara mara kwa mara au mimi kufanya kazi kama mtaalamu – na haya yalituruhusu sisi kuzungumza kwa busara sana kuhusu changamoto ambazo zingejitokeza, mahitaji na matarajio yale ambayo tulikuwa nayo sote wawili (pamoja na familia zetu), na maafikiano ambayo tungeweza kukubaliana.” **Mwanamke, Afrika**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 125 10/20/2015 4:32:06 PM

**Kumtumia Msiri Wako:**

Kuwa na msiri kama ilivyotamkwa ndani ya Sura ya 5 ni muhimu sana hususani katika hatua hii; anaweza kuwa na wewe na kuchangia hisia zako pamoja naye, mchangamshe mawazo yenu kwa pamoja na kuzungumzia jambo lolote mtakalopenda kulizungumzia.

Ambapo wazazi wanaweza kuwa wang`amuzi sana, lakini pia huwa na muelekeo wa kuwapenda kupita kiasi. Kuwapa kuchangia mabishano na huzuni yenu zote pamoja nao, kunaweza kuwaathiri sana, hata baada ya masuala yale yale ambayo yanaweza kuwa nyinyi mmeyashughulikia tayari na kuyasahau.

**Je, Nimefanya Uamuzi Sahihi?**

Ni muhimu kuzingatia hapa kwamba ni kawaida kabisa kuendelea kuwa bado na shaka kuhusu iwapo kama uamuzi sahihi umefanywa katika kuchagua mchumba wako; kwa hakika, ndiyo maana kipindi cha uchumba ni wakati muhimu sana kwa wachumba kuzoeana zaidi; kipindi cha uchumba kinaweza ama kuimarisha au kuvunja uchumba.

**Dalili za Kawaida:**

Kwa mara nyingine tena, sehemu hii inataja dalili za kawaida ambazo zinaonyesha kama akili na nafsi zipo katika mlingano au hapana katika kipindi cha uchumba.

# ANGALIZO:

Kama ambavyo imeelezwa hapo juu, ni muhimu sana kuzingatia kwamba mambo yafuatayo hayawabani; yenyewe ni muongozo tu ulioegemezwa kwenye mkusanyiko wa uzoefu na hivyo yanaweza kuwahusu kidogo au yasiwahusu hata kidogo.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 126 10/20/2015 4:32:07 PM

## 1. Vita Vya Ndani na Akili (na hisia Zisizotabirika)

Ingawaje hali hii inaweza kuwepo wakati wa hatua ya uchunguzi pia, kama hisia zako bado hazitabiriki wakati wa kipindi cha uchumba hivyo kwamba wakati wote zinabadilika kwa kupanda na kushuka, (yaani siku moja utajihisi umefurahi sana na umeridhika kwamba mchumba uliyempata ndiye hasa kwa ajili yako, na siku nyingine unajihisi mambo hayako sawa, yako vibaya na mchumba huyo siye hasa wa namna yako), basi hii inaweza kuwa ni dalili ya wazi kuwa akili haijawiana na nafsi. Akili inakuthibitishia kwamba kila kitu ni sawa na kukupatia sababu kwa nini mambo yapo sawa, lakini nafsi inajua kwa ndani sana kwamba si lazima mambo yawe sahihi. Endapo unakabiliwa na aina hii ya mzunguko wa furaha/huzuni, hali kama hii ni tete na ni mapigano ambayo hayaelekei kwisha hata baada ya ndoa. Kwa hiyo lazima urudi nyuma na utathmini kila kitu upya.

> "Wakati nikiwa nimesikia kutoka kwa wengi kabla yangu kwamba kipindi cha uchumba ndio 'wakati mzuri sana katika maisha yako', mimi nilikuwa ninapita kwenye mapambano makubwa sana ya ndani kabisa ya nafsi. Wakati kulikuwepo na siku ambapo mambo yalikuwa yanakwenda vizuri, palikuwepo pia na siku kama hizo ambapo nilikuwa najihisi nimepotea na kuchanganyikiwa, na sote tulijua kwamba kuna jambo ambalo halijawa sawa kabisa. Tulizungumza kuhusu suala hilo. Sote wawili tulikubaliana kwamba hatukuwa na amani na mtiririko wa hisia haukuwa mzuri kwetu sote. Tulizidi kuendelea kujipa moyo lakini nafuu tuliyoipata pale tulipoamua kuvunja mpango wote ndio iliyotufanya tutambue kwamba tulikuwa hatupangiwi kuwa wapenzi. Pia ilitufanya sote tutambue kwamba kuachana si kila mara kuwe kwa ukali kwani sote wawili tulikuwa na imani na hisia zetu na tulipata uungwaji mkono mzuri sana kutoka kwenye familia zetu, na kwa hakika ulitusaidia sana.!" **Mwanamume, Uingereza**

## 2. Kuwa Peke Yenu na Kimya Baina Yenu

Katika hali nyingi, kama baada ya kuchumbiana katika kipindi cha muda fulani na kimya baina yenu bado kinawanyima raha na kila mara mnataka kuwa karibu na watu wengine ili mazingira yasiwe ya wasiwasi baina yenu wawili, lazima mchukue hatua ya kurudi nyuma na kufanya uchambuzi wa mazingira wote pamoja ili muweze kuona kama kila kitu kiko sawa. Na hakuna jambo ambalo ni baya kabisa. Kimya na hali ya mazingira baina ya wachumba wawili wenye furaha yanatakiwa kuwa ya raha, kama kimya baina ya marafiki wawili wazuri ambao hawahisi ulazima wa wakati wote kusema kitu.

## 3. Mawasiliano ya Mara kwa mara:

Endapo kimya kisicho na raha au sababu zingine zinaelekeza kupungua kwa mawasiliano ya mara kwa mara baina yenu na kama mmoja wenu au wote mnaendelea kuja na visingizio kwa kukosekana kwa mawasiliano, mnahitaji kujua kwamba hali hiyo si ya kawaida, hususani katika zama hizi za intaneti ambapo kuandika barua-pepe huchukua sekunde chache tu. Kwa hiyo, mnahitaji kurudi nyuma hatua moja na mtathmini kama visingizio hivyo ni vya kweli au hapana au kama kuna mgongano katika mitindo na matarajio. Kwani wale walio na uhusiano wa masafa marefu, inaweza kuwa kupigiana simu mara moja kila wiki inatosha; katika mifano mingi ambapo mambo yanakwenda vizuri, ishara nzuri ni kwamba wote wawili hamuwezi kungojea simu ya wiki ijayo.

## 4. Muda Mnapokuwa Mbalimbali:

Kwa misingi kwamba Mut`a/Nikah inapokuwa imesomwa, mara mnapokuwa mbalimbali baada ya kuzungumza au kukutana, mnajihisi vipi? Mnakuwa na shauku kubwa sana ya kuzungumza au ku-

kutana tena? Kama ni hivyo basi hii ni dalili nzuri sana kwamba mambo yako shwari baina yenu nyote wawili.

## 5. Kutumia Muda na Wazazi wa Upande wa Pili:

Mara nyingi watu wanakisia vibaya ule umuhimu wa kutumia muda mrefu wa kutosha na wazazi wa mchumba wake. Ingawaje mwanzoni hii inaweza kutia wasiwasi kidogo, manufaa ya kutumia muda na wazazi wa mchumba wako ni pamoja na:

### a. Kupata Maoni Chini kwa chini ya Familia

Nani anayetawala ndani ya nyumba? Je, uhusiano baina ya wazazi ni wa kawaida, wanaokaribiana, wanaopendana au wenye mtafaruku, kwani hili litakuwa na uzito sana katika uhusiano wenu, kulingana na nini mtoto ataleta kwenye ndoa na matarajio yake mchumba baada ya kufunga ndoa.

### b. Kuwasimulia Mambo yao

Kama unaweza kuwasimulia wazazi wa mchumba wako, kwa mfano maadili wanayoshikilia, mambo wanayoyaamini, na kadhalika na kama mtoto na wazazi wana fungamano imara, basi ipo bahati nzuri kwamba wewe utamfurahia mtu ambaye unafunga ndoa naye.

## 6. Mabishano

Muda wa uchumba ni wakati ambapo mabishano yanaweza yasitokee, hususani kama ni uhusiano wa masafa marefu, na kwa hiyo kama mabishano yanatokea, mnahitaji kurudi nyuma na kutathmini kwa nini hali hiyo inatokea. Inawezekana ikawa ni jambo ambalo sio lazima kuwa na wasiwasi nalo, kwa kweli, linaweza kuwa hata na manufaa ya kuona jinsi gani nyinyi kama wachumba mnaweza kush-



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 129 10/20/2015 4:32:07 PM

ughulikia tofauti zenu, na jinsi mnavyoonyesha hisia zenu wakati wa mfadhaiko.

Hata hivyo, mnahitaji tu kufikiria kwa nini mabishano yanatokea, chimbuko la mabishano hayo ni nini, na kama lipo tatizo la msingi au hapana. Baadhi ya sababu zinazowezekana za mabishano zinaweza kuwa ni kutokana na tofauti za mitindo ya mawasiliano baina ya wanawake na wanamume, ugeni wa kushirikiana katika kila kitu, ukosefu wa uhuru ikilinganishwa na wakati wa ukapera, kuhamia ghafla kwenye umwandani ambako baadhi ya wasichana wanaweza kukosa raha nako mwanzoni, homoni mahali pote hapo, matarajio ya ujumla ikilinganishwa na hali halisi, na mambo kama hayo.

**Mabishano kwa kawaida huwa ya aina mbili:**

**a. Miongoni mwenu nyinyi wawili:**

Ambapo mabishano hutokea na ni ya kawaida, endapo mnaona kwamba polepole mmeanza kubishana na kushindwa kukubaliana zaidi na zaidi, na kama ni mwelekeo unaoendelea, hali hii inahitaji kujadiliwa na kuifanyia kazi.

**b. Mkiwa na familia zenu husika:**

Cha kusikitisha, matatizo mengine yanaweza kutokea kwa sababu ya familia; wakati ambapo wenza hao wanaweza kuwa wanaelewana vizuri lakini, ama familia za pande zote mbili hazielewani, au mmoja wa wenza hao haelewani na familia ya mwenzake. Hali labda inawezekana ikasababishwa na masuala ya binafsi, masharti ambayo yamewekwa kwenye upande mwingine au matarajio yasiyotegemewa kutoka upande mwingine.

"Wakati wa hatua ya kupanga sherehe za harusi yetu, tulikuwa na tatizo la kupata mahali pa kufanyia sherehe hizo, kwa sababu ya kukosekana ukumbi ulioandaliwa mwanzoni. Kwa bahati mbaya, hali hii iliingia kwenye mambo makubwa baina ya familia mbili kuhusiana na gharama za ukumbi, ukaribu, nafasi, vifaa na masuala mengine yanayohusiana. Hali hii ilisababisha mimi na mchumba wangu kupita huku na kule kujaribu kutafuta mpango muafaka ili kuridhisha ndoto za wazazi wetu. Bila hata kusema, ni wazi kwamba, haya yote yalitumika tu kuvuruga uhusiano kati yetu, karibu kabisa na wakati wa harusi. Hata hivyo, tulikuwa bado tunajua wote kwamba tulikuwa tunafaana wenyewe, katika kipindi hiki cha shinikizo kubwa, tulijilazimisha kuangalia mbele zaidi ya siku ya harusi na kukumbuka hasa kwa nini tulikuwa tunaoana. Siku ya harusi ni siku nzuri sana kwenu nyinyi na familia zenu, lakini si lolote ikilinganishwa na muda wa maisha ya ndoa ambao mnajifunga nyinyi wenyewe humo, kwa hiyo, ushauri wangu ni kukumbuka kwamba hiyo ndoa ndiyo lengo lenu." – **Mwanamke, Uingereza**

Kama ukiona kwamba una mabishano endelevu na wazazi wako mwenyewe na familia kwa sababu ya mwenzako, hii si dalili nzuri kwa mambo yanayokuja baadaye, hususani ambapo kwa kawaida kipindi cha uchumba huwa ndiyo wakati ambapo mabishano kama hayo kwa nadra sana hutokea. Suala hili huwa linatakiwa kushughulikiwa wakati wa hatua ya uchumba kwa sababu upo uwezekano mkubwa baadaye likawa kubwa na baya zaidi. Hatimaye, linaweza kufika mahali ambapo mvulana/msichana atalazimishwa kuchagua kati ya ama awe na mchumba wake au familia yake na matokeo yake ni matatizo makubwa na maumivu ya moyo.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 131 10/20/2015 4:32:07 PM

Hata hivyo, panaweza kuwa na masuala madogo ya mgongano, mathalani wakati wa kupanga na kutayarisha sherehe za harusi. Kwa kawaida hili ni eneo ambapo panaweza kuwa na mambo ya kipekee, hususani pale ambapo familia mbili zinatoka kwenye asili tofauti, pana uhakika wa kuwepo mambo ya mgongano.

**Itakuwaje kama Mambo Hayaendi Sawa?**

Wakati mwingine inawezekana kwamba wachumba wanahisi kwamba mambo yamekwenda mbali mno kufikia kuivunja posa, na huwa na wasiwasi kwamba kila mtu wakati huo amekwishajua kuhusu uchumba huo, au wana wasiwasi kuhusu kwamba watu watafikiriaje. Hujiridhisha wenyewe kwamba mambo yatakuwa mazuri, na kwamba mapenzi yatafuata na kwa hiyo wakamezea shaka zao na wakaoana. Hata hivyo, hatimaye huchoka kujifanya wanapendana kumbe hawapendani na lazima uhusiano utaharibika na kuingia kwenye machungu na mabishano, na inawezekana kutalikiana. Wakati ambapo kuvunja uchumba ni vigumu, lakini haina budi iwe hivyo ili kuepuka matatizo ya baadaye, hususani kama tamko la ndoa litakuwa limekwishasomwa, itakuwa ni vibaya zaidi kwa mambo kuishia katika matatizo makubwa mwishoni kabisa mwa mlolongo huo; matokeo yake yatakuwa mabaya na ya kufika mbali zaidi, hususani kama watoto watahusishwa.

Endapo uamuzi wa kuvunja uchumba unafanywa, pande zote mbili zinatakiwa kujaribu kutekeleza uamuzi huo kwa amani na kiheshima kadiri iwezekanavyo, kuombana msamaha pale ambapo ni muhimu. Pale ambapo ni lazima pawe na hisia hasi zaidi katika baadhi ya mambo kuliko kwenye mengine, ufumbuzi si kushutumiana au kufichua mambo yasiyo na maana kuhusu upande mwingine, lakini badala yake kuficha dosari zao na kufichua kiasi kidogo sana cha taarifa kwa watu kuhusu kuvunjika kwa mpango huo.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 132 10/20/2015 4:32:07 PM

Kwa kigezo cha kusonga mbele baada ya kuvunjika kwa uchumba, kwa namna nyingi kinaweza kuwa sawasawa na kule kusonga mbele baada ya kuvunjika kwa ndoa. Tafadhali angalia Sura ya 15 kwa taarifa zaidi.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 133 10/20/2015 4:32:07 PM

# SURA YA 13

# KANUNI MUHIMU ZA FIQHI: SEHEMU YA 2

## KIPINDI CHA UCHUMBA KANUNI ZA KIPINDI CHA UCHUMBA

**Kama Hakuna Kanuni ya ndoa Iliyosomwa:** [66]

Mwanamume na mwanamke wanakuwa sio maharim kwa kila mmojawao na hakuna tofauti baina yao na wengine ambao si maharim wao. Kwa hiyo, kutazamana kwa nia ya ashki, kushikana mikono au namna yoyote ya kugusana kimwili, kukaa nyinyi wawili tu mahali pa faragha, kutozingatia kuvaa hijabu na nguo za kutosha mbele yenu, kuwa katika mikusanyiko na kuchanganyikana kwa namna ile ambayo mke na mume ni kawaida kufanyiana, na kwa ufupi, uhusiano wa aina yoyote uliokatazwa baina ya watu wawili ambao sio mahrimu utatumika hapa na kwa hiyo wote wawili lazima wajizuie kufanya mambo haya.

**Endapo tamko la ndoa ya muda (*Mut`a*) limesomwa:** [67]

Madhali hili litakuwa limetokea kwa rukhusa ya mlezi wa mwanamke, mwanamume na mwanamke sasa ni halali (*maharim)* kwa kila mmoja wao. Hata hivyo, masharti yoyote ambayo yamewekwa wakati wa kutamkwa Mut`a lazima yafuatwe.

[66] Mfumo wa Maadili kwa Waislamu Wanamume na Wanawake, Kanuni ya 243

[67] Mfumo wa Maadili kwa Waislamu Wanamume na Wanawake, Kanuni ya 244



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 134 10/20/2015 4:32:07 PM

**Endapo tamko la ndoa ya kudumu (Nikah) limesomwa:**[68]

Katika kadhia hii, mwanamume na mwanamke ni halali kwa kila mmoja wao.

Endapo wachumba hao wanataka kufunga ndoa ya kudumu kabla ya kipindi cha ndoa ya Mut`a hakijaisha, basi mwanamume lazima itie nia ya 'kufuta' kipindi cha muda uliobakia kwa mwanamke ambapo inakuwa ndiyo mwisho wa Mut`a. Kama tamko la ndoa ya kudumu (Nikah) litasomwa bila ya kufikia mwisho rasmi wa ndoa ya Mut`a basi ndoa ya kudumu itabatilika.

**Uchumba Uliovunjika** [69]

Kama uchumba ukivunjika, ni lazima kuzingatia yafuatayo:

- Inapotokea ndoa ya muda imefungwa, halafu hata kama baada ya mwisho wa kipindi chake ndoa ya kudumu haijafungwa, mama wa msichana atakuwa maharim wa mwanamume huyo kwa muda wote atakaokuwa hai. [70]
- Pande zote mbili zina haki ya kutaka kurudishiwa zawadi walizokwisha kupeana:

1. Endapo zawadi zilikuwa ni zenye kuweza kuharibika (mfano, peremende), basi hakuna msingi wa kutaka kurudishiwa, zenyewe au thamani yake.
2. Endapo zawadi zilikuwa si zenye kuharibika (mfano, fedha au vito), basi upo uwezekano wa aina mbili;

    a. Kama zawadi hiyo bado ipo, basi irudishwe.

---

[68] Mfumo wa Maadili kwa Waislamu Wanamume na Wanawake, Kanuni ya 247

[69] Imechukuliwa kutoka kwenye Vielekezo (Pointers) - mwandishi Sayyid Muhammad Rizvi http:/ /www.duas.org/matri1.htm

[70] Mfumo wa Maadili kwa Waislamu Wanamume na Wanawake, Kanuni ya 246



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 135 10/20/2015 4:32:07 PM

b. Kama haipo tena, basi:

c. Kama haipo kwa sababu ya uzembe, basi lipa thamani yake

d. Kama si kwa kosa la mtu yeyote, basi hakuna malipo yoyote.

Hata hivyo, kufuatana na Sheria ya Kislamu, zawadi zilizotolewa kwa mtu unayehusiana naye kwa damu haziwezi kudaiwa kurudishwa (uhusiano wa damu maana yake ni uhusiano wa kibaiolojia ambao ni kinyume na uhusiano kupitia ndoa). Kwa hiyo, mathalani, kama uchumba ni baina ya mabinamu na halafu ukavunjika, wahusika hawawezi kudai kurudishiana zawadi walizopeana.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 136 10/20/2015 4:32:07 PM

# SURA YA 14

# ITAKUWAJE KAMA HUWEZI KUMPATA HUYO ANAYEFAA?

## KWA KUWA NA IMANI

Kama umekuwa unatafuta na hujaweza kumpata yule aliye sahihi kwako, usikate tamaa. Endelea kujaribu na Mwenyezi Mungu atakupatia kutoka kwenye neema zake zisizo na ukomo, na kukuongozea kwa mwenza wako wa maisha ya baadaye.

Wakati huohuo, ni muhimu kukumbuka yafuatayo hapa chini:

**1.** Bakia kuwa mwaminifu na usishawishike kukimbilia uovu, dhambi au uhusiano haramu wa ngono, Allah anasema ndani ya Qur`ani Tukufu:

وَلْيَسْتَعْفِفِ ٱلَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا حَتَّىٰ يُغْنِيَهُمُ ٱللَّهُ مِن فَضْلِهِۦ .....

**"Na wajizuilie na machafu wale wasiopata cha kuolea mpaka Mwenyezi Mungu awatosheleze katika fadhila Zake…" [24:33] 1**

**2.** Swala ya rakaa mbili ina nguvu ya kufaa sana kwa ajili ya kumzuia Shetani asikuathiri wewe. Imesimuliwa kutoka kwa Imam Ali (a.s.): "Mtu yeyote ambaye anamuona mwanamke na akakumbuka starehe ya jimai baada ya kumuona mwanamke huyo,

lazima aende kwa mke wake na kukidhi haja yake ya kujamiiana, kwa sababu kile alichonacho mwanamke huyo, mke wake anacho pia, na lazima usimpe shetani nafasi ndani ya moyo wako. Na kama mtu hana mke lazima aswali rakaa mbili, amtukuze Mwenyezi Mungu kwa wingi, na kumswalia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na lazima amwombe Mwenyezi Mungu ampe mwanamke muumini mzuri, mcha Mungu, na kwamba asitamani kufanya vitendo vilivyoharamishwa."

**3.** Ipo njia moja iliyo wazi kwa wale ambao, kwa sababu yoyote ile, hawawezi kuoa ndoa ya kudumu ni kutekeleza ndoa ya Mut`a ili kuweza kukidhi haja zake za kimaumbile kwa njia iliyo ruhusiwa kisheria:

..... وَأُحِلَّ لَكُم مَّا وَرَآءَ ذَٰلِكُمۡ أَن تَبۡتَغُواْ بِأَمۡوَٰلِكُم مُّحۡصِنِينَ غَيۡرَ مُسَٰفِحِينَۚ فَمَا ٱسۡتَمۡتَعۡتُم بِهِۦ مِنۡهُنَّ فَـَٔاتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ فَرِيضَةٗۚ وَلَا جُنَاحَ عَلَيۡكُمۡ فِيمَا تَرَٰضَيۡتُم بِهِۦ مِنۢ بَعۡدِ ٱلۡفَرِيضَةِۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمٗا ٢٤

**"…Na mmehalalishiwa wasiokuwa hao, kwamba muwatafute kwa mali yenu kwa kuoa bila ya kufanya zinaa. Ambao mumestarehe nao katika wao, basi wapeni mahari yao yaliyolazimu, wala si vibaya kwenu katika yale mliyoridhiana baada ya kutoa kile kilichowalazimu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima." (4:24)**

Kwa taarifa zaidi kuhusu Mut`a, tafadhali rejelea Sura ya 16.

# SURA YA 15

## KUCHAGUA MCHUMBA BAADA YA TALAKA KUENDELEA MBELE BAADA YA TALAKA

Katika kipindi baada ya talaka, fikira ya kuoa tena inaweza kuwa jambo lililopo mbali sana kwenye akili ya mtu. Hii si kwa sababu tu ya kushughulika na mambo mengi yaliyojitokeza kwenye ndoa iliyopita na kuvunjika kwake, lakini siku za usoni pia zinaweza kujazwa na wasiwasi na hofu. Hofu ya kuanza tena upya, hofu ya kukutana na watu na hofu ya kumjua mtu fulani kuanzia mwanzo kabisa wakati mwingine inaweza kumzidi mhusika, hususani kama ndoa iliyopita haikuwa na uzoefu mzuri, au talaka ilikuwa ya vurugu tupu. Kwa jumla, uwezekano wa kuoa tena unaweza kufikiriwa kuwa kama mzozo zaidi kuliko manufaa yake.

Hata hivyo, awamu hii itapita; kama ambavyo hisia hasi zitakuwa zinakufa, matamanio ya kuendelea na mipango ya ndoa yatatokeza, mbali na kuwepo hofu. Ni muhimu kukumbuka kwamba kila kitu hutokea kwa sababu na ni hapo tu kipindi hiki cha muda wako wa maisha kinapokuwa kimekwisha ndipo utambuzi unafanya mambo kuwa wazi zaidi. Upo usemi mashuhuri, “Jambo lisilokuua hukufanya tu uwe na nguvu zaidi;’ kwa kweli kama itakavyozungumziwa kwenye sehemu za mbele, zoezi zima litakuacha wewe ukiwa umejitambua zaidi na kujiandaa zaidi kwa ajili ya ndoa mnamo siku za usoni.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 139 10/20/2015 4:32:08 PM

Ni muhimu kukumbuka kwamba kutalikiana ni jambo linalo shika kasi kubwa sasa na hivyo linaathiri maoni ya watu kidogo tu kuliko ilivyokuwa, hususani kwenye miji mikubwa. Alhamdulillah, kuna fedheha chache zinazohusiana na talaka kuliko ilivyokuwa hapo zamani, na kwa hiyo hili linafanya hatua ya mtu kusonga mbele baada ya kutalikiana kuwa rahisi azaidi.

## Nianze Lini Kuanza Kukutana na Watu Tena?

Swali kubwa ambalo waliotalikiana hukutana nalo ni lini waanze kukutana na watu tena. Hili ni jambo ambalo sio wao tu ambao hujiuliza, lakini kutoka kwa wazazi na watu wengine wenye nia safi ambao wangependa kuwaona wanaendelea na maisha yao.

## Vipindi vya Eda ya Kislamu

Ni wajibu kuzingatia vipindi vya eda ambavyo vimewekwa na Sheria ya Kiislamu juu ya wanawake baada ya kutalikiwa. Pia ni muhimu kuzingatia kwamba mwanaume kukutana na mchumba mtarajiwa wakati wa mtengano wa eda yake, na kabla ya eda hiyo kwisha ni haramu katika Uislamu. Hii ni kwa sababu mtu aliye kwenye eda bado yu kwenye ndoa kisheria na wakati wote kunakuwepo na fursa ya wanandoa waliotengana kuweza kurejeana. Hii vilevile hutumika kwa wale ambao baada ya talaka rejea (Talaka iliyoanzishwa na mume), kwani wanandoa waliotalikiana, katika kadhia hii, wanaweza kuamua kutangua talaka yao ndani ya wakati wa kipindi cha eda.

Kwa mwanamke ambaye yupo kwenye kipindi cha Eda kwa sababu ya kufiwa na mume wake, ni karaha (*makruh*) kuzungumza na mtu kwa nia ya kutaka kuja kufunga ndoa. Hii pia ni hali ambayo inamkuta mwanamke ambaye amepewa talaka ambayo haitanguliki



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 140 10/20/2015 4:32:08 PM

(*Khula*: talaka iliyoanzishwa na mke), bila kujali kama wametengana kwa kipindi cha muda fulani kabla ya hapo au hapana.

Ni muhimu kukumbuka kwamba kipindi cha Eda ni kipindi kifupi tu, ambacho baada ya hapo hatua za ziada zinaweza kuchukuliwa.

**Utayari Kutoka Ndani ya Nafsi:**

Wakati mwingine familia zinaweza kutaka mtu kufunga ndoa tena, zaidi kuliko wahusika wenyewe wanavyotaka. Hii ni kwa sababu familia huhamasishwa na hisia za kutaka kumuona mtu wao anakuwa na furaha na kutulia tena. Wakati mwingine wahusika wanahisi wapo tayari, lakini wazazi na familia wanahisi wanapaswa kungojea.

Ni muhimu kutokuafiki shinikizo la nje, kwani unahitaji kuwa tayari wewe mwenyewe ndani ya nafsi yako. Jaribu kuyafanyia kazi masuala ya talaka na ukubaliane nayo kabla ya kuanza kukutana na watu kwani unaweza ukamkataa mtu kwa sababu tu umekutana na mtu mapema zaidi, na bado unayo kumbukumbu kuhusu uhusiano wa kwanza. Bila shaka unaweza ukawa tayari pale ambapo unaweza kukutana na mtu na kumuona kama mtu tu, bila kutoa taswira ya hali yako ya siku za nyuma na hisia zako kwake, yaani unaweza kutumia muda na mtu bila kulinganisha na kufananisha hali na maisha yaliyopita, mathalani, 'Mke wangu wa zamani alisema hivi hivi, ambavyo kwa hiyo lazima iwe na maana ya…….'

Usiharakishe mambo; haya sio mashindano ya kuona kama unaweza kuposa kabla ya mtalaka wako hajafunga uchumba tena. Wakati huohuo, usiliakhirishe jambo hilo kwa muda mrefu sana, usije ukaingiwa na woga na shaka. Unakuwa tayari unapotumia siku zako nyingi zaidi ukiwa unaangalia mbele badala ya kutazama nyuma.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 141 10/20/2015 4:32:08 PM

Pale ambapo ni muhimu kutokukubali shinikizo la nje, wakati huohuo usikubali ushauri wa wale wakupendao; kama familia yako inadhani kwamba bado hujawa tayari, jadili nao waziwazi kwa nini wanadhani bado hujawa tayari na uzishughulikie sababu zao, inawezekana wao wakawa sahihi. Na kinyume chake pia ni kweli pale ambapo wanaweza kufikiri kwamba upo tayari na hutaki kuharakisha mambo. Mazungumzo ya wazi na staha yatasaidia kudumisha upendo na mshikamano ndani ya familia.

Jambo la muhimu kuzingatia ni kwamba hakuna muundo wa muda maalum uliopangwa wa kufunga ndoa upya tena (zaidi ya muda wa Eda za Kislamu uliowekwa). Muda inaouchukua unatofautiana kwa kila mtu na mambo mengi huingiliana; haiba za watu, muda iliodumu ndoa ya zamani, sababu za kuvunjika kwa ndoa hiyo, namna jinsi kuachana kulivyotokea, na kadhalika. Mtu mmoja wao anaweza kuwa tayari kukutana na watu baada ya muda mfupi sana, mwingine anaweza kuchukua muda mrefu zaidi.

**Dalili za Kawaida:**

Zipo dalili za kawaida ambazo zinaashiria kwamba upo tayari kuendelea na kuanza kukutana na watu tena ukiwa na maoni ya kutaka kufunga ndoa tena. Hizi zinafanana sana na zile zilizoelezwa kwa muhtasari ndani ya Sura ya 2. Hizi ni pamoja na:

**1.** Silika

**2.** Shauku ya kujamiiana

**3.** Kutaka mwenzi

**4.** Kusumbuliwa na upweke.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 142 10/20/2015 4:32:08 PM

> “Baada ya kuvunjika kwa ndoa yangu ya kwanza, nilikaidi kwamba nisingeolewa tena. Si kwamba nilikuwa sitaki kuolewa tena - kwa sababu nilikuwa ninataka -lakini sikuhisi ningekuwa na nguvu ya kufanya hivyo tena, na kama ningeweza kuona nafsini mwangu kumwamini au kumpenda mtu fulani kwa mara ya pili. Pia nilijihisi kutokuwa salama kuhusu kuwa mtalaka, nikifikiria kwamba hakuna mtu mwenye kufaa kufikiriwa ambaye angeweza kuvutiwa na mimi. Lakini jinsi siku zilivyosonga mbele, ukweli wa kuwa peke yangu ukaniingia. Hakuna idadi ya marafiki au familia ambayo ingeweza kuziba mwanya huo, kwa hiyo watu walipoanza kunifuata wakiwa na shauku, nilianza kuhisi matumaini tena na nikaanza kulifikiria tena.” **– M wanamke, Uingereza**

**Mchakato ni Upi?**

Mchakato ni kama ule ule wa kwanza, njia ni zilezile - wazazi, wasuluhishaji na washenga. Hata hivyo, unaweza ukaona kwamba wakati huu mambo yanakuwa nje ya utaratibu zaidi; itifaki zinazohusika zinakuwa chache sana, na baadhi ya watalaka huona kwamba wazazi pia wanakuwa watulivu zaidi, mathalani katika kuwaruhusu wachumba watarajiwa kukutana sehemu za nje badala ya mvulana kwenda nyumbani kwa msichana kwanza, na kadhalika.

Kila hali ni tofauti: baadhi ya watu huona kwamba kuna mikutano michache zaidi iliyopangwa, na hutoa taarifa kwamba mikutano ilifutwa kwa notisi fupi. Kwa upande mwingine, wengine wametoa taarifa kwamba idadi ya watu wenye kuvutiwa kwa kweli iliongezeka! Kwa hiyo, ni muhimu kufanyia kila mazingira uamuzi wa peke yake.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 143 10/20/2015 4:32:08 PM

Washenga wachache wanakuwa na imani kubwa kwamba mtalaka anaweza tu kulinganishwa na mtalaka mwingine. Uwe na uhakika kuona iwapo kama hiyo ndio hali iliyopo miongoni mwa wasuluhishaji na washenga ambao unashughulika nao, ili uzuie hili lisijekuwa kizuizi kwenye mchakato wa kufunga ndoa tena.

## Unapaswa Kufunga Ndoa na Nani?

### Vigezo:

Unapotafuta mchumba baada ya kuwa kwenye ndoa kabla ya hapo, 'orodha' ya kile unachotafuta kwa kawaida hubadilika. Mchakato wa kuwepo kwenye ndoa na halafu kupita kwenye mpito wa talaka kwa kawaida humkomaza mtu, hufanya iwe wazi zaidi kuhusu ni nini anachokitaka, na, labda la muhimu zaidi, kile asichokitaka na ataona ugumu namna ya kukishughulikia katika ndoa ijayo.

Watalaka huelekea kuona kwamba ndoa ya mara ya pili inafikiriwa zaidi kuwa njia ya kufikia lengo badala ya lengo lenyewe. Inahusu zaidi kujenga mazingira mazuri yaliyojaa upendo kwa ajili yenu wenyewe na familia, kuanzisha maelewano na kutoshelezeka baina ya yenu na kuridhika katika sehemu hiyo ya maisha yenu, ili kukuwezesheni nyinyi kufanikiwa kwenye malengo yenu mengine, kama vile ukaribu zaidi kwa Mwenyezi Mungu.

> "Niliona ukweli kwamba kule mimi kutalikiwa kulikuwa kwa manufaa yangu. Nilikomaa zaidi, nilifikiria juu ya mambo makubwa zaidi, na ya busara zaidi kwa jumla katika maisha." – **Mwanamke, Uingereza.**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 144 10/20/2015 4:32:08 PM

**Kufunga Ndoa na Mtalaka mwingineo**:

Kufunga ndoa na mtalaka mwingine kunaweza kuwa na manufaa yake. Upo uwezekano wa kuwepo kukubaliana kukubwa na kuelewana baina ya watu hao wawili, ambako kwa dhahiri ni kifuta machungu. Hata hivyo, usijiwekee sharti la kukutana na mtalaka tu; katika baadhi ya kadhia, kama watu wote ni watalaka, hii inaweza kurudufu mizigo itakayoletwa kwenye uhusiano wao!

> "Mara ya pili wote wawili tulijiona tukiwa tunajiamini zaidi wakati wa mkutano wetu wa kwanza. Pengine hii ilikuwa kwa sababu ya ukubwa wa uzoefu wa maisha katika kipindi kifupi kama hicho, labda ilikuwa ni ule ukweli kwamba baina ya 'mkutano wa kwanza' katika mzunguko wa kwanza na 'mkutano wetu wa kwanza' baada ya kutalikiana, miaka mingi ilikuwa imepita na kwa jumla tumekuwa watu wazima tu, na wenye hekima zaidi." – **Mwanamke, Canada**

**Kufunga Ndoa na Mtu Asiye Mtalaka:**

Kama alivyotajwa hapo juu, kufunga ndoa na mtu ambaye si mtalaka inaweza kuwa na maana ya kwamba ninyi hamna mengi ya 'zamani' baina yenu ya kushughulikia. Hata hivyo, inawezekana wakati wote asielewe pale uliposimamia wewe. Kwa hiyo patahitajika mawasiliano makubwa zaidi na subira. Zingatia akilini hata hivyo, kwamba watu wanaokukabili wewe, kwa sifa walizonazo, tayari mawazo yao hayafungamani na upande wowote, ni wenye kuvumilia mawazo ya wengine na hawakuathiriwa sana na nembo na fedheha za kitamaduni.

"Baada ya kutalikiwa, niliamua kimya kimya kukutana na wale tu ambao nao pia ni watalaka, nikifikiria kwamba mtu ambaye hajaoa angekosa ukomavu katika uendeaji wake kwenye ndoa, matarajio, na maisha kwa ujumla. Pia sikutaka kuwa kwenye mazingira ambapo ule ukweli kwamba nilikuwa nilikwisha kuolewa kabla kutumiwa dhidi yangu katika uhusiano. Nilitaka kuolewa na mtu ambaye nilihisi atakuwa sawa yangu. Kwa hiyo, niliweza kukataa maombi kutoka kwa wale ambao hajawa watalaka, lakini, kwa udadisi tu, bado niliweza kupata habari zao kupitia kwenye jumuiya na marafiki. Nilianza kutambua kwamba baadhi yao walijulikana kuwa watu wazuri, wapole na wenye kufuata dini – sifa zote zile ambazo tunaambiwa tuzitafute kwa mchumba mtarajiwa. Hakuna mahali popote katika Uislamu ambapo pamependekezwa utafute 'mtalaka' kama sifa, sasa nilikuwa ninafanya nini? Ningewezaje kudai kwamba ninamwachia Mwenyezi Mungu aniongoze kwa mtu ambaye ni sawa yangu ikiwa mimi mwenyewe nilijiwekea masharti na sikutaka hata kuyapatia nafasi ?

Kwenye mkutano wangu wa kwanza na mtu ambaye si mtalaka, moja ya mwanzo niliyomuuliza lilikuwa 'Hivi hukerwi ya kwamba mimi ni mtalaka?' Alinyamaza na akanitazama, akijibu, 'Iwapo Mtume wetu (s.a.w.w.) hakuhisi ilikuwa ni kushusha hadhi yake kuoa mtalaka, sasa mimi nitawezaje!?' Nilitambua jinsi gani nilivyokuwa na mawazo finyu na kejeli yake ni kwamba kwenye mazingira ambayo mimi nilidhani kuwa ningeonekana kuwa niliolewa kabla, kwa kweli ilikuwa ni mimi ndiye ambaye nilikuwa nikiwatambua watu wengine kuwa hawajafunga ndoa hapo kabla."



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 146 10/20/2015 4:32:08 PM

**Vikwazo Vinavyowezekana kuwepo:**

**1. Wewe**

Kama utakavyokuwa unapita kwenye mlolongo tena, ni kawaida tu kwamba wewe mwenyewe utakuwa beuzi na kwa jumla mchache wa kuamini. Kwa sababu ya matokeo mabaya yaliyopita utaelekea kuwa mwangalifu zaidi na pia utadhamiria kutokuthubutu kufanya kosa tena. Hata hivyo, kuwa na utambuzi kuhusu hisia hizi inaweza kukusaidia wewe kuzidhibiti na kutoziruhusu kuathiri mno maamuzi yako utakayoyafanya. Ndiyo, utapenda mambo yawe kamilifu zaidi ili usije ukateseka tena, lakini bahati ya kumpata mtu ambaye atakuwa na 100% ya yale unayoyataka wewe haina muelekeo kabisa! Kuwa mwangalifu, lakini isiwe wa kuzidi mno.

**2. Familia:**

Wakati ambapo familia yako kwa jumla wakiwa na nia njema, wanaweza wakasema mambo ambayo yanaweza kukuumiza zaidi kuliko kukusaidia, hususani kwa wanawake. Mifano inajumuisha, ‘Usiwe na wasiwasi kwani angalau unayo kazi ambayo unaitegemea au “Unaweza kujichunga mwenyewe’. Hatari iliopo kwenye maana ya maneno haya kama yanavyochukuliwa na watalaka ni kwamba wanaweza wasifunge ndoa tena. Chukua ushauri huo kwa uangalifu mkubwa sana, wanafikiria maslahi yako mema nyoyoni mwao; kuyaacha maoni hayo yapite bila kuyazingatia sana inaweza kuwa njia bora sana kuelekea mbele .

**3. Mawazo ya watu wengine:**

Pamoja na familia, watu wengine wanaweza kusema mambo ambayo yanaweza kuumiza. Kama kwa familia, yachukulie mambo kwa wepesi na usiyafikirie sana. Usiruhusu mawazo kama hayo



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 147 10/20/2015 4:32:08 PM

kukushusha na kukufanya uwe na kinyongo au kukuteketeza. Omba msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu akusaidie katika hili.

'Usifikirie sana kuhusu jambo hili!' ni mojawapo ya mawazo kama hayo unayoweza kusikia tena na tena. Ndiyo na hapana. Ndiyo kwa maana ya usizingatie sana maoni hayo, na jaribu kusonga mbele. Hapana kwa maana ya kwamba usiyafukie moja kwa moja; unahitaji kushughulikia talaka yako ili uweze kusonga mbele.

**Viashirio Vyenye Msaada:**

**1. Kipindi cha Katikati**

Baada ya talaka yako, usiangukie kwenye mtego wa kuwa mwenye kinyongo na kuwaelezea watu kuhusu mtalaka wako na talaka juu ya talaka hiyo. Kuwa na mwenendo mwema, ujiamini na ukatae kuonekana mnyonge au kuwa mpweke na kujifikiria binafsi tu. Msimamo utakaochagua kuufuatisha utakuwa na athari juu ya mahusiano yako ya siku za usoni. Onyesha kwamba umejifunza mambo na umekuwa mtu bora zaidi.

**2. Uwe Mng`ang`anizi:**

Kufunga ndoa mara nyingine tena ni kugumu kuliko ile ndoa ya mara ya kwanza. Kushikilie na uwe na imani. Fanya mahesabu-linganisha ni ndoa ngapi zilizopo ambazo zimefanikiwa zikilinganishwa na ndoa zilizovunjika, na hususani fikiria zaidi wale watalaka ambao wamesonga mbele na kufanikiwa kufunga ndoa tena - wapo wanamume/wanawake wazuri na wanaostahili wengi na Inshallah utampata mmoja.

**3. Upende vitendo:**

Endapo unaona kwamba haukabiliwi sana, usikate tamaa. Inawezekana tu kuwa kwa sababu watu hawajui kama wewe upo



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 148 10/20/2015 4:32:08 PM

‘tayari’ kusonga mbele, hususani kama talaka ni ya hivi karibuni. Au inawezekana kuwa baadhi ya watu wanajihisi vibaya ya kulikabili suala hili nyeti na wewe. Kwa hiyo dhima ipo kwako, katika masuala mengi, kuwaendea wazazi wako na kuwaambia kwamba sasa upo tayari, au hata wewe kwa bidii ya kuwaendea washenga na ujaribu kuwaulizia uone kama wanaye mtu wanayemfikiria. Hii ndio hali halisi, uwe ni mwanamume au mwanamke; zingatia mfano wa Bibi Khadija na Mtume Muhammad (s.a.w.w.), ulisimuliwa kwenye sura zilizopita.

### 4. Mfumo Saidizi:

Umuhimu wa mfumo saidizi haupaswi kupuuzwa. Mfumo huu wa usaidizi kwa kawaida unakuwepo katika muundo wa familia yako, lakini pale ambapo haupo, jumuiya inapaswa kwa ukamilifu kabisa kuweka ‘kundi’ lenye makao malumu au msaada wa namna fulani. Usiogope kupata msaada; kutegemea na nini kilichotokea, tafuta ushauri kama ni lazima. Hii itakusaidia kupunguza mzigo, ambako, kama ilivyotajwa huko juu, ni muhimu kabla ya kujaribu kukutana na mtu.

### 5. Omba, omba, omba du’a!

Usiibeze nguvu ya du’a - omba, omba na kuomba zaidi na zaidi. Usijali kiasi gani utazungumza na mtu kuhusu hili, unayeweza kumgeukia, Yule ambaye anaelewa kwa ukamilifu ni Mwenyezi Mungu. Du’a zilizomo ndani ya *Sahifa Sajjadiya* ni kwa matokeo mazuri/kuomba kile kilicho bora zaidi ni muhimu kwa ajili ya kuielekeza akili.

Tafadhali pia rejelea Sura ya 10 na 14 ndani ya kitabu hiki juu ya Kumtegemea Mwenyezi Mungu na Kuwa na Imani.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 149 10/20/2015 4:32:08 PM

**Mkutano:**

**Kuijadili hiyo Talaka**

Bila shaka kila mtu utakayekutana naye atakuwa na maswali na anastahili kupata majibu kamili; kwa hiyo, unahitaji kuwa na uwezo wa kuzungumzia juu ya hilo. Hata hivyo, katika mkutano wa kwanza, inaweza kuwa ni fikira nzuri kutozama kwa kina kwenye maelezo; mhakikishie mtu huyo uliye naye kwamba suala hili limekwisha, na badala yake muelekeze mazungumzo kwenye masuala ya mchukuano baina yenu. Halafu, endapo mambo hayaendi mbele, utakuwa umepunguza sana ufichuaji wa melezo yako binafsi.

Endapo mambo yataendelea vizuri, unaweza kuzungumzia mambo kwa kina zaidi. Hata hivyo, usihisi kuhitaji kujitetea - baadhi ya watu wanaweza kutumia muda wote wa mkutano wakiielezea talaka, hata baada ya miaka mingi baada ya tukio hilo! Usimruhusu mtu huyo kuona upande wa machungu yako.

Juu ya upande wa kutojiandaa, wewe unaweza kuwa umekubali lakini yule mtu ambaye unayekutana naye atakuwa na maswali elfu moja; jaribu kujibu maswali kwa ufasaha kwa kiasi unachofikiri ni sawa, na jaribu kupata njia ya kuendeleza mazungumzo. Ulikuwa mtu kamili kabla ya kuwa mtalaka; jaribu kumfanya yule mtu unayekutana naye apate kukujue wewe ni NANI - kwamba wewe ni zaidi ya kuwa nembo tu.

**Ushauri:**

Endapo wewe ni mtu ambaye hujapata kuwa na uhusiano kabla ya hapo na sasa unakutana na mtalaka, ushauri wetu kwako unafuata mwelekeo ule ule kama huo hapo juu; usilenge kwenye ushauri huo kwenye mkutano wa kwanza kwa kiasi chochote cha udadisi utaka-



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 150 10/20/2015 4:32:09 PM

oweza kuwa nao. Mjue mtu kwanza bila kumhukumu kwa ule ukweli kwamba yeye ni mtalaka. Kuwa mpole katika kuuliza maswali, usijihisi kustahili kujua maelezo yote, na yote kwa mara moja.

Usiamini tetesi zozote au udaku ambao utakuwa umesikia, lakini si vibaya kufanya utafiti kutoka kwenye vyanzo vya kuaminika juu ya nini kilitokea. Wakati huohuo, usiwe mjinga, kama jambo fulani halielekei kuwa sahihi kuhusu 'taarifa' basi unayo haki kabisa ya kuulizia zaidi na kutathimini.

## Kufanya Uamuzi

### Nitajuaje?

Mbinu zilezile za kuamua kama mtu huyo ni 'sawa yako' au hapana ambazo zimeelezewa ndani ya Sura ya 8 pia zinatumika hapa.

### Kuweka Mambo Sawa

Ni muhimu kutahadharisha hapa kwamba mtu awe mtalaka au hapana, huu bado ni uamuzi muhimu sana ambao kwa dhahiri unabadilisha maisha. Usihisi kwamba utatakiwa kuweka mambo sawa au kuafikiana, au kwamba wewe upo kwenye nafasi ndogo sana ya kutaka kitu. Kwa hiyo wakati hupaswi kuzidi mno katika hali ya kutaka ukamilifu, usijiendee tu kwa yeyote yule anayekutaka wewe lakini uwe na uhakika kwamba upo ulinganifu baina ya nafsi na akili yako.

### Mawasiliano:

Kujiweka katika taratibu za mawasiliano baina yenu wawili ni nyenzo ya manufaa sana katika kuwawezesha kufanya uamuzi sahihi.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 151 10/20/2015 4:32:09 PM

Kuwa na uwezo wa kuzungumzia maoni yenu na hisia zenu katika hatua hii pia ni ishara nzuri ya uhusiano wenu utavyokuwa baada ya kuoana, endapo uamuzi ni 'ndiyo!'

**Uhusiano Mpya**

Baada ya kufunga ndoa tena, makubaliano na kuvumiliana ni mambo yanayohitaji kuendelezwa. Uwe tayari juu ya ndoa yako ya zamani kutokeza mara kwa mara, lakini usirejelee kwa mwenza wako wa zamani kila siku! Hata hivyo, endapo kutajitokeza jambo, unapaswa kuhisi kutulia vya kutosha kulizungumzia na mwenzi wako. Jaribu kuepuka kulinganisha kwenye akili yako na hasa usitamke kwa sauti. Pamoja na kwamba mwanzoni ni jambo la kawaida kufanya, baada ya muda kupita tabia hii itatoweka endapo kama huiendekezi.

Mazoea na mafungamano kati yenu yanaweza yasiwe na nguvu moja kwa moja tangu mwanzo; mnahitajika kuyafanyia kazi kwa sababu yaliyopita yanaweza kuwa yamekufanyeni kuwa waangalifu zaidi; pia mnaweza kuwa na umri mkubwa zaidi na hivyo, kujizatiti zaidi katika tabia zako, hali ambayo itakusababishia ugumu kidogo katika kujirekebisha, lakini si kwamba haiwezekani.

Pia tahadhari kuhusu jinsi ambavyo mambo ya zamani yamekuathiri wewe; mathalani, unaweza kuwa mkosoaji kupita kiasi wa masuala ambayo yatatokeza kwenye ndoa mpya ambayo huenda yalitokea kwenye ndoa ya zamani. Au unaweza kuwa mwepesi kuhisi zaidi mambo mengine, hapa tena ni kwa sababu ya yale yaliyotokea kabla. Utambuzi wa hili utakushawishi kurudi hatua moja nyuma na kujibu kwa namna yenye uhalisi, badala ya kujibu kutokana na silika na uchungu.

Kwa ujumla, na kwa ndoa za kwanza vilevile, ujiandae kuwa tayari. Usiyachukulie mambo kibinafsi na usilifanye suala kuwa



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 152 10/20/2015 4:32:09 PM

jambo ambalo si lenyewe; lichukulie suala hilo kwa kulidhibiti, lizungumzie, lifanyie kazi, halafu songa mbele.

"Wakati ambapo sote wawili (watalaka) tulikuwa tunajiamini zaidi kwenye mkutano wetu wa kwanza, jambo hili halikuwa hivyo ilipofikia wakati wa kufanya uamuzi. Wote wawili tukawa watu wa kujaribu, na pamoja na kuhisi uhakika, wale mashetani wabaya walikuwepo hapo. Na ulipofikia wakati wake, ilikuwa vigumu sana kuacha kudhihirisha. Tulishinda vipi? Tuliweka mawasiliano waziwazi. Wakati wa kufanya uamuzi ulipofika, tulilizungumzia jambo hili sisi wawili, kwa faragha baina yetu. Kwa kufanya hivyo, tuliweza kuzungumzia wasiwasi wetu, tulizungumzia hofu zetu kwa hali ya dhati iliyo makini, na tulifuta uwezekano wowote wa kuonyesha hisia kali ambazo zingeweza kuwepo.

Tunahisi huu ni utaratiaabu mzuri kwa ajili ya hali ambapo ama mmoja au wote wanaohusika ni watalikiwa. Mheshimiane, jizuieni kuhukumiana, na zaidi ya yote, jitolee kusaidia katika kipindi hicho - msaada huohuo ambao labda ungetoa wakati wa ndoa. Tulichukua muda wa kulala nalo tukilitafakari, na wakati wa usiku huo tuliomba kwa nyoyo zetu zote kwa ajili ya muongozo na uwazi. Ni vigumu kuelezea hizo hisia; najua kwamba nilihisi kuchukuana kikamilifu na mtu huyu, kama vile kitu fulani ndani kabisa nafsini mwangu kilitambua kitu fulani ndani mwake. Ama tulikuwa pamoja ana kwa ana au kuongea kwenye simu, nilihisi utulivu mkubwa na ushwari ulio kamilifu. Bado palikuwepo hii hofu nzito ya udanganyifu. Unapofika wakati wake, unapaswa kuchangamkia tu - na kuhusu sisi wote kuwa ni watalaka, kuweza kuzungumzia jambo hilo ilikuwa na maana kwamba tulikuwa tunaweza kuchukua hatua hiyo ya imani pamoja." **Mwanamke, Canada**



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 153 10/20/2015 4:32:09 PM

# SURA YA 16

# MIKATABA

## MIKATABA KATIKA UISLAMU

Wakati wa uchumba, utaratibu wa Mut`a au Ndoa ya daima unaweza kusomwa. Haya yamezungumziwa zaidi hapo chini, na dhana ya Mahari pia imetazamwa kwa kina. Mikataba inayofanyika kabla ya ndoa pia itazungumziwa.

### Mut`a (Ndoa ya Muda)[71]

Kama ilivyotamkwa awali, kwenye matukio mengi zaidi, wanandoa watarajiwa husoma utaratibu wa Mut`a, wakiwa wanatambua kwamba ndani ya kipindi fulani cha muda, watakuwa wanafunga ndoa ya kudumu.

Ndoa ya Mut`a ina masharti mbalimbali ambayo lazima yafuatwe, ambayo miongoni mwao tunasisitizia yaliyo muhimu zaidi:

1. Kama msichana ni bikira, basi lazima apate kibali cha mlezi wake kabla ya ndoa ya Mut`a kufungwa. Mlezi wake ama ni baba yake au babu yake wa upande wa kiumeni. Kama hawa wawili watakuwa hawapo, basi hatahitaji ruhusa.

2. Kipindi cha muda na mahari lazima vitajwe na kukubaliwa na pande zote mbili kabla ya utaratibu wa ndoa ya Mut`a hau-

[71] Kitabu cha Muongozo wa Ndoa za Kiislamu. "*The Islamic Marriage Guidebook*, Islamic Humanitarian Service (www.al-haqq.com)"



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 154 10/20/2015 4:32:09 PM

jasomwa, vinginenyo ndoa hiyo itakuwa batili. Kulingana na ukomo wa muda wa ndoa ya Mut`a unavyohusika, haitoshi kusema kitu kama 'Mut`a itakuwa halali hadi tutakapooana kwa ndoa ya kudumu' – badala yake, tarehe halisi lazima itajwe.

**3.** Wahusika wanaweza kuwekeana masharti, kama vile kusema hapatakuwepo na tendo la jimai au masharti mengine – haya pia lazima yatengenezwe na kukubalika kabla ya utaratibu huo kusomwa. Hata hivyo, endapo baadaye pande zote mbili zinakubaliana kubadili masharti yoyote yaliyokubaliwa, wako huru kufanya hivyo. Hata hivyo, kwenye mazingira haya, kama msichana ni bikira basi mabadiliko haya lazima yafanyike kwa ruhusa ya mlezi tena.

**4.** Tamko lazima lisomwe sawasawa kwa lugha asili ya Kiarabu na kama hii haiwezekani basi mwakilishi ambaye anaweza kusoma kwa Kiarabu sahihi anapaswa kusoma utaratibu ya Mut`a. Kama hii pia haiwezekani basi chaguo la tatu ni msichana na mvulana wanaweza kusoma tafsiri ya utaratibu wa Mut`a kwa lugha yao, lakini lazima wahakikishe kwamba utaratibu huo unabeba maana ileile iliomo kwenye lugha asili ya Kiarabu.[72]

**5.** Endapo wachumba wanaamua kuoana kwa ndoa ya kudumu kabla ya muda wa ndoa ya Mut`a kwisha, mume lazima 'afute' muda uliobakia wa Mut`a kwa mkewe. Mara likifanyika hili, basi ni hapo tu ndipo wanaweza kuoana kwa ndoa ya kudumu. Kama wenza wapo katika ndoa ya muda na halafu wakajaribu

---

72 Tafadhali zingatia kwamba haya ni kufuatana na fatwa ya Ayatullah al-Uzma al-Hajj as-Sayyid as-Sistani. Muqallidina wa Marajai wengine wanapaswa kuangalia hukmu zao juu ya haya na masuala mengine yaliyomo kwenye mazungumzo haya.



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 155 10/20/2015 4:32:09 PM

kuoana kwa ndoa ya kudumu ambapo muda wa ndoa ya muda haujaisha, basi ndoa yao ya kudumu itakuwa imebatilika, na katika kukamilika muda wa ndoa ya muda, hawatawekwa kwenye kundi la watu waliooana.

**Kusoma tamko la Mut`a:**[73]

Kwenye mfano uliopo hapo chini, tutadhania kwamba watu wanaohusika wanasoma tamko lao la Mut`a wenyewe (badala ya kuwa na mwakilishi wa kila upande):

Bibi harusi mtarajiwa anapaswa kusema:

زوجتك نفسي للمدة المعلومة على المهر المعلوم

**Zawajtuka linafsi fil muddatil ma`luumati `alal mahril ma`luum.**
**"Nimekuoza nafsi yangu kwa muda maalum na kwa mahari maalum"**

Bwana harusi matarajiwa atajibu:

قبلت

***Qabiltu***

"Nimekubali"

(Tafadhali zingatia kwamba sharti la msingi la nia, wakati "Nimekubali" inapotamkwa na mwanamume, ni kwamba tamko hili lazima lisomwe kwa nia ya **"Insha"** – hili ni neno la kisheria katika Sheria ya Kiislamu ambalo lina maana kwamba kupitia huko kusomwa tamko la ndoa, uhusiano utakuwa umeanzishwa baina ya watu wawili ambao haukuwepo kabla ya kusoma tamko hilo).

[73] *Islamic Laws*, (Sheria ya Kiislamu, Kanuni 2378)



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 156 10/20/2015 4:32:09 PM

**Ndoa ya Kudumu**[74]

Kwa kulingana na desturi ya kudumu milele ya Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w.) katika mtindo wa kusoma tamko la ndoa ya kudumu, kama alivyofanya wakati wa ndoa ya binti yake Fatimah, (s.a.) kwa Ali ibn Abi Talib (a.s.) sherehe inatanguliwa na khutba au utangulizi wa kutukuza Upweke wa Mwenyezi Mungu na sifa Zake, na halafu kumsalia na kumtakia rehma na amani Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) na watu wa nyumba yake (a.s.). Mara baada ya kusomwa haya, taratibu halisi ya tamko la ndoa inasomwa

Kwa mujibu wa Ulamaa wetu walio wengi, tamko lazima lisomwe kwa lugha sahihi ya Kiarabu. Hata hivyo, Ayatullah al-Uzma Sayyid Ali al-Husaini as-Sistani, kwenye kitabu chake cha hivi karibuni kiitwacho "*A Code of Practice for Muslims in the West*", anasema kwamba kama mwanamume au mwanamke hawezi kusoma Kiarabu kwa usahihi, basi wanapaswa kuteua mwakilishi ambaye angeweza kusoma tamko kwa niaba yao. Na kama hili pia haliwezekani, basi wanaweza kusoma tamko kwa lugha ya kwao (tafsiri) alimuradi maana inabaki ileile kama ilivyo kwenye Kiarabu.

Inapendekezwa kwamba tamko la ndoa lisomwe wakati wa usiku,[75] na pawepo na mashahidi. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema pia kwamba: "Tangazeni ndoa hii na ifanyike ndani ya msikiti."[76] Haipendezi kusoma tamko la ndoa wakati wa '*Qamar dar Aqrab*,' wakati mwezi unapita kwenye hatua ya 'nge' *Scorpio*.[77]

---

[74] Yamechukuliwa zaidi kutoka kwenye *The Islamic Marriage Guidebook* 'Kitabu Cha Muongozo wa Ndoa za Kislamu', Al-Haqq Publications

[75] *Halliytul Muttaqin*, uk.108-109

[76] *Kaz al-Ummal*, Na. 44536

[77] *Hallyatul Muttaqin*, uk. 108-109



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 157 10/20/2015 4:32:09 PM

**Usomaji wa tamko la ndoa:**

Tutachukulia kwamba wahusika watasoma tamko la ndoa yao wao wenyewe (kinyume na ile ya kuwa na mwakilishi wa kila upande):

اعوذ بالله من الشيطان الرجيم
بسم الله الرحمن الرحيم

Najikinga kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya Shetani aliyelaaniwa.

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

الحمد لله إقراراً بنعمته ولا إله إلاّ اللـه إخلاصاً لوحدانيته وصلى اللـه على محمد سيد بريَّته والأصفياء من عترته

Sifa Zote ni Stahiki Yake Mwenyezi Mungu kwa kutambua fadhila Zake, na [tunashahidilia] hakuna Mungu ila Mwenyezi Mungu kwa utiifu mkamilifu kwenye Upweke Wake; Mwenyezi Mungu amrehemu Muhammad, wa kwanza kabisa katika viumbe Vyake, na watu watakatifu wa nyumba yake [Muhammad].

أما بعد : فقد كان من فضل اللـه على الأنام أن أغناهم بالحلال عن الحرام ، فقال سبحانه :

وَأَنكِحُوا الأَيَامَى مِنكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ عِبَادِكُمْ وَإِمَآئِكُمْ إِن يَكُونُوا فُقَرَآءَ يُغْنِهِمُ اللـه مِن فَضْلِهِ وَاللـه وَاسِعٌ عَلِيمٌ وقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: النِّكَاحُ مِنْ سُنَّتِي ، فَمَنْ رغب عن سُنَّتِي فَلَيْسَ مِنِّي ،

Hivyo basi: Miongoni mwa fadhila za Mwenyezi Mungu kwa watu ni kwamba Amewapa wao njia halali (za maisha) ili kuwakinga na yale yaliyoharamishwa. Na Yeye, Aliyeko Juu Zaidi, amesema, "Waozeni wale ambao hawakuolewa miongoni mwenu na waadilifu miongoni mwa watumwa wenu wanamume na watumwa wenu wanawake. Kama wao ni fukara Mwenyezi Mungu atawatajirisha kutokana na neema Zake, na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa rehema, Mwenye kujua". Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema, "Miongoni mwa sunnah zangu ni kuoa. Kwa hiyo yeyote anayekataa kufuata (sunnah) yangu huyo hatokani nami (taifa langu)."

| | |
|---|---|
| 1a) Bibi harusi mtarajiwa atasema: | أنكحت نفسي لك على المهر المعلوم |
| 1b) Bwana harusi mtarajiwa atasema: | قبلت النكاح لنفسي على المهر المعلوم |
| 2a) Halafu, bibi harusi mtarajiwa atasema: | زوجت نفسي لك على الصداق المعلوم |
| 2b) Halafu, bwana harusi mtarajiwa atasema: | قبلت التزويج لنفسي على الصداق المعلوم |
| 3a) Bibi harusi mtarajiwa atasema: | أنكحت و زوجت نفسي لك على المهر المعلوم |
| 3b) Bwana harusi mtarajiwa atasema: | قبلت النكاح والتزويج لنفسي على المهر المعلوم |



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 159 10/20/2015 4:32:09 PM

Mistari hii hurudiwa mara mbili au mara tatu kwa ajili ya tahadhari kuhakikisha imesomwa inavyofaa. Baada ya kusomwa mistari hii michache, mwanamume na mwanamke wanaunganishwa pamoja kufuatana na sheria za Uislamu. Hakuna 'sherehe' nyingine inayohitajika - chakula (waliimah) wanachopewa wale waliohudhuria kinapendekezwa, lakini mambo mengine ni sehemu ya mazoea ya kitamaduni.

## Mahari - Zawadi kwa Mke[78]

Mahari kama linavyotafsiriwa kwa kawaida - ni sehemu isiyotenganishika na ndoa na masharti yake. Mahari ni lazima iainishwe na kukubalika kabla ya ndoa, ni zawadi kwa mke na kwa vyovyote haiwezi kutafsiriwa kama bei au thamani ya mwanamke.

Kwa kuchunguza hadithi za Kislamu, tunaona kwamba si lazima fedha au dhahabu au vitu vya kimaada vitolewe kama mahari - badala yake, kitu chochote ambacho mwanamke ataomba na mwanamume anakubali inachukuliwa kuwa ni mahari. Ni kwa sababu hii tunaona kwamba wakati wa Mtume (s.a.w.w.) mwanamume alimuoa mwanamke na mahari yake ni kwamba angemfundisha Qur`ani. Kuna mifano mingi kama huu katika historia ya Waislamu ambapo Mahari ilikuwa ama kiasi kidogo sana au zawadi isiyokuwa ya kimada.

Kwa bahati mbaya, kwenye jumuiya nyingi siku hizi, mwelekeo umekuwa kuweka kiasi kikubwa cha fedha, vito, dhahabu, na bidhaa zingine kuwa ndiyo Mahari - ambapo katika Uislamu, kitendo kinachopendekezwa ni kuweka kiasi 'kidogo' au cha kati kuwa Mahari hivyo kwamba mume mtarajiwa asiwekwe katika hali ya ugumu wa kulipa na hivyo, Mahari kubwa kwa kweli ni makuruhu

[78] *The Islamic Marriage Guidebook*, Islamic Humanitarian Service (www.al-haqq.com)



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 160 10/20/2015 4:32:09 PM

(jambo lisilopendeza) au linalojaribu kuzuiwa kabisa. Hata hivyo, Mahari haitakiwi kuwa ndogo sana hivyo kwamba haiwezi kumpa mke ulinzi wowote au msaada endapo mambo yanaharibika.

Kwa mujibu wa wanazuoni, endapo kama mahari imewekwa kwa kiwango ambacho kwamba hata mnamo siku za usoni mwanamume hataweza kuilipa, au kama mwanamume hana nia ya kulipa mahari, basi uhalali wa ndoa hiyo upo mashakani.

Mume na mke wanaweza kukubaliana muda ambao mume atalipa Mahari na kama ambavyo imekwishasemwa kwenye vitabu vya sheria za Kiislamu, kama mke akidai fedha hiyo baada ya muda wake stahiki kufika, basi inakuwa ni wajibu kwa mume kulipa hata kama ikimaanisha kwamba ni lazima achukue mkopo. Kama hatalipa ambapo uwezo wa kulipa anao, basi atakuwa amefanya dhambi na atawajibishwa na Mwenyezi Mungu.

Kuhusu Mahari na umuhimu wake, Imam Ali (a.s.) amesema: "Hii (Mahari) ni sharti muhimu kuliko masharti mengine, ambapo kupitia humo ndipo sehemu za siri zikaweza kufanywa kuwa halali kuruhusiwa juu yako.

Tunahitimisha sehemu hii juu ya umuhimu wa Mahari kwa onyo kali kutoka kwa Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w.) kuhusu wanamume hao ambao hukataa kuwapa wake zao kile walichoahidi kuwapa:

"Mwanamume ambaye anamdhulumu mke wake kuhusu Mahari anachukuliwa kama mzinzi mbele ya Mwenyezi Mungu. Mnamo siku ya Hukumu, Yeye atamwambia mtu huyo, 'Ee Mja wangu! Nilikuoza wewe kwa mja wangu mwaminifu juu ya ahadi Yangu na ulimdhulimu mja wangu mwaminifu.' Wakati huo Mwenyezi Mungu atachukua amali zote nzuri za mwanamume huyu na atampa mwanamke huyo kulingana na haki yake kwamba alichukua

(Mahari). Itakapokuwa hakuna amali zozote njema zinazobakia, basi Mwenyezi Mungu atamuamuru kwenda Jahannam pamoja na watu wengine ambao walivunja ahadi zao. Mwenyezi Mungu amesema, 'Na kuweni waaminifu katika ahadi zenu. Hakika ahadi ni kitu ambacho (wewe) utaulizwa."

## Mikataba ya Kabla ya Ndoa.[79]

Mikataba ya ndoa bado halijawa jambo la kawaida katika jumuiya yetu, lakini ni suala ambalo linahitaji kuzungumziwa ili kwamba watu waweze kufanya uamuzi wenye ujuzi.

Lengo la ujumla la mikataba ya ndoa ni kueleza bayana haki fulani ambazo zitajitokeza kama ikitokea wanandoa kutalikiana. Haki hizi kwa kawaida zimelengwa kuwalinda au kuwanufaisha wanawake.

Kwa desturi kumekuwepo na hoja fulani zinazotolewa dhidi ya mikataba kama hii. Hizi zimedokezwa hapo chini, pamoja na hoja-pinzani, ambazo zinaunga mkono kuwepo kwa mikataba kama hii.

### 1. Mikataba ya ndoa hutoa picha ya ndoa isiyokuwa na matumaini:

Si kila ndoa ni ndoa iliyo kamilika yenye wenza wawili wenye furaha. Si rahisi kwa mtu kuweza kutabiri kabla kama ndoa fulani itavunjika. Juu ya hayo, baadhi ya ndoa huvunjika kwa amani, ambapo katika mifano mingine kutalikiana ni mchakato mgumu. Ni dhahiri kwamba ni jambo lisilowezekana kusaini mkataba wakati wa kutalikiana, kwa hiyo, kimantiki mkataba husainiwa muda mfupi kabla ya harusi Uwepo wa mkataba wa ndoa hauelekei kuzuia ndoa ambayo ingevunjika baadaye; nia ya msingi ni kuongeza vifungu na ulinzi endapo patatokea kutalikiana, badala ya kuzuia talaka.

[79] Imechukuliwa zaidi kutoka kwenye 'Ufumbuzi wa Ndoa' (*Solutions of Marriage*) Sehemu ya 4 ya 4 Shabbir M H Alibhahi, & Fatima Y Alibhai and co.

**2. Mikataba ya ndoa husababisha talaka:**

Hoja hii inashauri kwamba watu wanaosaini mikataba ya ndoa wanaanzisha jambo la urithi wa kisaikolojia ambalo hutengeneza 'njia ya kutokea' kama uhusiano ukiwa na mtafaruku. Hata hivyo, inaweza kuhojiwa kwamba wanamume na wanawake ambao husaini mikataba kwa nia njema watakuwa kama walivyojifunga ya kufanya ndoa yao idumu kama wale ambao hawakusaini mkataba. Hakuna mtu anayeomba talaka. Wala talaka si jambo mbadala rahisi usio na maumivu. Ibara fulani ndani ya mkataba zinaweza hata kufanya talaka kuwa na mvuto dhaifu.

**3. Mikataba ya ndoa hutengeneza vikwazo ndani ya ndoa:**

Mikataba imebuniwa ili itumike pale tu ambapo ni muhimu. Ibara hazikubuniwa ili zitumike kumuadhibu yeyote baina ya wanandoa lakini badala yake ni kusaidia kuepusha migongano panapotokea kutalikiana. Hata hivyo, kama ambavyo imeonyeshwa kabla, uwepo wa mkataba uliosainiwa wenyewe unaweza ukaongeza nafasi ya kwamba utatumika mahali pa ile njia mbadala nyingine, ambayo ingekuwa ni kutafuta ushauri wa kitaalamu, kutathimini malengo na shabaha upya na kufanya sadaka. Ufumbuzi moja ni ibara ambamo wenza wote wawili wanakubaliana kuhusu kipindi cha ushauri kabla ya kufikiria kutalikiana.

**4. Mikataba ya ndoa humpendelea mke:**

Pamoja na kwamba Uislamu kwa ujumla unaunga mkono ukweli kwamba wanamume na wanawake ni sawa mbele ya Mwenyezi Mungu, jamii, ama ya Magharibi au Mashariki, hazioni hivyo. Hakuna shaka kwamba mikataba imeundwa kwa msingi hasa kumlinda mke. Hii ni kwa sababu tu kwamba mke anaelekea kuwa dhaifu katika talaka kuliko mume. Hoja hii inaungwa mkono na mazoea ya kihistoria na ushahidi wa hadithi fupi. Hali hii ni ya kweli zaidi



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 163 10/20/2015 4:32:09 PM

pale ambapo mwanamke hana chanzo chake mwenyewe cha maana cha kumpatia kipato.

**Mkataba wa Kabla ya Ndoa Una Nini?**

Kutokana na mazungumzo ya hapo juu, ni dhahiri kwamba yapo mambo mazuri na mabaya ndani ya mikataba ya ndoa. Kabla ya kuamua iwapo pawepo na mkataba wa ndoa au hapana, ni muhimu sana kuelewa mkataba unaahidi nini. Kwa vyovyote orodha ya mada haikukamilika; inawezekana yapo mambo ambayo hayakutiliwa maanani. Hata hivyo, hapa chini yapo mambo muhimu ambayo mara nyingi huwekwa kwenye mikataba:

**1. Haki ya Talaka:**

Katika desturi ya Kislamu, haki ya kutaliki kimsingi ni ya mume. Mkataba unaweza kuruhusu, ikichukuliwa kwamba wote wawili mume na mke wanakubaliana, kwamba yeyote kati ya wao wawili anaweza kuwa na haki ya kutaliki. Inawezekana pawepo na ibara na masharti muhimu pale ambapo mmojawapo wa wanandoa anaweza kuanzisha mchakato wa talaka, na kwa pamoja mwanasheria na mtaalam wa kidini wanapaswa kuombwa ushauri wakati wa kutengeneza mkataba.

**2. Haki ya Kuoa Mke Mwingine:**

Uislamu unamruhusu mwanamume kuoa hadi wake wanne kwa ndoa ya kudumu. na wake wengi wa ndoa ya Mut`a kadiri atakavyo hiari mwenyewe, bali ikiwa na mipaka kama ilivyoelezwa bayana ndani ya Sheria ya Kislamu. Hata hivyo, mwanaume hahitaji kumtaarifu mkewe kuhusu hizi ndoa zinazofuatia. Mkataba unaweza kutaja kwamba mume hawezi kuoa mke mwingine bila ruhusa ya mkewe aliyenaye wakati bado ndoa yao inaendelea. Pia panaweza kuwe-



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 164 10/20/2015 4:32:09 PM

po vifungu kadhaa kwa ajili hili (yaani mume anaweza kuoa mke mwingine endapo mke wake ni mgumba, kama akipata ulemavu wa akili, na kadhalika.) Jambo moja muhimu la kuzingatia ni kwamba mkataba hauwezi, kufuatana na fatwa za wanazuoni wa Kislamu, kubatilisha haki ya mwanamume kuoa mke mwingine. Badala yake mkataba ungeweza kumruhusu mwanamke kuwa na haki ya kuomba talaka bila ya kwenda kwa mwanasheria au mwakilishi wake kuitekeleza talaka kisheria. Nje ya mkataba wa ndoa, mwanamke wa Kiislamu hawezi kumuomba talaka mume wake kwa sababu tu, ameoa mke wa pili.

### 3. Malezi ya Mtoto/Watoto:

Endapo kuna watoto ambao wamezaliwa wakati wa ndoa yao, basi suala la malezi ya watoto hawa litakuwa ni jambo kubwa endapo wazazi watatengana ama kuachana. Uislamu unatoa haki ya malezi ya mtoto ambaye umri wake ni angalau miaka miwili kwa baba, ambapo mahakama za Kimagharibi hutoa haki hii kwa mama. Hivyo, endapo wenza hao hawawezi kukubaliana kuhusu haki za malezi ya watoto, wangeweza kuainisha kwa njia ya mkataba, kama ni mahakama ya Kiislamu au mahakama ya serikali ya mtaa inayopaswa kuamua. Kama hakuna mbinu kati ya hizi iliyobainishwa, mmojawapo wa watalaka anaweza kuchagua mahakama ya Kiislamu ndiyo ishughulikie shauri ambapo mwingine anaweza kuchagua mahakama ya serikali ya mtaa iamue shauri hilo. Hii husababisha kiasi fulani cha msuguano na adha ndani ya familia. Wapinzani wa mikataba wanasema kwamba kama wenza wa Kiislamu wamekubali kuoana kwa sheria ya Kiislamu, wanapaswa kutalikiana kwa sheria za Kiislamu na kukubali matokeo yake. Hata hivyo, tunajua baadhi ya mifano ambayo mmoja au mwingine kati ya wenza haridhiki na uamuzi wa kidini na anatafuta marekebisho kwenye mahakama ya kisekula, na kusababisha matatizo makubwa juu ya wazazi na watoto.

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
   ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 166 10/20/2015 4:32:09 PM

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema

89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali (as)
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 169 10/20/2015 4:32:09 PM

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l’Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Tawhiid Na Shirki katika Qur’ani Tukufu
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Kishia (Al- Muraja’aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 172 10/20/2015 4:32:09 PM

213. Imam Ali (as) na Mambo ya Umma
214. Imam Ali (as) na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
227. Yafaayo kijamii
228. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
229. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
230. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
231. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya Kiislamu
232. Imam Mahdi Na Bishara Ya Matumaini
233. Jihadi
234. Majanga Na Jukumu La Jamii
235. Muhadhara wa Maulamaa
236. Mashairi ya Kijamii
237. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
238. Mwanamke Katika Harakati za Mageuzi
239. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
240. Yusuf Mkweli
241. Hotuba Za Kiislamu na Haki Za Binadamu

242. Ugaidi wa Kifikra katika Medani ya Kidini
243. Imam Mahdi (as) – Imam wa zama hizi na Kiongozi wa Dunia
244. Imam Mahdi (as) ni Tumaini la Mataifa
245. Imam Husein (as) ni Utu na Kadhia
246. Talaka Tatu
247. Uswalihina Dhahiri na Batini yake
248. Upotofu ndani ya kitabu cha mitaala kwa Shule za Sekondari juu ya Uislamu
249. Imam Husein (as) ni Kielelezo cha kujitoa Muhanga na Fidia
250. Uislamu wa Shia

## KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Ya Muhammadi (s.a.w.w) Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique



44_14_KUCHAGUA MCHUMBA _20_Oct_2015.indd 174 10/20/2015 4:32:10 PM